VOLUME III

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2020—2025)

## TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

VOLUME III

**JUNI 30, 2021**

# YALIYOMO

1. YALIYOMO………………………………………………… 1

2. UTANGULIZI ……………………………………………… 2

3. MIRADI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020-2025
*(TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021)*

3.1 MIRADI YA ELIMU…………………………………………… 5

3.2 MIRADI YA AFYA……………………………………………91

3.3 MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI………………105

3.4 MIRADI YA MAJI ……………………………………………123

3.5 MIRADI YA UJENZI WA BARABARA ………………........131

4. KAMPENI ZA UCHAGUZI & UELIMISHAJI WA

VIPAUMBELE VYA JIMBO LETU …………………………135

5. MENGINEYO ………………………..…………………..169

6. HITIMISHO ……………………………………………………175

7. SHUKRANI ……………………………………………………177

## UTANGULIZI

Kitabu hiki ni moja ya chapisho linalotoa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kuanzia Mwaka 2020 hadi 2025

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, ameweka utaratibu wa kuchapisha vitabu vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani za Uchaguzi za CCM ndani ya Jimbo lao kama ifuatavyo:

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020:**

Vitabu viwili (2) vilichapishwa:

(i) Julai 7, 2019 (Volume I)

(ii) June 30, 2020 (Volume II)

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025:**

Mashapisho ya utekelezaji wa Ilani hii ya Uchaguzi yameanza kutolewa kwenye vitabu kama ifuatavyo:

(iii) Juni 30, 2021 (Volume III)

(iv) June 30, 2022 (Volume IV)

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374. Jimbo letu limechagua vipaumbele vitano kutoka ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025. Vipaumbele hivyo ni: (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, (iv) Tabianchi na Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni.

Maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, raslimali watu na taasisi za fedha na uchumi ni nyenzo muhimu zinazohitajika kufanikisha utekelezaji wa miradi inayoibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano.

Wanavijiji kwa kushirikiana na viongozi wao wa ngazi mbalimbali hupendekeza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji yao, na huchangia nguvukazi na mali zao kwenye utekelezaji wa miradi ya chaguo lao. Uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya

wanavijiji unafuata taratibu na sheria zilizowekwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Tano, chini ya uongozi mzuri wa Hayati Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli, na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan zinapongezwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea kuboresha na kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi wa Jimbo hili.

Kitabu hiki (Volume III) ni chapisho linaloelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha (1 Julai 2020-30 Juni 2021). Vilevile, taarifa hii inaonesha michango mingi na mikubwa iliyotolewa na Serikali Kuu, Mbunge wa Jimbo, Wanavijiji, baadhi ya Wazaliwa wa Jimboni mwetu, na Wadau wengine wa maendeleo ya Musoma Vijijini.

Kitabu hiki, kama vilivyo vingine vyote vya taarifa za maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini hugawiwa bure. Haviuzwi!

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU

## (30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)

**Tarehe 30 Juni 2021: Idadi ya shule Jimboni mwetu ni:**
*Shule Shikizi: 12 zinatumika na upanuzi wake unaendelea
*Shule za Msingi: 111 Serikali & 3 Binafsi
Maktaba 2 zimejengwa na zinatumika & 2 nyingine zinajengwa
*Shule za Sekondari: 21 Kata/Serikali, 2 Binafsi & 4 zinajengwa (Kata)
3 zina Maabara 3 (fizikia, kemia na baiolojia)
18 zinaendelea kujenga Maabara hizo

# WANANCHI NA SERIKALI WASHIRIKIANA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA RUSOLI SEKONDARI

Posted on May 16, 2021



*WANAVIJIJI na VIONGOZI wao (akiwemo Diwani wao Mhe Boaz Nyeura) washiriki kwenye ujenzi wa Chumba kimoja cha Darasa cha RUSOLI SEKONDARI*

RUSOLI SEKONDARI ni Shule ya Kata ya Rusoli iliyofunguliwa Mwaka 2010. Kata hii ina Vijiji 3 ambavyo ni: Buanga, Kwikerege na Rusoli.

**IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA**

MWALIMU MKUU wa Sekondari hii, Mwalimu Tausi Juma amesema kuwa Shule ina jumla ya WANAFUNZI 444. Mahitaji ya Vyumba vya Madarasa ni 12 vilivyopo ni 10.

Kutokana na Ufaulu wa Wanafunzi wengi wa Darasa la VII kuongezeka, kuna MIRUNDIKANO mikubwa ya WANAFUNZI madarasani. Kwa mfano, KIDATO cha KWANZA chumba kimoja cha Darasa kina WANAFUNZI 54 badala ya 40!

**MAABARA 3 (Fizikia, Kemia & Bailojia)**

SEKONDARI hii inazo MAABARA zote tatu ambazo vyumba vyake vimo ndani ya JENGO moja.

SERIKALI ilitoa Tsh MILIONI 20 kuboresha na kukamilisha Maabara ya Kemia, na hivi karibuni SERIKALI imetoa tena Tsh MILIONI 30 kuboresha na kukamilisha Maabara ya Fizikia.

**UJENZI WA VYUMBA VIPYA VYA DARASA**

MTENDAJI KATA ya Rusoli, Ndugu Goodluck Mazige amesema WANANCHI WAMEAMUA kujenga VYUMBA VIPYA 3 VYA MADARASA ili kuondoa MIRUNDIKANO ya WANAFUNZI madarasani.

KIONGOZI huyo, na DIWANI wa Kata hiyo, Mhe Boaz Nyeura wamesema wanaanza na ujenzi wa chumba kimoja cha Darasa ambacho kitakamilika kabla ya tarehe 30.5.2021

**MICHANGO YA WANAVIJIJI**

*NGUVUKAZI ya kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

*Tsh 5,000 kuchangwa na kila KAYA ndani ya KATA hiyo ya Rusoli.

DIWANI Mhe Boaz Nyeura anaomba WADAU wa MAENDELEO wakiwemo WAZALIWA na Kata hiyo wajitokeze na kuchangia ujenzi wa Vyumba Vipya 3 vya Madarasa ya Sekondari yao.

DIWANI huyo anatoa SHUKRANI nyingi sana kwa wanaochangia UBORESHAJI wa MIUNDOMBINU ya RUSOLI SEKONDARI ambao ni:

*WANAVIJIJI wa Kata yao

*SERIKALI yetu

*WAZALIWA wa Kata hiyo ambao ni: Profesa Lawrence Mseru, William Makunja, Berias Mkama, Jeff Makongo, Laiton Samamba, Robert Masige, Majura Maingu, Feada Manyiri na Stephan Kaema.

*YEBHE CHIKOMESHE ni Kikundi cha WAZALIWA wa Kijiji cha Rusoli ambacho KINACHANGIA MAENDELEO ya nyumbani kwao yakiwemo ya Rusoli Sekondari. Kikundi hiki kimechimba KISIMA cha MAJI ya Kijijini kwao. Vilevile, Kikundi hiki kilinunua VIFAA vya MAABARA vya Rusoli Sekondari na hivi karibuni

kimenunua Computer na Photocopy ya Sekondari hiyo – HONGERENI SANA SANA!

**MICHANGO YA MBUNGE WA JIMBO**
*Saruji Mifuko 70
*Kuchangia kulipa POSHO ya Mwalimu wa Kujitolea wa Masomo ya Sayansi kwa mwaka mmoja.
*Vitabu vingi vya Maktaba

**MATOKEO YA KIDATO CHA II (2020)**
Jumla ya Watahiniwa: 107
Div I = 6 Div II= 9 Div III = 26 Div IV= 66

**MATOKEO YA KIDATO CHA IV (2020)**
Jumla ya Watahiniwa: 64
Div = 1 Div II = 6 Div III = 7 Div IV = 44 Div O = 6

**KARIBUNI TUCHANGIE MAENDELEO YA RUSOLI SEKONDARI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SEKONDARI MPYA ILIYOFUNGULIWA MWAKA HUU (2021) YAANZA UJENZI WA MADARASA MAPYA YATAKAYOHITAJIKA MWAKANI (2022)

Posted on April 25, 2021



*Ujenzi unaoendelea wa Vyumba vipya vya Madarasa vitakavyohitajika Mwakani (Januari 2022) kwenye SEKONDARI MPYA iliyofunguliwa Mwaka huu.*

KIGERA SEKONDARI ni Shule mpya iliyoanza ujenzi wake Mwaka 2019 kwa NGUVU za WANANCHI wa Vijiji 2 wakishirikiana na WADAU wa MAENDELEO (Wazaliwa wa Vijiji hivyo viwili) na VIONGOZI wao (Madiwani 2 kwa nyakati tofauti, na Mbunge wa Jimbo).

SEKONDARI hii ni ya Vijiji 2 vya Kakisheri na Kigera vyote vya Kata ya Nyakatende. Hii ni SEKONDARI ya PILI ya Kata hii. Sekondari yake ya KWANZA (Nyakatende Sekondari) iko Kijijini Nyakatende.

**MIUNDOMBINU ILIYOKWISHAKAMILISHWA**

*Vyumba Vipya 2 vya Madarasa vinavyotumiwa na Kidato cha Kwanza
*Choo chenye Matundu 11
*Jengo la Utawala lenye Ofisi 9

**SHULE KUFUNGULIWA**
KIGERA Sekondari ilifunguliwa rasmi tarehe 22.2.2021 na tayari WANAFUNZI 122 wa KIDATO cha KWANZA wameanza masomo shuleni hapo.

**IDADI YA WALIMU**
*SEKONDARI hii mpya ina WALIMU 5 wa kuajiriwa na MWALIMU 1 wa kujitolea.

**UJENZI UNAOENDELEA**
*Nyumba ya Mwalimu (inakamilishwa)
*Maabara 3 (zinakamilishwa)

**WACHANGIAJI WA AWAMU YA KWANZA YA UJENZI (2019-2021):**
*WANAVIJIJI – Nguvukazi (kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji)
*WANAVIJIJI – Fedha taslimu Shilingi 2,000 kwa kila Mkazi (ndani ya Vijiji hivyo viwili) mwenye umri wa zaidi ya Miaka 18
*WAZALIWA wa Vijiji 2 – kulipa gharama za Mafundi
*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo

- Saruji Mifuko 150
- Mabati 108

*MBUNGE huyo wa JIMBO amelipia PANGO la miezi 6 (Februari – Julai 2021) ili WALIMU 2 wapate makazi Kijijini Kigera karibu na Sekondari hiyo.

**MFUKO WA JIMBO UMECHANGIA**
*Saruji Mifuko 300
*Mabati 216
*HALMASHAURI (Musoma DC) Tsh Milioni 5

**MADAWATI NA SAMANI ZA OFISI ZA WALIMU**
*WAZAZI wa WANAFUNZI 122 wa Kidato cha kwanza wamechangia

- Madawati

*DIWANI wa Kata ya Nyakatende, Mhe Marere John Kisha amechangia

- Samani za Ofisi za Walimu (Viti 8 na Meza 4)

**MAJI YA BOMBA**
RUWASA WILAYA inakamilisha ujenzi wa Miundombinu ya MAJI ya BOMBA (kutoka Ziwa Victoria) ya Sekondari hii.

**UJENZI WA VYUMBA VIPYA 3 VYA MADARASA YA MWAKANI (2022)**
MAOTEO ya WANAFUNZI wa KIDATO cha KWANZA wa Mwakani (2022) ni kupokea WANAFUNZI kati ya 132 na 150 kwenye Sekondari hii.

Kwa hiyo, vinahitajika VYUMBA (vingine) VIPYA 3 vya Madarasa.

**UJENZI WA AWAMU YA PILI (kuanzia April 2021 na kuendelea)**
WANAVIJIJI wenye Sekondari hii (Vijiji 2 – Kakisheri & Kigera) WAMEANZA ujenzi wa VYUMBA hivyo 3 vitakavyohitajika mwakani (Januari 2022) na BOMA la CHUMBA kipya cha kwanza litakamilika kabla ya tarehe 30.4.2021. Ujenzi utaendelea na kuhakikisha ifikapo Septemba 2021, MABOMA mengine mawili (2) yatakuwa yamekamilishwa.

**WACHANGIAJI WA UJENZI WA AWAMU YA PILI**
*WANAVIJIJI wa Vijiji 2 wanaendelea kujitolea (NGUVUKAZI) kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

*WANAVIJIJI hao wanachangia fedha taslimu Shilingi 1,000 kwa kila mwenye umri wa zaidi ya miaka 18.

*MZALIWA wa Kijiji cha Kigera, Ndugu Lucas Mashauri – ameanza kuchangia ujenzi huu mpya kwa kutoa Saruji Mifuko 10.

*Ndugu Lucas Mashauri ni MCHANGIAJI MKUU wa Miradi ya Maendeleo ya Kata ya kwao ya Nyakatende – HONGERA SANA NDUGU YETU!

# TUNAKARIBISHWA KUCHANGIA UJENZI WA SEKONDARI MPYA YA KIGERA

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kigera, Ndugu Magafu Katura anaendelea KUWAKARABISHA WADAU wa MAENDELEO kuchangia ujenzi huu unaoenda kwa KASI kubwa na UBORA wa juu.

Aidha, MWENYEKITI huyo anatoa shukrani za dhati kwa WANAVIJIJI na WAZALIWA wa Vijiji vya Kakisheri na Kigera, DIWANI na MBUNGE wao kwa MICHANGO yao kwenye Mradi huu wa Maendeleo ya Wananchi wa Kata ya Nyakatende.

SHUKRANI za kipekee wanapewa Mkuu wa Wilaya (DC), Dr Vicent Naano Anney kwa usimamiaji mzuri na makini wa ujenzi wa KIGERA SEKONDARI.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KATA YA KIRIBA YAANZA UJENZI WA SEKONDARI YA PILI

Posted on May 21, 2021



*Picha hii inaonesha baadhi ya Wananchi wa Kijiji cha Bwai Kumsoma wakiwa kwenye ujenzi wa Sekondari yao mpya, BWAI SEKONDARI, inayotarajiwa kufunguliwa mwakani (Januari 2022). Hii itakuwa SEKONDARI ya PILI ya Kata ya Kiriba.*

UMBALI MREFU wa kutembea na MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani ni sababu kuu zinazofanya baadhi ya KATA za Jimbo la Musoma Vijijini KUAMUA kuwa na SEKONDARI zaidi ya moja.

KATA ya KIRIBA inayoundwa na Vijiji vitatu (3) ambavyo ni Bwai Kwitururu, Bwai Kumsoma, na Kiriba ina Sekondari moja ya Kata (KIRIBA SEKONDARI) iliyojengwa Kijijini Bwai Kwitururu.

SEKONDARI hii ilifunguliwa Mwaka 2006, na ina jumla ya WANAFUNZI 731 (Kidato cha 1-4).

WANAFUNZI wa Vijiji vya Bwai Kumsoma na Kiriba wanalazimika kutembea umbali wa kati ya KILOMITA 5 hadi 12 kwenda masomoni KIRIBA SEKONDARI.

Vilevile, kuna MIRUNDIKANO mikubwa ya Wanafunzi madarasani. Kwa mfano, Wanafunzi wa KIDATO cha KWANZA wako sitini (60) ndani ya chumba kimoja cha darasa.

**WANANCHI WAAMUA KUJENGA SEKONDARI YA PILI YA KATA**

KIJIJI cha Bwai Kumsoma chenye WAKAZI 10,500 KIMEAMUA kujenga SEKONDARI yake ili KUTATUA MATATIZO yaliyotajwa hapo juu.

SEKONDARI inayojegwa na KIJIJI kimoja hiki, chenye VITONGOJI NANE (8), itaitwa BWAI SEKONDARI na inajengwa ndani ya KITONGOJI cha BUSIKWA

WANAFUNZI wa kujiunga na SEKONDARI inayojengwa wapo wa kutosha kwani Kijiji cha Bwai Kumsoma kina SHULE za MSINGI TATU (3), na Wanafunzi wa Vijiji vingine viwili vya Kata hii watakaribishwa kujiunga na BWAI SEKONDARI inayotarajiwa kufunguliwa mwakani (Januari 2022).

MAOTEO ya WANAFUNZI watakaojiunga na Kidato cha Kwanza mwakani (Januari 2022) kwenye Sekondari hii mpya ni kati ya 150 na 170.

**MABOMA YANAYOJENGWA KWENYE SEKONDARI MPYA**

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Bwai Kumsoma, Ndugu PIMA MASINDE KITUNDU ameeleza kwamba ujenzi wa Shule hii ulianza rasmi mwezi uliopita (Aprili 2021), na unatekelezwa kwa mpangilio ufuatayo:

*Boma la Vyumba 3 vya Madarasa
*Vyoo vya Wanafunzi na Walimu
*Boma la Jengo la Utawala
*Maabara 3 (Fizikia, Kemia na Bailojia)
*Boma la Nyumba ya Mkuu wa Shule

MTENDAJI KATA, Ndugu Pendo Isaach Mwita, na MRATIBU ELIMU KATA, Mwl Beatrice Ndosi, wanafuatilia kwa karibu sana ujenzi wa Sekondari hii mpya – TUNAWASHUKURU SANA!

**WACHANGIAJI WA MRADI HUU WA UJENZI**

MICHANGO itatolewa kwa awamu mbalimbali na kwa kuanzia:

*NGUVUKAZI za Wanakijiji zitatumika kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

*FEDHA taslimu, Tsh 10,000/= kwa kila mkazi mwenye umri kati ya miaka 18 na 59

*DIWANI wa Viti Maalum, Ndugu FLORA MAGWA ameanza kuchangia kwa kutoa SARUJI MIFUKO 5 (mitano)

*MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ameanza kuchangia kwa kutoa SARUJI MIFUKO 50 (hamsini)

**WANAKIJIJI WANAOMBA TUSHIRIKIANE NAO KUJENGA SEKONDARI MPYA**

MWENYEKITI Ndugu Pima Masinde Kitundu, kwa niaba ya Wananchi na Serikali ya Kijiji cha Bwai Kumsoma, anaomba WADAU wa MAENDELEO wakiwemo WAZALIWA wa KATA ya KIRIBA wajitokeze kuchangia MRADI huu wa ujenzi wa SEKONDARI ya pili ya Kata yao.

**ELIMU NI KIPAUMBELE CHA KWANZA MUSOMA VIJIJINI (KATA 21)**

*Tunazo Sekondari 21 za Kata
*Tunazo Sekondari 2 za Binafsi
*Tunajenga Sekondari Mpya 4

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SEKONDARI YA KATA YAJENGA MAABARA YA KIWANGO KIZURI

Posted on February 28, 2021



*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo akikakugua MAABARA ya KEMIA na VYUMBA VIPYA 4 vya MADARASA ya Dan Mapigano Memorial Secondary School ya Kata ya Bugoji*

JIMBO la Musoma Vijijini lina KATA 21 lenye jumla ya VIJIJI 68.

**IDADI YA SEKONDARI JIMBONI**
*21 za Kata/Serikali
*2 Binafsi
*4 MPYA zinajengwa vijiji vya Kabegi, Nyasaungu, Nyegina na Seka
*7 MPYA zimepangwa kuanza kujengwa Mwaka huu (2021): vijijini Bukumi, Busamba, Bwai, Kataryo/Mayani, Kurwaki/Nyang'oma, Muhoji na Wanyere.

**UJENZI WA MAABARA KWENYE SEKONDARI ZA JIMBONI**
*Kila SEKONDARI iko kwenye hatua mbalimbali za ujenzi wa MAABARA 3 – Biology, Chemistry and Physics

**DAN MAPIGANO MEMORIAL SECONDARY SCHOOL**
SEKONDARI ilifunguliwa Mwaka jana (2020) na ina jumla ya WANAFUNZI 265 (139 Form I & 126 Form II). WALIMU wapo 6 na wote wameajiriwa na SERIKALI.

**WANAOTOA MICHANGO YA UJENZI WAKE**
*Wanavijiji
*Serikali
*Diwani wa Kata
*Mbunge wa Jimbo
*Wazaliwa wa baadhi ya Vijiji

**UJENZI uliokwishakamilika:**
*Vyumba 5 vya Madarasa
*Ofisi 2 za Walimu
*Choo chenye Matundu 8

**UJENZI unaondelea:**
*Vyumba 4 vya Madarasa
*Maabara 3
*Ofisi 1 ya Walimu
*Choo chenye Matundu 8
*Nyumba 1 ya Walimu

Jumamosi, 27.2.2021, MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo alikagua ujenzi unaondelea kwenye SEKONDARI hii ya KATA ya BUGOJI yenye Vijiji 3 – Bugoji, Kaburabura na Kanderema.

**MAABARA ZINAZOJENGWA**
SERIKALI imetoa Tsh MILIONI 50 kuchangia ujenzi wa MAABARA Shuleni hapo – TUNAISHUKURU SANA SERIKALI YETU KWA MCHANGO HUU MUHIMU SANA!
WANAVIJIJI wanachangia NGUVUKAZI kwenye ujenzi wa MAABARA hizi.

**MAABARA YA KEMIA**
UBORA wa MAABARA hii ni wa kiwango kizuri, na ujenzi wake utakamilika kabla ya tarehe 15 Machi 2021.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MBUNGE WA JIMBO AWATOA WANAFUNZI WANAOJIFUNZIA MCHANGANI NA AKODISHIA NYUMBA KIJIJINI ITUMIWE NA WALIMU WA SEKONDARI MPYA

Posted on February 28, 2021



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, alipokuwa Kigera Sekondari (Kata ya Nyakatende) na Shule Shikizi Egenge (Kata ya Etaro)*

MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo anakagua ujenzi unaoendelea kwenye SHULE za MSINGI na SEKONDARI za Jimbo hilo.

**SHULE SHIKIZI EGENGE**
Shule hii iko kwenye Kitongoji cha Egenge, Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro.

IDADI ya WANAFUNZI wa Shule hii ni kama ifuatavyo: 60 Awali, 30 Darasa la I na 60 Darasa la II.

Prof Sospeter MUHONGO ameamua KUNUNUA VIBAO vya KUJIFUNZIA vya Wanafunzi wa DARASA LA AWALI na wa DARASA LA KWANZA baada ya kuambiwa kwamba Wanafunzi hao wanajifunza kwa KUANDIKA MCHANGANI.

Vilevile, Mbunge huyo amekubali KUEZEKA PAA la Vyumba 2 vya Madarasa vinavyojengwa hapo.

Shule ina Vyumba 4 vya Madarasa vilivyojengwa na SERIKALI (Miradi ya EQUIP & EP4R) kwa kushirikiana na WANANCHI wa Kitongoji cha Egenge.

Vilevile, WANANCHI hao wanajenga Vyumba vingine 4 kwa kushirikiana na DIWANI na MBUNGE wao wa Jimbo.

LENGO KUU ni Shule SHIKIZI EGENGE iwe na MIUNDOMBINU ya Shule kamili ya Msingi kabla ya tarehe 30 Disemba 2021.

**SEKONDARI MPYA YAFUNGULIWA KIJIJINI KIGERA**
KIGERA Sekondari imefunguliwa Jumatatu, tarehe 22.2.2021 na tayari WANAFUNZI 103 kati ya 122 wa Kidato cha Kwanza wameanza masomo.

WALIMU 5 ni wa kuajiriwa na Serikali na 1 ni wa kujitolea.

UJENZI unaendelea kwa kasi kubwa na MAABARA zitakamilika kabla ya tarehe 1.6.2021.

SEKONDARI hii MPYA ni kati ya Sekondari mpya 5 zinazojengwa Jimboni mwetu, na nyingine 4 zitaanza kujengwa mwaka huu.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ametembelea Sekondari hiyo mpya na kutatua tatizo la MAKAZI ya WALIMU hapo Kijijini.

MBUNGE huyo ameamua kulipia PANGO la MIEZI 6 ili WALIMU 2 waweze kupata MAKAZI hapo Kijijini, karibu na Sekondari hiyo.

**ELIMU NDIYO INJINI KUU YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UJENZI WA VIWANGO VIZURI VYA SEKONDARI MPYA YA KATA: MIUNDOMBINU YA MAJI INAJENGWA

Posted on February 8, 2021



*MIUNDOMBINU ya KIGERA SEKONDARI ambayo itafunguliwa Mwezi huu (Februari 2021)*

KATA ya NYAKATENDE inayoundwa na Vijiji 4 vya Kakisheri, Kamguruki, Kigera na Nyakatende ina SEKONDARI MOJA inayohudumia VIJIJI hivyo na Vijiji vya Kata jirani ya IFULIFU.

Kwa hiyo, SEKONDARI moja hiyo inakabiliwa na MATATIZO ya MIRUNDIKANO ya WANAFUNZI madarasani, na wengine wanatembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 10 kwenda masomoni.

WANANCHI wa Vijiji 2 (Kigera na Kakisheri) wameamua KUJENGA SEKONDARI yao ambayo itakuwa ni Sekondari ya pili ndani ya Kata hiyo (Nyakatende), na inaitwa KIGERA SECONDARY SCHOOL.

## UJENZI WA UBORA WA JUU

AFISA ELIMU na WATAALAMU wa ujenzi wa Halmashauri yetu wanakiri kwamba KIGERA SEKONDARI inajengwa kwa kuzingatia matakwa ya ujenzi yanayotolewa na SERIKALI yetu.

PONGEZI nyingi ziende kwa WANAVIJIJI na WAZALIWA wa Vijiji hivyo, na UONGOZI mzuri na madhubuti wa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kigera, Ndugu Magafu Katura.

**MICHANGO YA UJENZI**
Michango ya ujenzi wa Sekondari hii inatolewa na:

*WANAVIJIJI – Nguvukazi, yaani kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

*WANAVIJIJI – Fedha taslimu, Shilingi 2,000 kwa kila MKAZI wa Vijiji hivyo viwili na mwenye umri wa zaidi ya miaka 18.

*WAZALIWA wa Vijiji 2 hivyo. Hawa wanalipa gharama za mafundi na wananunua baadhi ya vifaa vya ujenzi.

*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo amekwishachangia SARUJI MIFUKO 150 na MABATI 108

*MFUKO wa JIMBO umechangia SARUJI MIFUKO 300 na MABATI 216.

*HALMASHAURI yetu imechangia Shillingi 5,000,000/= (Tshs 5m)

**MADAWATI NA SAMANI ZA OFISI**
*WAZAZI wa WANAFUNZI 124 watakaoanza masomo KIGERA SEKONDARI wametengeneza Madawati.

*DIWANI wa Kata ya Nyakatende, Mhe Marere John Kisha amechangia Samani za Ofisi za Walimu (Viti 8 na meza 4)

**MIUNDOMBINU YA MAJI INAJENGWA**
*RUWASA inakamilisha ujenzi wa MIUNDOMBINU ya MAJI kwa ajili ya matumizi ya Sekondari hiyo mpya – hii ni sehemu ya MRADI wa RUWASA wa USAMBAZAJI MAJI (kutoka Ziwa Victoria) kwenye Kata ya Nyakatende.

**MIUNDOMBINU INAYOKAMILISHWA ILI SEKONDARI IFUNGULIWE**
*Vyumba 2 vya Madarasa vimekamilika
*Jengo la Utawala lenye Ofisi 9 limekamilika.

*Boma la CHOO cha Matundu 11. Tundu 1 la choo ni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum – limekamilika
*Ujenzi wa CHOO cha WALIMU umeanza.
*Boma la MAABARA 3 linakamilishwa
*Nyumba 1 ya MWALIMU imeanza kujengwa

**WANAFUNZI WALIOFAULU KUINGIA KIDATO CHA KWANZA**

WANAFUNZI 191 wa Kata ya Nyakatende wamefaulu kujiunga na Kidato cha Kwanza. Hivyo, WANAFUNZI hao 191 watagawanywa kwenye SEKONDARI 2 za Kata hiyo yaani, Nyakatende Sekondari na Kigera Sekondari (itakayofunguliwa Mwezi huu, Februari 2021). Kigera Sekondari iko tayari kupokea wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, na tayari ina:
*Vyumba 2 vya Madarasa
*Choo chenye Matundu 11
*Madawati ya Wanafunzi
*Viti na Meza za Walimu
*Miundombinu ya Maji ya RUWASA

**ELIMU NI INJINI YA UCHUMI, MAENDELEO NA USITAWI IMARA WA KILA TAIFA**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# FEDHA ZA MFUKO WA JIMBO ZACHANGIA UKAMILISHAJI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MUSOMA VIJIJINI

Posted on January 10, 2021



*Baadhi ya MIUNDOMBINU inayojengwa kwenye SEKONDARI MPYA ya VIJIJI 2 (Kakisheri & Kigera) vya Kata ya Nyakatende. SEKONDARI hii itafunguliwa Mwezi huu, Januari 2021.*

UJENZI na UBORESHAJI wa MIUNDOMBINU ya SHULE zote za Jimboni mwetu unachangiwa na:

*Wanavijiji

*Serikali

*Mbunge wa Jimbo

*Wadau wa Maendeleo, k.m. PCI Tanzania, na Benki za NMB, CRDB na TPB

*Wazaliwa wa baadhi ya Vijiji

**IDADI YA SHULE NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI**

(Jimbo lina Vijiji 68, Kata 21)

**(i) SHULE SHIKIZI: 12**

Ujenzi na upanuzi wa Shule hizi unaendelea. Baadhi ya Shule hizo tayari zinatoa ELIMU ya AWALI ya WATOTO wa chini ya MIAKA 6.

**(ii) SHULE ZA MSINGI: 111**

Vyumba vipya vya Madarasa vinaendelea kujengwa na kuboreshwa kwenye shule hizi.

Vyumba VIPYA 380 vimejengwa kwenye shule hizi ndani ya miaka mitano (2016-2020).

MAKTABA zinaendelewa kujengwa (nyingine tayari zimekamilika na zinatumika) kwenye baadhi ya shule hizi MIUNDOMBINU mingine inaendelea kujengwa na kuboreshwa, hasa NYUMBA mpya za WALIMU na VYOO vipya.

**(iii) SHULE ZA MSINGI ZA BINAFSI: 3**

*Zipo Shule za Binafsi 3 ndani ya Jimbo letu.

**(iv) SEKONDARI ZA KATA:**

20 + 5 mpya SEKONDARI MPYA zilizofunguliwa Mwaka jana (2020) ni mbili:

*Dan Mapigano Memorial Secondary School ya Kata ya Bugoji

*Busambara Secondary School ya Kata ya Busambara

Vyumba VIPYA 120 vimejengwa kwenye Sekondari zetu 20 ndani ya miaka mitano (2016-2020).

(**v) SEKONDARIZA BINAFSI: 2**

*Zipo Sekondari 2 za Madhehebu ya Dini ya Katoliki (RC) na Wasabato (SDA)

(**vi) SEKONDARI MPYA ZA KATA ZINAZOJENGWA**

SEKONDARI zinazojengwa na zitakazofunguliwa Mwaka huu (2021) ni:

*Seka Secondary School ya Kata ya Nyamrandirira (Sekondari ya pili ya Kata)

*Nyasaungu Secondary School ya Kata ya Ifulifu (Sekondari ya kwanza ya Kata)

*Kigera Secondary School, Kata ya Nyakatende (Sekondari ya pili ya Kata)

*Bukwaya Secondary School ya Kata ya Nyegina inakamilisha miundombinu (Sekondari ya pili ya Kata)
*Ifulifu Secondary School ya Kata ya Ifulifu inayojengwa Kijijini Kabegi. Inakamilisha miundombinu (Sekondari ya Kata ya pili)

**USIMAMIAJI MZURI & MADHUBUTI**
*MKUU wa Wilaya (DC), Dr Vicent Anney Naano anapongezwa sana kwa KUSIMAMIA ujenzi huu na mwingine, kwa MAFANIKIO makubwa, tokea Mwaka 2016.

**MGAO WA FEDHA ZA MFUKO WA JIMBO**
(Jan 2021, Tshs 52.43m)

**MANUNUZI & UGAWAJI:**
*Mabati: 1,134
*Saruji Mifuko (supa):1,020
JUMLA: Tshs 52,176,378 (Tshs 52.18m)
*HALMASHAURI yetu ndiyo inayotunza FEDHA za MFUKO wa JIMBO, na ndiyo inafanya MANUNUZI ya VIFAA vya UJENZI baada ya kupewa MAELEKEZO kutoka kwenye Kamati ya Mfuko wa Jimbo chini ya Mwenyekiti wake, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo

**MGAO – MALENGO**
*Kukamilisha MIUNDOMBINU ya SHULE MPYA ili zifunguliwe Mwaka huu (2021).
*Kuongeza idadi ya Vyumba VIPYA vya Madarasa kwenye Sekondari zilizofunguliwa Mwaka jana (2020)

**SEKONDARI MPYA (2021):**
**(1) SEKA SECONDARY SCHOOL**
(Kata ya Nyamrandirira)
*Mabati 216
*Saruji Mifuko 200

**(2) KIGERA SECONDARY SCHOOL**
(Kata ya Nyakatende)
*Mabati 216
*Saruji Mifuko 200

**(3) NYASAUNGU SECONDARY SCHOOL**
(Kata ya Ifulifu)
*Mabati 54
*Saruji Mifuko 80

**SEKONDARI MPYA ZA MWAKA JANA (2020)**
(4) DAN MAPIGANO MEMORIAL SECONDARY SCHOOL
(Kata ya Bugoji)
*Mabati 216
*Saruji Mifuko 180

**(5) BUSAMBARA SECONDARY SCHOOL**
(Kata ya Busambara)
*Mabati 216
*Saruji Mifuko 180

**SHULE ZA MSINGI MPYA**
(6) MWIKOKO SHULE SHIKIZI
(Kitongoji cha Mwikoko, Kijiji cha Chitare, Kata ya Makojo)
*Mabati 108
*Saruji Mifuko 80

**(7) NYASAENGE SHULE SHIKIZI**
(Kitongoji cha Nyasaenge, Kijiji cha Kataryo, Kata ya Tegeruka)
*Mabati 108
*Saruji Mifuko 100

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
[www.musomavijijini.or.tz](http://www.musomavijijini.or.tz)

# KATA YA NYAMRANDIRIRA YADHAMIRIA KUPATA SEKONDARI YAKE YA PILI ITAKAYOFUNGULIWA JANUARI 2021

Posted on January 1, 2021



*MIUNDOMBINU ya SEKA SEKONDARI inavyoendelea kujengwa Kijijini Seka, Kata ya Nyamrandirira.*

Kata ya Nyamrandirira inaundwa na Vijiji Vitano (5) ambavyo ni: Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka.

Kata hii ina Sekondari moja tu iliyoko Kijijini Kasoma (KASOMA SECONDARY SCHOOL) yenye Kidato cha kwanza hadi cha sita.
UMBALI MREFU wa zaidi ya km 10 wa kutembea kwa Wanafunzi walio wengi, na MIRUNDIKANO yao Madarasani ni sababu zilizowafanya WANANCHI wa Kata hii kuamua kujenga SEKONDARI ya pili Kijijini Seka (SEKA SECONDARY SCHOOL).

Akizungumza na Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu Fedson Masawa, DIWANI wa Kata ya Nyamrandirira, Mhe Nyeoja Wanjara amesema kuwa lengo lao ni kukamilisha ujenzi wa VYUMBA 5 vya MADARASA kabla ya tarehe 30 Januari 2021.

MIUNDOMBINU mingine muhimu inayohitajika ili SEKA SEKONDARI ifunguliwe itakamilishwa kabla ya tarehe 30 Januari 2021 ambayo ni:
*Choo chenye Matundu 8
*Jengo la Utawala
MAJENGO mengine yatakayojengwa ni: Maabara, Maktaba, Vyumba zaidi vya Madarasa, Nyumba za Walimu, n.k.

SEKA SEKONDARI ni moja ya Sekondari Mpya 5 zinazojengwa ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini lenye Sekondari 20 za Serikali/Kata na 2 za Binafsi.

**Wachangiaji wa Ujenzi huu ni:**
**(i) WANANCHI KWA MPANGILIO HUU:**
*Kijiji cha Kaboni – kila Kaya inachangia Tsh 10,000/=
*Kijiji cha Seka – kila Kaya inachangia kati ya Tsh 20,000/= na 15,000/=
*Kijiji cha Kasoma – kila Kaya inachangia Tsh 10,000/=
*Kijiji cha Chumwi – kila Kaya inachangia Tsh 6,500/=
*Kijiji cha Mikuyu – kila Kaya inachangia Tsh 20,000/=

**(ii)NGUVUKAZI ZA WANAVIJIJI WA VIJIJI VYOTE 5**
Kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

**(iii) MBUNGE WA JIMBO**
Prof Sospeter Muhongo tayari amekwishachangia SARUJI MIFUKO 250 (mia mbili hamsini). MBUNGE huyo ametoa AHADI ya kutoa MICHANGO zaidi iwapo KASI ya UJENZI itaongezeka, na hasa ya ujenzi wa VYOO vya Shule.

**(iv) WAZALIWA WA KATA YA SEKA**
*Wazaliwa 21 tayari wamechangia jumla ya Tsh 1,884,000/=

**(v) WADAU WENGINE WA MAENDELEO**
Mgodi wa MMG uliopo Kijijini Seka umechangia:
*Mawe tripu 20
*Molamu tripu 10
*Mchanga tripu 10
Vilevile, MMG imetoa AHADI ya kujenga Jengo moja la Shule.

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Seka, Ndugu Damian Mjara, kwa niaba ya Wananchi wa Kata Nyamrandirira, anawaomba WADAU wa MAENDELEO wajitokeze na kuwachangia MABATI, SARUJI, NONDO, MADAWATI, n.k. ili SEKA SEKONDARI ifunguliwe tarehe 30 Januari 2021.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SEKONDARI NYINGINE MPYA INAYOJENGWA KWA NGUVU ZA WANANCHI NA MBUNGE WAO KUFUNGULIWA JANUARI 2021

Posted on December 29, 2020



*Ukamilishaji wa MIUNDOMBINU ya KIGERA SECONDARY SCHOOL itakayofunguliwa Januari 2021*.

JIMBO la MUSOMA VIJIJINI lenye Kata 21 zenye Vijiji 68 linajenga SEKONDARI MPYA 5 ili kutatua MATATIZO sugu mawili – mirundikano madarasani na umbali mrefu wanaotembea baadhi ya Wanafunzi.

Kwa hiyo, idadi ya SEKONDARI za Serikali Jimboni humo zitaongezeka kutoka 20 hadi 25. Vilevile, zipo Sekondari 2 za Madhehebu ya Dini.

MWAKA MPYA (2021): Kata nyingine 6 zitaanza ujenzi wa Sekondari ya pili ya Kata zao.

KATA ya NYAKATENDE yenye Vijiji 4 (Kakisheri, Kamguruki, Kigera na Nyakatende) ina Sekondari moja tu (NYAKATENDE SEKONDARI) ambayo imeelemewa na wingi wa Wanafunzi kutoka Vijiji 4 na wengine wanatoka Kata jirani ya Ifulifu.

Kwa hiyo, UJENZI wa SEKONDARI ya PILI ya Kata hiyo ni muhimu sana.

**KIGERA SEKONDARI ITAFUNGULIWA JANUARI 2021**

Vijiji 2 (Kakisheri na Kigera) vya Kata hiyo VIMEAMUA kujenga SEKONDARI yao ili watoto wao waachane kabisa na mirundikano madarasani na kutembea mwendo wa zaidi ya kilomita 10 kwenda masomoni.

**WANAOCHANGIA UJENZI WA KIGERA SEKONDARI**

(i) WANAVIJIJI wa Vijiji viwili wanachangia NGUVUKAZI zao- kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

(ii) WANAVIJIJI hao wanachangia FEDHA taslimu: Shilingi 2,000 (elfu mbili) kwa kila mkazi mwenye umri wa kuanzia miaka 18.

(iii) WAZALIWA wa Vijiji hivyo viwili: wanalipa GHARAMA zote za MAFUNDI na wananunua baadhi ya VIFAA vya ujenzi.

(iv) DIWANI wa Kata ya Nyakatende, Mhe Marere John Kisha ambae ni mmoja wa WAZALIWA na Vijiji 2 nae anachangia kama Wazaliwa wenzake.

*Vilevile, DIWANI huyu anatengeneza MADAWATI 130 ya WANAFUNZI watakaoanza Kidato cha kwanza shuleni hapo Januari 2021.

(v) MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo amekwishachangia

*Saruji Mifuko 150

*Mabati 108

MFUKO wa JIMBO umechangia:

*Saruji Mifuko 100

*Mbunge huyo atachangia, Januari 2021, zaidi ya VITABU 1,000 (elfu moja) vya SAYANSI vya Maktaba ya Sekondari hiyo mpya.

**MAJENGO YANAYOKAMILISHWA UJENZI**

*VYUMBA 2 vya Madarasa vimeishaezekwa, frame za milango na madirisha zimewekwa, sasa wanapiga jamvi kwa ajili ya kuweka sakafu.

*JENGO la Utawala lenye Ofisi 9 limeezekwa na madirisha yamewekwa.

*BOMA la CHOO cha Matundu 11 limeishaezekwa. Tundu 1 la Choo ni kwa ajili ya Wanafunzi wenye mahitaji maalum.

*Boma la Maabara linajengwa

*Boma la Nyumba ya Mwalimu linajengwa

**WANAFUNZI 191 WA KATA WAMEFAULU**
Wanafunzi 191 wa Kata ya Nyakatende wamefaulu kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari 2021.

Kwa hiyo, WANAFUNZI hao 191 watagawanywa kwenye SEKONDARI 2 za Kata – Nyakatende & Kigera Secondary Schools.

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Kigera, Ndugu Magafu Katura anatoa maombi mapya yafuatayo ya kuchangia ujenzi huu kwa hatua waliyoifikia:
*Saruji Mifuko 100
*Topu 31 za Milango
*Frame 21 za Milango ya Choo na ya Jengo la Utawala
*Vitasa 31vya Milango
*Bawaba 31 (pair) za Milango
*Masinki 15 ya Choo
*Mabomba piece 5 ya Choo
*Rangi Lita 80

HALMASHAURI ya Wilaya ya Musoma IMECHANGIA Shilingi MILIONI TANO (Tsh.5m) kwenye ukamilishaji wa ujenzi wa Miundombinu ya Sekondari hii mpya.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANANCHI WA KIJIJI CHA NYASAUNGU WASHIRIKIANA NA MBUNGE WAO KUJENGA SEKONDARI YA KIJIJI CHAO

Posted on December 29, 2020



*Ukamilishaji wa ujenzi wa MIUNDOMBINU ya NYASAUNGU SEKONDARI ya Kijiji cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu.*

KATA ya IFULIFU ni Kata pekee kati ya Kata 21 za Jimbo la Musoma Vijijini ambayo HAINA SEKONDARI yake.

WANAFUNZI wa Sekondari kutoka VIJIJI 3 vya Kata hii, yaani, Kabegi, Kiemba na Nyasaungu wanasoma kwenye Sekondari za Kata jirani za Mugango na Nyakatende.

WANAVIJIJI wa Kata ya IFULIFU WAMEAMUA kujenga Sekondari zao za Kata kwa utaratibu huu:
*Kijiji cha Nyasaungu kinajenga Sekondari yake kwa kushirikiana na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo
*Vijiji vya Kabegi na Kiemba nao wanajenga Sekondari yao kwa kushirikiana na Mbunge wao, Prof Sospeter Muhongo.

**NYASAUNGU SEKONDARI**

Ujenzi wa Sekondari hii ulianza Julai 2019. WANANCHI wa Kijiji cha Nyasaungu waliamua kujenga Sekondari yao iitwayo NYASAUNGU SEKONDARI ili kutatua kero ya Watoto wao kutembea kilomita 24 kwenda masomoni kwenye Sekondari za Kata jirani.

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Nyasaungu, Ndugu Magesa Chacha Marera, amesema kuwa ujenzi huo hadi hapo ulipofikia unaendeshwa kwa NGUVU za WANANCHI wa Kijiji cha Nyasaungu pekee, na michango ya Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo.

**MAKUNDI YANAYOCHANGIA UJENZI WA NYASAUNGU SEKONDARI**

(i) KAYA zenye NG'OMBE zaidi ya 100, michango yao ni zaidi ya Tshs 200,000 (laki mbili)
(ii) KAYA zenye NG'OMBE kati ya 50 na 99, michango yao ni Tshs 100,000 (laki moja)
(iii) KAYA zenye NG'OMBE chini ya 50, michango yao ni Tshs 40,000 (elfu arobaini).
(iv) NGUVUKAZI za Wanakijiji za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.
(v) MICHANGO ya Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo
*MABATI 108
*SARUJI MIFUKO 35
*NONDO 20

MFUKO wa JIMBO umechangia:
*Mabati 54

**MIUNDOMBINU INAYOKAMILISHWA SEKONDARI IFUNGULIWE JANUARI 2021**

*VYUMBA 2 vya Madarasa tayari vimeishaezekwa
*CHUMBA 1 cha Darasa tayari kimeishaezekwa na hiki kitatumika kwa muda kama OFISI ya WALIMU
*CHOO chenye MATUNDU 6 kinaezekwa kabla ya tarehe 1.1.2021

**WANAFUNZI 124 WA KATA WAMEFAULU**

NYASAUNGU Sekondari, yenye VYUMBA 2 vya MADARASA inategemea kupokea baadhi ya WANAFUNZI hao wa Kata.

UONGOZI wa KIJIJI cha Nyasaungu unatoa maombi kwa WADAU wa MAENDELEO waungane nao kwenye ujenzi wa SEKONDARI

yao – wanaendelea na ujenzi wa Vyumba vya Madarasa, Jengo la Utawala, Maabara, Maktaba, Nyumba za Walimu, Vyoo, n.k.

SEKONDARI hii MPYA itakuwa tayari kupokea Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Januari 2021.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAVIJIJI WAMEDHAMIRIA WATOTO WAO WASITEMBEE UMBALI MREFU KWENDA MASOMONI

Posted on December 19, 2020



*MIUNDOMBINU inayojengwa KIGERA SEKONDARI itakayokuwa tayari kupokea WANAFUNZI wa KIDATO cha KWANZA Januari 2021.*

KATA ya NYAKATENDE yenye Vijiji 4 (Kakisheri, Kamguruki, Kigera na Nyakatende) inayo SEKONDARI MOJA tu, NYAKATENDE SEKONDARI ambayo ina MIRUNDIKANO ya WANAFUNZI madarasani. Vilevile, baadhi ya WANAFUNZI wanatembea zaidi ya KILOMITA 10 kwenda masomoni kwenye Sekondari hiyo iliyofunguliwa Mwaka 2006, yenye WANAFUNZI 784 na ina UPUNGUFU wa Vyumba 4 vya Madarasa.

**SULUHISHO LA KERO ZA MIRUNDIKANO NA UMBALI MREFU WA KUTEMBEA**

VIJIJI 2 vilivyoko mbali na Nyakatende Sekondari VIMEAMUA KUJENGA SEKONDARI yao wenyewe. VIJIJI hivyo ni Kakisheri na Kigera.

**MICHANGO YA UJENZI WA SEKONDARI MPYA**

MICHANGO ya ujenzi wa Sekondari ya Vijiji hivyo viwili inatolewa na:

*WANAVIJIJI wanachangia NGUVUKAZI zao kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

*WANAVIJIJI wanachangia FEDHA taslimu, Shilingi 2,000 kwa kila mwenye umri wa miaka 18 na zaidi.

*WAZALIWA wa Vijiji vya Kakisheri na Kigera WANALIPA GHARAMA za MAFUNDI ujenzi na WANANUNUA baadhi ya VIFAA vya ujenzi.

*DIWANI wa Kata ya Nyakatende, Mhe Marere John Kisha, ni mmoja wa WAZALIWA wanaochangia ujenzi huu. Vilevile, ameanza kutengeneza MADAWATI 130 ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza watakaoanza MASOMO Januari 2021 kwenye Sekondari hiyo inayoitwa," KIGERA SECONDARY SCHOOL."

*MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo AMEISHACHANGIA:

- Saruji Mifuko 150
- Mabati 108

*MFUKO wa JIMBO umeishachangia:

- Saruji Mifuko 100

MBUNGE wa JIMBO kwa KUSHIRIKIANA na WADAU wengine wa MAENDELEO ataendelea kuchangia ujenzi huu.

**MAJENGO YANAYOKAMILISHWA UJENZI**

*VYUMBA 2 vya Madarasa vimeishaezekwa na madirisha yamewekwa.

*JENGO la UTAWALA lenye Vyumba (Ofisi 9) limeishaezekwa na madirisha yamewekwa.

*BOMA la CHOO chenye MATUNDU 11 litaezekwa kabla ya tarehe 30.12.2020. Tundu 1 ni kwa Watu wenye ULEMAVU.
*BOMA la MAABARA 2 litaezekwa kabla ya tarehe 30.12.2020
*BOMA la NYUMBA 1 ya MWALIMU litaezekwa kabla ya tarehe 30.12.2020

**WANAFUNZI WALIOFAULU**
*WANAFUNZI 191 wa Kata ya Nyakatende WAMEFAULU kuendelea na MASOMO ya SEKONDARI.

Kwa hiyo, WANAFUNZI hao 191 watagawanywa kwenye SEKONDARI 2 za Kata, yaani NYAKATENDE SEKONDARI

iliyoanza Mwaka 2006, na KIGERA SEKONDARI itakayoanza Januari 2021.

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Kigera, Ndugu Magafu Katura anatoa MAOMBI ya kuchangiwa SARUJI MIFUKO 300 na RANGI LITA 80 ili kukamilisha Maboma ya Sekondari yao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SERIKALI YATOA SHILINGI MILIONI 50 ZA KUUNGA MKONO JITIHADA ZA WANAVIJIJI ZA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SEKONDARI YAO YA KATA

Posted on November 23, 2020



*Baadhi ya WANAVIJIJI wa Kata ya Kiriba na MAFUNDI wao wakiwa kwenye ujenzi wa JENGO la UTAWALA la Kiriba Sekondari.*

JIMBO la Musoma Vijijini lenye Kata 21 lina Vijiji 68 na lina jumla ya SEKONDARI 20 za KATA, na SEKONDARI MPYA 5 za Kata zinatarajiwa kufunguliwa Januari 2021. Vilevile, Jimbo lina SEKONDARI 2 za BINAFSI za Madhehebu ya Dini.

KATA 5 – Etaro, Makojo, Mugango, Suguti na Tegeruka zimepanga kuanza kujenga SEKONDARI ya PILI ya Kata zao.

**KIRIBA SEKONDARI:**

VIJIJI 3 vya Kata ya KIRIBA ambavyo ni Bwai Kumusoma (Paris), Bwai Kwitururu (London) na Kiriba VIMEAMUA KUJITOLEA kuboresha MIUNDOMBINU ya Sekondari yao, KIRIBA SEKONDARI.

UBORESHAJI uko kwenye ujenzi wa MAABARA 3, MABWENI 2, JENGO la UTAWALA na NYUMBA za WALIMU.

**SHILINGI MILIONI 50 ZA SERIKALI:**
SERIKALI yetu inapewa SHUKRANI nyingi kwa kutoa Shilingi MILIONI 50 kuchangia ujenzi wa JENGO la UTAWALA la Sekondari hiyo.

WANAVIJIJI kutoka Vijiji 3 vya Kata hiyo wanachangia NGUVUKAZI kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji. Hayo yamesemwa na Mwalimu Mkuu wa Sekondari hii, Mwl Paul Mtani.

DIWANI MTEULE wa Kata ya Kiriba, Mhe Hamisi Saire ametoa SHUKRANI nyingi kwa SERIKALI na kwa MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo kwa MICHANGO yao MINGI ya kuboresha MIUNDOMBIMU ya ELIMU ndani ya Kata yao.

MBUNGE huyo wa Jimbo la Musoma Vijijini alishachangia KIRIBA SEKONDARI jumla ya Saruji Mifuko 175, Rangi ndoo 10 na Vitabu 1,000 vya Maktaba.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KIGERA SEKONDARI KUFUNGULIWA JANUARI 2021 – SEKONDARI YA PILI YA KATA

Posted on November 21, 2020



*Baadhi ya MABOMA ya KIGERA SEKONDARI itakayofunguliwa Januari 2021 – KARIBU UCHANGIE ujenzi huu.*

Kata ya Nyakatende yenye Vijiji 4 ina Sekondari 1 ambayo imeelemewa na wingi wa Wanafunzi na baadhi yao wanatembea umbali mrefu (zaidi ya kilomita 5) kwenda masomoni.

Vijiji 2 vya KIGERA na KAKISHERI vimeamua kujenga SEKONDARI yao (KIGERA SEKONDARI) kwani WATOTO wao ndio wanatembea umbali mrefu kwenda NYAKATENDE SEKONDARI.

**MICHANGO YA UJENZI ILIYOKWISHATOLEWA**

*NGUVUKAZI za Wakazi wa Vijiji vya Kigera na Kakisheri (kusomba maji, mchanga, mawe na kokoto)

*MICHANGO ya FEDHA taslimu ya awali: Shilingi 2,000 kwa kila mkazi (vijiji 2) mwenye umri kati ya miaka 18 na 59.

*WAZALIWA wa Vijiji 2 wanawalipa MAFUNDI na fedha nyingine zinanunua vifaa vya ujenzi.

*SARUJI MIFUKO 150 ya Mbunge wa Jimbo, Profesa Muhongo

*SARUJI MIFUKO 100 ya Mfuko wa Jimbo

**MAJENGO YANAYOHITAJIKA KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA (2021)**

*Maoteo ya Wanafunzi wa Kata ya Nyakatende watakaojiunga na Kidato I ni 190.

*Maoteo ya Wanafunzi watakaojiunga na Kidato I KIGERA SEKONDARI ni 120.

*Maoteo ya Wanafunzi wa Kidato I watakaoenda NYAKATENDE SEKONDARI ni 70.

**MICHANGO MINGINE YA MBUNGE WA JIMBO NA DIWANI MTEULE**

*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo atachangia MABATI 108 (bando 9, geji 28)

*Diwani Mteule, Mhe Marere John Kisha atatengeneza MADAWATI 120 ya Wanafunzi wa Kidato I.

**ELIMU KWANZA**

Jimbo la Musoma Vijijini lenye KATA 21, lina:

*Sekondari 20 za Kata/Serikali

*Sekondari 2 za Binafsi

*Sekondari Mpya 5 zinazotarajiwa kufunguliwa Januari 2021 (Bukwaya, Kigera, Nyasaungu, Ifulifu na Seka)

*Sekondari Mpya 5 zitakazoanza kujengwa mwakani (2021) za Kata za: Etaro, Makojo, Mugango, Suguti na Tegeruka.

*HIGH SCHOOLS zitaongezeka kutoka 2 (1 Serikali & 1 Binafsi) hadi 6 ndani ya miaka 5.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## MICHANGO INAHITAJIKA ILI SEKA SEKONDARI IFUNGULIWE JANUARI 2021

Posted on November 21, 2020



*Baadhi ya MABOMA ya SEKA SEKONDARI yanayopaswa kukamilishwa kabla ya tarehe 30.12.2020 – UNAKARIBISHWA SANA UCHANGIE ujenzi huu*

KATA ya NYAMRANDIRIRA ina Vijiji 5 (Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka) na Sekondari moja, KASOMA SEKONDARI. Sekondari hii imeelemewa na WINGI wa WANAFUNZI wa kutoka Vijiji 5 WANAORUNDIKANA madarasani.

Baadhi ya Wanafunzi hao wanatembea UMBALI MREFU wa zaidi ya kilomita 10 kwenda masomoni kwenye Sekondari hiyo.

SULUHISHO: kujenga Sekondari ya pili ya Kata hiyo. Ujenzi umeanza na lengo kuu ni kuifungua mwakani (Januari 2021).

**MAJENGO YANAYOJENGWA KWA SASA**
*Vyumba 8 vya Madarasa
*Jengo la Utawala
*Vyoo vya Wanafunzi & Walimu
*Maabara
*Maktaba
*Nyumba za Walimu

**MAJENGO YANAYOHITAJIKA KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA MWAKANI**

**IDADI YA WANAFUNZI:**
*Maoteo: Wanafunzi 250 wa Kata ya Nyamrandirira watafaulu kujiunga na Kidato I mwakani, Januari 2021
*Maoteo: Wanafunzi 100 watajiunga na SEKA SEKONDARI
*Wanafunzi 150 watajiunga na KASOMA SEKONDARI

**MAJENGO YANAYOPASWA KUKAMILISHWA KABLA YA TAREHE 30 DISEMBA 2020:**

(1) Vyumba 3 vya Madarasa
(2) Ofisi 1 ya Walimu
(3) Choo chenye Matundu 8

**WANAOCHANGIA UJENZI HUU (hadi leo hii):**
(1) Wanavijiji wa Vijiji 5
(2) Viongozi wa Vijiji/Kata
(3) Mgodi Mdogo wa Dhahabu wa Seka
(4) Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo (alishachangia Saruji Mifuko 150

**MABATI 54:**
Tarehe 24.11.2020, Mbunge wa Jimbo, Prof S Muhongo atachangia MABATI 54 ya kuezeka Chumba 1 cha Darasa.

**WAZALIWA WA KATA YA NYAMRANDIRIRA:**
*Wanavijiji bado wanasubiri kwa shauku kubwa AHADI za MICHANGO ya WAZALIWA (na marafiki zao) wa Kata hiyo.

**MICHANGO IPELEKWE kwa:**
*Mtendaji: 0756 680 887
*DC wa Wilaya ya Musoma

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MIRADI YA UJENZI WA SEKONDARI MPYA TISA (9) ZA KATA ITAKAMILISHWA NA WANANCHI WAKISHIRIKIANA NA SERIKALI YA CCM

Posted on September 29, 2020




*Jimbo la Musoma Vijijini lina JUMLA ya SEKONDARI 20 za KATA. Sekondari zote hizi ziko kwenye UJENZI wa MAABARA, MAKTABA, VYUMBA VIPYA VYA MADARASA, OFISI & NYUMBA ZA WALIMU, n.k.*

Jimbo la Musoma Vijijini lina UJENZI wa SEKONDARI MPYA TANO (5) za Kata zilizopangwa zifunguliwe mwakani (Januari 2021). SEKONDARI MPYA hizo ni:

(i) Kigera, Kata ya Nyakatende,
(ii) Nyasaungu, Kata ya Ifulifu,
(iii) Ifulifu (inajengwa Kijijini Kabegi), Kata ya Ifulifu,
(iv) Seka, Kata ya Nyamrandirira, na
(v) Bukwaya, Kata ya Nyegina.

Kata hizo 5 zitakuwa na SEKONDARI zaidi ya MOJA ndani ya Kata zao.

## VITENDO KWANZA

Kata nyingine za Jimbo la Musoma Vijijini nazo zimepanga kuwa na SEKONDARI zaidi ya MOJA ndani ya Kata zao. Kwa hiyo, zimeishafanya maamuzi ya kuanza kujenga SEKONDARI MPYA. Kata hizo ni:

(i) Suguti, itajenga Sekondari mpya Kijijini Wanyere
(ii) Tegeruka, Sekondari mpya itajengwa katikati ya Vijiji vya Kataryo na Mayani,
(iii) Etaro, itajenga Sekondari mpya Kijijini Busamba, na
(iv) Mugango, Sekondari mpya itajengwa katikati ya Vijiji vya Kurwaki na Nyang'oma

Ifikapo MWAKA 2025, Jimbo la Musoma Vijijini, lenye Kata 21 litakuwa na:

*SEKONDARI 29 za Kata (Serikali)
*SEKONDARI 2 za Binafsi (SDA & KATOLIKI)
*VETA 1 – maombi yameishapelekwa Serikalini

*MAENDELEO KWANZA*
*CHAGUENI CCM TUKAMILISHE MIRADI YETU
*CHAGUENI DKT MAGUFULI ili TUKAMILISHE MIRADI YETU*
*CHAGUENI PROF MUHONGO & MADIWANI 21 WA CCM wa KATA 21 za Jimbo letu ili TUKAMILISHE MIRADI YETU

PICHA zilizopo ukurasa wa 46 zinaonesha ujenzi unaoendelea kwa baadhi ya SEKONDARI MPYA za KATA za Jimbo la Musoma Vijijini.

**"TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA"**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz


DAN MAPIGANO MEMORIAL Sec


KIGERA Sec School


SEKA Sec School

# SEKONDARI MPYA ZINADAIWA VYUMBA VIPYA VYA MADARASA KWA AJILI YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA CHA MWAKANI (2021)

Posted on July 10, 2020



*Wanafunzi wa Dan Mapigano Memorial Secondary School, wakiwa Darasani.*

JIMBO la Musoma Vijijini lina SEKONDARI MPYA 2 (Dan Mapigano Memorial Secondary School, Kata ya Bugoji & Busambara Secondary School, Kata ya Busambara) zilizofunguliwa Mwaka huu (2020). MIUNDOMBINU ILIYOPO inatosheleza MAHITAJI ya sasa ya KIDATO CHA KWANZA (Form I).

MAOTEO ya Wanafunzi wa FORM I mwakani (2021) ni haya:
(i) Dan Mapigano Memorial Secondary School ya Kata ya Bugoji INATARAJIA KUPOKEA Wanafunzi 250 wa Form I (Jan 2021)

Vyumba Vipya vinavyohitajika ni 5, vilivyopo ni 2. UJENZI wa Vyumba Vipya 3 umeanza na unapaswa kukamilika kabla ya tarehe 1.10.2020.

Prof Sospeter Muhongo ATACHANGIA MABATI 54 ya Geji 28 (yanayotosha kuezeka darasa moja) kabla ya tarehe 14.7.2020

(ii) Busambara Secondary School ya Kata ya Busambara INATARAJIA KUPOKEA Wanafunzi 270 wa Form I (Jan 2021)
Vyumba Vipya vinavyohitajika ni 7, vilivyopo ni 1. UJENZI wa Vyumba Vipya 6 umeanza na unapaswa kukamilika kabla ya tarehe 1.10.2020.

Prof Sospeter Muhongo ATACHANGIA MABATI 54 ya Geji 28 (yanayotosha kuezeka darasa moja) kabla ya tarehe 14.7.2020

**SEKONDARI NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI**
*Sekondari za Serikali au Kata ni 20.
Ujenzi wa MAABARA kwenye Sekondari zote 20 HAUJAKAMILIKA!
*Sekondari za Binafsi ni 2
*Sekondari zinazojengwa na zimepagwa zifunguliwe mwakani (2021) ni 5: Seka (Kata ya Nyamrandirira), Nyasaungu, Kabegi (zote za Kata ya Ifulifu), Kigera (Kata ya Nyakatende) na Bukwaya (Kata ya Nyegina). Kata nyingine zilizopanga kuanza kujenga Sekondari ya pili ni Etaro, Mugango na Suguti.

**UAMUZI WA KUONGEZA HIGH SCHOOLS JIMBONI MWETU**
Tunayo MOJA TU, KASOMA High School, Arts subjects (Kata ya Nyamrandirira)

Baraza la Madiwani lilishaamua KUONGEZA High Schools (hasa za MASOMO ya SAYANSI) kwenye Sekondari zifuatazo: (i) Bugwema, (ii) Mtiro, (iii) Mugango na (iv) Mkirira.

KARIBUNI TUCHANGIE ujenzi wa Secondary & High Schools Jimboni mwetu

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAVIJIJI WANAJENGA VYUMBA 2 VYA MADARASA NA MATUNDU 28 YA VYOO VYA WANAFUNZI

Posted on February 15, 2021



*Hatua ya ujenzi iliyofikiwa kwa MABOMA ya Vyumba viwili vya Madarasa, na MASHIMO 28 ya VYOO vya Wanafunzi wa BUGWEMA SEKONDARI ya Kata ya Bugwema.*

WANAVIJIJI wa Kata ya Bungwema yenye Vijiji 4 (Bugwema, Kinyang'erere, Masinono na Muhoji) wanashirikiana na VIONGOZI wao kujenga Vyumba viwili (2) vya Madarasa, Ofisi moja (1) ya Walimu na Matundu 28 ya VYOO vya Wanafunzi kwenye SEKONDARI yao (Bugwema Secondary School).

Akishuhudia ujenzi unaoendelea shuleni hapo, MSAIDIZI wa MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu Fedson Masawa, amejiridhisha na maendeleo mazuri kwenye ujenzi huo.

**MICHANGO YA UJENZI KUTOKA KWA WANAVIJIJI**

MTENDAJI KATA (WEO) hiyo, Ndugu Josephat Phinias amesema WANAVIJIJI wamekubaliana kuchanga Tsh 5,000 kutoka kila KAYA kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba vya Madarasa.

Vilevile, kila KAYA inachanga Tsh 15,000/= kwa ajili ya ujenzi wa MATUNDU 28 ya VYOO vya Wanafunzi.

KIONGOZI huyo anaomba WADAU wa MAENDELEO wawachangie MABATI 108 kwa ajili ya kuezeka MABOMA wanayoyajenga.

**MICHANGO YA MBUNGE WA JIMBO**
Prof Sospeter Muhongo, Mbunge wa Jimbo lenye Bugwema Sekondari ameishaichangia shule hii kama ifuatavyo:
*VITABU vingi vya Maktaba
*POSHO ya Mwalimu 1 wa MASOMO ya SAYANSI kwa kipindi cha MIAKA MIWILI (2).
*SARUJI MIFUKO 70
*Kupeleka WAFADHILI wa ujenzi wa MAABARA

MWALIMU MKUU wa Bugwema Sekondari, Mwl Joseph Emmanuel Ndaro ameeleza kwamba SEKONDARI hiyo ilianzishwa MWAKA 2006, ina WANAFUNZI 556. Shule ina Vyumba vinane (8) vya Madarasa, na inapungukiwa vinne (4)

MWALIMU MKUU huyo ameeeleza UFAULU wa Shule yao wa Mwaka jana (2020) wa Kidato cha PILI (II) na NNE (IV) kama ifuatavyo:

**KIDATO CHA II MWAKA 2020**
Daraja la I = Wanafunzi 5 (ME 4 na KE 1)
Daraja II = 7 (ME 6, KE 1)
Daraja III = 13 (ME 10, KE 3)
Daraja IV = 51 (ME 24, KE 27)
Daraja 0 = 7 (ME 5, KE 2)

**KIDATO CHA IV MWAKA 2020**
Daraja I = Wanafunzi 3 (ME 3, KE 0)
Daraja II = 4 (ME 4, KE 0)
Daraja III = 8 (ME 7, KE 1)
Daraja IV = 50 (ME 28, KE 12)
Daraja 0 = 24 (ME 7, KE 17)

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# WANAKIJIJI WAANZA KUTEKELEZA MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VIPYA 17 VYA MADARASA YA SHULE YAO YA MSINGI

Posted on June 14, 2021



*Viongozi wa Serikali ya Kijiji cha Nyambono na Mwalimu Mkuu wa S/M Nyetasyo wakishiriki kwenye Mradi wa ujenzi wa VYUMBA VIPYA 17 vya Shule hiyo iliyoko Kijijini Nyambono, Kata ya Nyambono.*

UONGOZI wa Serikali ya Kijiji cha Nyambono kwa kushirikiana na Wananchi wa Kijiji hicho wameanza kutekeleza MRADI wa ujenzi wa VYUMBA VIPYA 17 vya Madarasa kwenye Shule yao ya Msingi, S/M NYETASYO.

Shule ya Msingi Nyetasyo yenye wanafunzi 873 ni moja kati ya Shule mbili za Msingi zilizopo Kijijini Nyambono. Shule hii ilianzishwa Mwaka 1944 ikiwa inamilikiwa na Kanisa la Mennonite. Mwaka 1978, Shule ilitaifishwa na Serikali.

MWALIMU MKUU wa S/M Nyetasyo, Mwl Rutoryo Hitra ameelezea MAHITAJI ya Shule hiyo kama ifuatavyo:
*Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 23, vilivyopo ni 6
*Madarasa yanayosomea nje ni mawili (Darasa la Awali na Darasa la II).

MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani ni mikubwa:
*Darasa la III lina chumba kimoja chenye Wanafunzi 121
*WALIMU wanaohitajika ni 23, waliopo ni 9
*NYUMBA za Walimu zinahitajika 23, zilizopo ni 4
*VYOO vya Wanafunzi – yanahitajika Matundu 39, yaliyopo ni 10
*CHOO cha Walimu – yanahitajika Matundu 2, hakuna hata tundu moja.

**UFAULU WA MITIHANI KWENYE S/M NYETASYO:**
*DARASA la IV (2020)
Watahiniwa: 113
Waliofaulu: 110

***DARASA LA VII (2020)**
*Watahiniwa: 62
*Waliofaulu: 45

**WANAKIJIJI WAFANYA MAAMUZI YA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWENYE SHULE YAO**
AFISA MTENDAJI (VEO) wa Kijiji cha Nyambono, Ndugu Mugeta Kaitira amesema SERIKALI ya KIJIJI chao imekubaliana na WANAKIJIJI kuanza kutekeleza MRADI wa ujenzi wa Vyumba vipya 17 vya Madarasa ya Shule yao, na kwamba WANAKIJIJI watachangia:
*FEDHA taslimu, Tsh 11,500/= kutoka kila kaya
*NGUVUKAZI ya kusomba mchanga, mawe, kokoto na maji ya ujenzi.

**MICHANGO ILIYOKWISHATOLEA**
*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo ameishatoa michango yake kama ifuatavyo:
(i) Madawati 60
(ii) Vitabu zaidi ya 1,000 vya Maktaba

*MFUKO wa JIMBO umechangia
(i) Tsh Milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba vipya vitatu (3) vya Madarasa.

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA NYAMBONO**
Wananchi wa Kijiji cha Nyambono wanawaomba WAZALIWA wa Kijiji hicho, na WADAU mbalimbali wa MAENDELEO wawaunge mkono kwenye MIRADI ya ujenzi na uboreshaji wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye S/M NYETASYO

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAKIJIJI WASHIRIKIANA NA SERIKALI KUONGEZA VYUMBA VYA MADARASA KWENYE S/M BULINGA

Posted on June 6, 2021



*MATUNDA ya USHIRIKIANO wa WANAKIJIJI na SERIKALI kwenye ujenzi na ukamilishaji wa Vyumba vipya 3 vya Madarasa na Choo chenye Matundu 6 kwenye S/M BULINGA B ya Kijijini Bugunda, Kata ya Bwasi.*

SHULE ya MSINGI BULINGA B ilifunguliwa Mwaka 2014. Shule hii ipo Kijiji cha Bugunda, Kata ya Bwasi.

MWALIMU MKUU wa Shule hii, Mwalimu Marwa James ameelezea yafuatayo kuhusu Vyumba vya Madarasa vya Shule hiyo:
*Idadi ya Wanafunzi ni 672
*Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 15, vilivyopo ni 6.
*Mirundikano ya Wanafunzi madarasani ni mikubwa. Kwa mfano, Darasa la IV lina Wanafunzi 145 kwenye chumba kimoja cha darasa.

**MCHANGO WA SERIKALI WA KUTATUA TATIZO LA UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA**

Serikali kupitia Mradi wake wa EP4R imetoa Tsh MILION 65.5 kwa ajili ya ujenzi wa:
*Vyumba vipya 3 vya Madarasa
*Choo chenye Matundu 6

*Ununuzi wa Madawati 69
*Ununuzi wa Matenki 3 ya Maji

MTENDAJI KATA wa Kata ya Bwasi, Ndugu Mashaka Kagere amesema WANAKIJIJI wameshiriki vizuri sana kwenye MRADI huu kwa kufanya yafuatayo:
*kuchimba msingi wa Vyumba vipya 3 vya Madarasa
*kuchimba shimo la choo
*kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi

VIONGOZI na WANAKIJIJI wa Kijiji cha Bugunda wanaishukuru sana SERIKALI kwa mchango wake ambao utapunguza tatizo la uhaba wa Vyumba vya Madarasa kwenye Shule ya Kijijini mwao.

**MICHANGO MINGINE ILIYOTOLEWA KWENYE S/M BULINGA B**
*PCI Tanzania imechangia:
(i) Ujenzi wa Matundu 6 ya choo
(ii) Huduma ya chakula shuleni hapo

*MBUNGE wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo ameishachangia:
(i) Saruji Mifuko 60
(ii) Madawati 70
(iii) Vitabu vingi vya Maktaba

**UFAULU WA MITIHANI KWENYE S/M BULINGA B**
*MATOKEO ya Darasa IV (2020)
Watahiniwa 82
Waliofaulu 70
MATOKEO ya Darasa la VII (2020)
Watahiniwa 55
Waliofaulu 27

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA BUGUNDA**
WAZALIWA wa Kijiji cha Bugunda na Kata ya Bwasi kwa ujumla wake, WANAOMBWA wachangie MAENDELEO ya nyumbani kwao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAKIJIJI WANAENDELEA KUTATUA TATIZO LA UPUNGUFU WA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWENYE SHULE YAO

Posted on June 1, 2021



*Ukamilishaji wa Vyumba vipya vya Madarasa na Ofisi ya Walimu kwenye S/M Etaro ya Kijiji cha Etaro, Kata ya Etaro*

SHULE ya MSINGI ETARO ilifunguliwa Mwaka 1995. Shule hii iko Kijijini Etaro, Kata ya Etaro.

MWALIMU MKUU wa Shule hii, Mwl Mangire Mahombwe ameeleza yafuatayo:
*Shule ina jumla ya Wanafunzi 1,079 na ina Walimu 14.
*Shule ina Vyumba vya Madarasa 9, vinavyohitajika ni 23.
*Mirundikano madarasani ni mikubwa mno. Kwa mfano, Darasa la Saba (VII), Wanafunzi wote 154 wanasomea kwenye chumba kimoja (1) cha darasa.
*Shule ina matundu 30 ya choo, yanayohitajika ni 48.

### UONGEZAJI WA VYUMBA VIPYA VYA MADARASA NA OFISI YA WALIMU

UJENZI wa Vyumba vipya vitano (5) vya Madarasa na Ofisi moja (1) ya Walimu wa Shule hii ulianza Mwaka 2017.

**MICHANGO YA UJENZI WA VYUMBA VIPYA 5 VYA MADARASA & OFISI 1 YA WALIMU**

MTENDAJI wa KIJIJI cha Etaro (VEO), Ndugu Sophia Anthony ameelezea uchangiaji wa ujenzi unaondelea kwenye S/M ETARO ni kama ifuatavyo:

*NGUVUKAZI za Wanakijiji cha Etaro: wanasomba mawe, kokoto, mchanga na maji

*FEDHA taslimu, Tsh 10,000/= (elfu kumi) zinachangwa kutoka kila KAYA. Kijiji kina KAYA 556.

*PCI Tanzania imejenga matundu 10 ya choo – Ahsante sana PCI Tanzania!

*MNARA wa SIMU, HALOTEL umechangia
(i) Saruji Mifuko 60
(ii) Mabati 54
(Ahsante sana HALOTEL)

*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo, amechangia:
(i) Saruji Mifuko 60
(ii) Mabati 54
(iii) Madawati 227
(iv) Vitabu vya Maktaba zaidi ya 1, 000 (elfu moja)

*MFUKO wa JIMBO umechangia:
(i) Mabati 244

*MKUU wa MKOA, Marehemu Mhe Tupa: Mwaka 2012, alitoa Tsh. MILIONI 10 kwa ajili ya Mradi wa Maji Kata ya Etaro.

Kata hiyo ilipopata Mradi mwingine wa Maji, fedha hizo zimetumika kwenye ujenzi huu.

**UFAULU WA S/M ETARO**

Mbali ya upungufu mkubwa wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye Shule hii, UFAULU wake ni wa kuridhisha:

**MATOKEO YA DARASA LA IV (2020):**
* Watahiniwa 96
* Waliofaulu 93

**MATOKEO YA DARASA LA VII (2020):**
* Watahiniwa 90
* Waliofaulu 72

**OMBI KUTOKA KWA WANAKIJIJI CHA ETARO**
WAZALIWA wa Kijiji cha Etaro na Kata ya Etaro kwa ujumla, na WADAU wengine wa MAENDELEO, wanaombwa KUCHANGIA ujenzi na uboreshaji wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye Shule yao (S/M Etaro).

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU KWENYE SHULE ZA MUSOMA VIJIJINI UNAENDELEA: VYOO VIPYA VYAJENGWA SHULENI LYASEMBE

Posted on April 8, 2021



*MAJENGO na UKAMILISHAJI wa MATUNDU 22 ya CHOO KIPYA cha S/M Lyasembe ya Kijijini Lyasembe, Kata ya Murangi.*

SERIKALI yetu imetoa SHILINGI 31,936,072.11 (Tsh Milioni 31.94) kuchangia ujenzi wa VYOO VIPYA kwenye Shule ya Msingi LYASEMBE ya Kijijini Lyasembe, Kata ya Murangi.

WANAKIJIJI wamejitolea kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji (NGUVUKAZI) kwa ajili ya ujenzi wa MATUNDU MAPYA 22 ya CHOO KIPYA cha Shule yao ya Msingi.

MWALIMU MKUU wa Shule hiyo, Mwl Athuman Mnkende amesema Shule ilianza Mwaka 1975 na ina jumla ya WANAFUNZI 872.

SHULE hiyo inapaswa kuwa na MATUNDU 40 ya CHOO. Ujenzi wa kutumia FEDHA zilizotolewa na SERIKALI, na NGUVUKAZI za WANAKIJIJI, umewezesha kukamilisha CHOO KIPYA chenye MATUNDU 22 na kufanya Shule hiyo kuwa na VYOO 2 vyenye jumla ya MATUNDU 28 (13 Wasichana, 13 Wavulana na 2 Walimu).

MWALIMU MKUU huyo anaishukuru sana SERIKALI yetu kwani vyoo vilivyokuwa vinatumiwa ni vya muda mrefu (1975) na vilikaribia kujaa. Kwa hiyo, bila msaada wa SERIKALI, Shule ingalifungwa kwa kukosa Vyoo vya Wanafunzi.

MTENDAJI wa Kijiji cha Lyasembe, Ndugu Chikonya Chikonya anawashukuru sana WANAKIJIJI kwa MCHANGO wa NGUVUKAZI zao uliowezesha ujenzi kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

DIWANI wa Kata ya Murangi, Mhe Hamisi Nyamamu amewasihi wanafunzi na walimu kutunza na kudumisha usafi wa choo hicho kipya ambacho kimejengwa kwa USHIRIKIANO wa Serikali yetu na Wananchi wa Kijiji cha Lyasembe.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ameishaichangia S/M Lyasembe:
*Madawati 80
*Vitabu vingi vya Maktaba

*Madarasa yanayohitajika ni 20 yaliyopo ni 10

**MATOKEO YA MITIHANI YA MWAKA JANA (2020)**

*STD IV (2020)
Watahiniwa 104
Waliofaulu 99 (95.2%)

*STD VII (2020)
Watahiniwa 70
Waliofaulu 43 (61.4%)

**TUCHANGIE UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA S/M LYASEMBE**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA – MAKTABA ZAENDELEA KUJENGWA KWENYE SHULE ZA MSINGI

Posted on March 19, 2021



*Katika MATUKIO mbalimbali kwenye S/M KARUBUGU ya Kijijini Kurwaki, Kata ya Mugango, Prof Sospeter Muhongo alitembelea Darasa la III la Shule hiyo kushuhudia mirundikano ya wanafunzi madarasani.*

WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kushirikiana na SERIKALI kuboresha mazingira ya KUJIFUNZIA na KUFUNDISHIA kwenye SHULE za MSINGI na SEKONDARI za Jimboni mwetu.

## UJENZI WA MAKTABA KWENYE S/M KARUBUGU

KIJIJI cha KURWAKI kimeamua kujenga MAKTABA kwenye Shule yao ya Msingi, S/M KARUBUGU, iliyofunguliwa Mwaka 1963.

MWALIMU MKUU wa Shule hii, Mwl Rehema Ramadhan amesema kwamba Shule ina jumla ya WANAFUNZI 830 na WALIMU 5.

## UFAULU WA MITIHANI YA MWAKA JANA (2020)

MWALIMU MKUU huyo ameeleza UFAULU huo kama ifuatavyo:

STD IV (2020)
*Watahiniwa: 82
*Waliofaulu: 82

STD VII (2020)
*Watahiniwa: 73
*Waliofaulu: 60

**UJENZI WA MAKTABA YA KISASA**

MTENDAJI wa Kijiji cha Kurwaki, Ndugu Abeid Makamba Ndagala amesema kwamba ujenzi wa MAKTABA ya S/M KARUBUGU ulianza Jumatatu, 8.3.2021 na wanakusudia kukamilisha ujenzi wa BOMA la MAKTABA kabla ya tarehe 30.3.2021.

**WACHANGIAJI WA UJENZI HUU**

*WANAKIJIJI:
Wanachangia NGUVUKAZI kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.
*WANAKIJIJI wanachangia FEDHA taslimu Tsh. 5,000/= kwa kila KAYA.
*MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo anachangia SARUJI ya UJENZI wa BOMA la MAKTABA hii. Leo,16.3.2021 amechangia SARUJI MIFUKO 50 ataendelea kuchangia hadi Boma likamilike.
*PCI (TANZANIA) itafadhili umaliziaji wa ujenzi wa MAKTABA hiyo baada ya kukabidhiwa BOMA linalojengwa na WANAKIJIJI. Aidha, PCI (TANZANIA) itaweka SAMANI zinazohitajika kwenye MAKTABA hiyo.

**VITABU VYA MAKTABA YA S/M KARUBUGU**

Wachangiaji wa VITABU vya MAKTABA hiyo ni:
*PCI (Tanzania)
*MBUNGE wa Jimbo

Kazi mbalimbali kwenye S/M KARUBUGU ya Kijijini Kurwaki, Kata ya Mugango.
*Ufyatuaji wa matofali ya ujenzi wa Maktaba.
*Uchimbaji wa Msingi wa Boma la Maktaba
*Ujenzi wa Msingi wa Boma la Maktaba

*Mirundikano ya Wanafunzi madarasani. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo alitembelea Darasa la III la Shule hiyo kushuhudia mirundikano ya Wanafunzi madarasani.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SERIKALI YASHIRIKIANA NA WANAKIJIJI KUTATUA MATATIZO YA UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA

Posted on March 14, 2021



*Ujenzi unaondelea (Vyumba vya Madarasa & Vyoo) kwenye S/M BUSEKERA ya Kijijini Busekera, Kata ya Bukumi.*

SHULE YA MSINGI BUSEKERA ilifunguliwa Mwaka 1954. Shule hii iko Kijijini Busekera, Kata ya Bukumi.

MWALIMU MKUU wa Shule hii, Mwl Kevin Majogoro amesema kwamba Shule ina jumla ya WANAFUNZI 1,271.

MAHITAJI ya Madarasa ni Vyumba 24, vilivyopo ni 10!

MIRUNDIKANO ya WANAFUNZI madarasana ni mikubwa. Kwa mfano, Darasa la AWALI lina Wanafunzi 234 kwenye chumba kimoja na Darasa la VII lina Wanafunzi 111 ndani ya chumba kimoja!

**SERIKALI YATOA MCHANGO WA KUJENGA MADARASA NA VYOO**

SERIKALI kupitia MRADI wake wa EP4R imetoa Tsh MILIONI 47.7 kwa ajili ya ujenzi wa VYUMBA 2 vya MADARASA na CHOO chenye MATUNDU 7 ya S/M Busekera.

**MICHANGO YA WANAKIJIJI**

MTENDAJI wa Kijiji cha Busekera, Ndugu Faustine Majura amesema WANAKIJIJI wameshirikishwa kwa:
*kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji
*kuchimba shimo la choo
*kuchimba msingi wa Vyumba 2 vya madarasa.

**SHUKRANI KWA SERIKALI YETU**

Wananchi na Viongozi wa Kijiji cha Busekera WANAISHUKURU sana SERIKALI kwa kuwachangia Tsh Milioni 47.7.

**MICHANGO YA MBUNGE WA JIMBO**

MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo amekuwa akihamasisha na kuchangia uboreshaji wa MAZINGIRA ya KUJIFUNZIA na KUFUNDISHIA kwenye SHULE zote za Jimboni mwao.

MICHANGO ya Mbunge huyo kwenye S/M Busekera ni:
*Saruji Mifuko 60
*Mabati 54
*Madawati 94
*Vitabu vingi vya Maktaba

MATOKEO ya DARASA la IV (2020):
*Watahiniwa 123
*Waliofaulu 120

MATOKEO ya DARASA la VII (2020):
*Watahiniwa 69
*Waliofaulu 45

**TUCHANGIE KUBORESHA UFAULU WA S/M BUSEKERA**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijni.or.tz

# WANAFUNZI WASIOJUA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) WAPUNGUA KWA KASI KUBWA NA UTORO WATOWEKA BAADA YA KITONGOJI CHA MWIKOKO KUJENGA SHULE YAKE

Posted on February 22, 2021



*Ujenzi unavyoendelea kwenye Shule Shikizi MWIKOKO ya Kitongoji cha Mwikoko, Kijijini Chitare, Kata ya Makojo.*

WANAVIJIJI wa JIMBO la Musoma Vijijini wanaendelea KUSHIRIKIANA na SERIKALI kuboresha MAZINGIRA ya kujifunzia na kufundishia WANAFUNZI wa SHULE za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) yenye Jimbo la Musoma Vijijini.

**UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA MSINGI**

*VYUMBA vipya 395 vya Madarasa vimejengwa kwenye Shule za Msingi za Serikali (111) ndani ya Miaka 5 (2015-2020)

MICHANGO ya ujenzi huo imetolewa na Wanavijiji, Serikali, Madiwani, Mbunge wa Jimbo na baadhi ya Wazaliwa wa Vijiji husika.

*SHULE SHIKIZI 12 zinajengwa na kupanuliwa kuwa Shule za Msingi kamili

MICHANGO ya ujenzi huo inatolewa na Wanavijiji, Serikali, Madiwani, Mbunge wa Jimbo na baadhi ya Wazaliwa wa Vijiji husika.

*MAKTABA za Shule za Msingi zinaendelea kujengwa na kufunguliwa

MICHANGO ya ujenzi wa MAKTABA inatolewa na Wanavijiji, PCI TANZANIA, Madiwani, Mbunge wa Jimbo na baadhi ya Wazaliwa wa Vijiji husika.

*VYOO vya kutosha vimejengwa kwa wingi kwenye Shule za Msingi – ahsante sana PCI TANZANIA kwa mchango wenu mkubwa kwenye ujenzi wa vyoo mashuleni. Wanavijiji wamechangia nguvukazi.

**SHULE SHIKIZI MWIKOKO**

Shule Shikizi Mwikoko ipo kwenye Kitongoji cha Mwikoko, Kijijini Chitare, Kata ya Makojo

WANAFUNZI 299 wa chini ya miaka minane (8), yaani Darasa la CHEKECHEA hadi la PILI wameacha kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 4 kwenda masomoni kwenye Shule za Msingi za CHITARE A & B.

MWALIMU Magige Simon, Msimamizi na Mlezi wa Shule Shikizi Mwikoko amesema uwepo wa Shule hiyo kwenye Kitongoji hicho, umezaa matunda mazuri yafuatayo:

(i) UTORO unatoweka na Wanafunzi wanazidi kupenda shule
(ii) IDADI ya WANAFUNZI wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) INAPUNGUA kwa kasi kubwa mno kwa Wanafunzi wa Darasa la I & II wa Kitongoji hicho

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Mwikoko, Ndugu Athuman Mtembela anawashukuru wale wote wanaochangia ujenzi wa shule yao.

**MICHANGO YA UJENZI WA SHULE SHIKIZI MWIKOKO**

(i) WANAKIJIJI – nguvukazi (kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji) na fedha taslimu Tsh 10,300 kutoka kwa kila KAYA.

(ii) SERIKALI kupitia Mradi wake wa EQUIP umechangia Tsh Milioni 60.

(iii) DIWANI wa Kata, Mhe Kuyenga Masatu amechangia Tsh 500,000

(iv) MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo amechangia SARUJI MIFUKO 100.

(v) MFUKO wa JIMBO umechangia SARUJI MIFUKO 80 na MABATI 108.

MALENGO ya Wakazi wa Mwikoko ni kwamba ifikapo Mwakani (2022) Shule Shikizi yao iwe Shule kamili ya Msingi yenye MADARASA 7.

**KUMBUKA:**
Kwa miaka 2 mfululizo (2019 & 2020) WANAFUNZI wa Darasa la IV wa Musoma Vijijini WAMEONGOZA Mkoa wa Mara kwenye MITIHANI ya Darasa la IV.

*Tuendelee kuboresha MAZINGIRA ya kujifunzia na kufundishia WANAFUNZI wetu – TUTAFANIKIWA!

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## UJENZI NA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU WAPANDISHA UFAULU WA SHULE ZA MSINGI

Posted on January 27, 2021

UFAULU WA HALMASHAURI ZA MKOA WA MARA KATIKA UPIMAJI WA SFNA 2020

| | HALMASHAURI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| 1 | MUSOMA DC | 98.04 |
| 2 | RORYA | 96.8 |
| 3 | MUSOMA MC | 96.11 |
| 4 | TARIME DC | 93.73 |
| 5 | BUTIAMA | 93.72 |
| 6 | BUNDA DC | 92.95 |
| 7 | TARIME TC | 90.3 |
| 8 | SERENGETI | 87 |
| 9 | BUNDA TC | 77.9 |
| | MKOA WA MARA | 91.83 |

*Matokeo ya Darasa la Nne ya Mwaka jana (SFNA 2020) ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Mara.*

MICHANGO ya WANAVIJIJI, SERIKALI, MBUNGE wa JIMBO na MADIWANI yawezesha Jimbo la Musoma Vijijini kujenga VYUMBA VIPYA 395 vya MADARASA kati ya Mwaka 2015 na 2020.

VYUMBA VIPYA hivyo 395 vimejengwa kwenye SHULE za MSINGI 111 na SHULE SHIKIZI 14.

**MUSOMA VIJIJINI YAONGOZA MKOA**

Kwa miaka miwili mfululizo (2019 & 2020) Shule za Msingi za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) ZIMEFANYA VIZURI na kuongoza Mkoa wa Mara kwenye MITIHANI ya DARASA la NNE (SFNA, standard four national assessment) na Mwaka jana (2020) ufaulu ulikuwa wa kiwango cha 98.04% – PONGEZI NYINGI ziende kwa Wanafunzi, Walimu, Wazazi, DC Dr Anney Naano & Timu yake, na DEO (Elimu ya Msingi) & Timu yake.

Kwa miaka ya nyuma, Halmashauri yetu ilikuwa inashikilia mkia Mkoani Mara. Haya ni MABADILIKO MAKUBWA yaliyochangiwa na UJENZI na UBORESHAJI wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye Shule za MSINGI za Halmashauri hii.

**VYUMBA VIPYA VYA MADARASA VYAENDELEA KUJENGWA**

Mbali ya ujenzi wa Vyumba vipya 395 ndani ya miaka 5, MBUNGE wa JIMBO na MADIWANI wa Kata zote 21 WAMEAMUA kwamba ifikapo tarehe 1.7.2021, SHULE zote za MSINGI hazitakuwa na MADARASA CHINI ya MITI.

Vilevile, MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani itapungua kwa kiasi kikubwa.

WANAVIJIJI wanaomba SERIKALI yao iendelee kuchangia ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa kwenye Shule zao.

**UJENZI WA MAKTABA KWENYE SHULE ZA MSINGI**

JIMBO la Musoma Vijijini LINAENDELEA kujenga MAKTABA kwenye Shule zake za Msingi.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo anaendelea kugawa VITABU kwenye Shule zote za Msingi na Sekondari. VITABU hivi ni vya Maktaba za Shule na vingi ni vya Masomo ya Sayansi na Lugha ya Kiingereza.

**PCI TANZANIA YATOA MICHANGO MIKUBWA**

PCI Tanzania inaendelea kuchangia ujenzi wa MAKTABA na utoaji wa VITABU kwenye Maktaba hizo – Ahsante sana PCI Tanzania.

PICHA zilizoko ukurasa wa 71 zinaonyesha:

*Maktaba ya S/M Butata (Jengo lenye rangi ya krimu) – Wanafunzi wakiwa ndani ya Maktaba hiyo.

*Maktaba ya S/M Rukuba (Jengo lenye rangi nyeupe). Hii Maktaba iko Kisiwani Rukuba

*Matokeo ya Darasa la Nne ya Mwaka jana (SFNA 2020) ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Mara (angalia ukurasa wa 69)



*wanafunzi wakiwa ndani ya Maktaba ya S/M Butata*



*Maktaba ya S/M Butata (Jengo lenye rangi ya krimu)*



*Maktaba ya S/M Rukuba (Jengo lenye rangi nyeupe). Hii Maktaba iko Kisiwani Rukuba*

# KITONGOJI CHA NYASAENGE CHAAMUA KUJENGA SHULE YAKE YA MSINGI

Posted on January 5, 2021



*MIUNDOMBINU ya SHULE SHIKIZI NYASAENGE inayojengwa ndani ya Kitongoji cha Nyasaenge, Kijiji cha Kataryo, Kata ya Tegeruka.*

WATOTO wa Kitongoji cha NYASAENGE wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 10 kwenda masomoni kwenye SHULE ya Msingi KATARYO.

Kitongoji cha NYASAENGE ni moja kati ya VITONGOJI 6 (sita) vya Kijiji cha KATARYO. Kijiji hiki ni moja ya Vijiji 3 (Kataryo, Mayani na Tegeruka) vya Kata ya TEGERUKA

Kijiji cha KATARYO kina SHULE 2 za MSINGI, yaani KATARYO na KATARYO B.

WANANCHI wa Kitongoji cha NYASAENGE wameamua kutatuta tatizo la umbali mrefu unaotembewa na WATOTO wao kwenda masomoni kwa KUJENGA SHULE yao ya MSINGI, ambayo itaanza ikiwa SHULE SHIKIZI NYASAENGE.

MIUNDOMBINU ya SHULE SHIKIZI hiyo inayokamilishwa ni:
*Vyumba 2 vya Madarasa
*Ofisi 1 ya Walimu
*Choo chenye Matundu 8

Kwa hiyo, WANANCHI wa KITONGOJI cha NYASAENGE wanaomba WATATO wao waanze MASOMO yao ya AWALI kwenye Shule Shikizi yao itakayotambuliwa na Halmashauri yetu.

MRATIBU wa Elimu Kata ya Tegeruka, Ndugu Modest Fadhili amesema kuwa jumla ya WANAFUNZI 149 wa Darasa la Awali wanasomea CHINI ya MTI hapo Kitongojini Nyasaenge wakifundishwa na MWALIMU wa KUJITOLEA, Ndugu Mauna Rugeye.

**KITONGOJI CHA NYASAENGE CHAFANYA VIZURI MASOMONI**

Mbali ya umbali mrefu wa kutembea, WANAFUNZI wa kutoka Kitongoji cha NYASAENGE, wamefaulu vizuri Mitihani ya Darasa la VII (2020) wakishinda Vitongoji vingine vitano (5).

Matokeo ya Darasa la VII (2020) ni haya hapa:

**S/M Kataryo:**

Kati ya Wanafunzi 16 waliofaulu, jumla ya Wanafunzi 11 (Wasichana 6 na Wavulana 5) wametoka Kitongoji cha Nyasaenge

**S/M Kataryo B**

Kati ya Wanafunzi 37 waliofaulu, jumla ya Wanafunzi 13 (Wasichana 8 na Wavulana 5) wametoka Kitongoji cha Nyasaenge

**WACHANGIAJI WA UJENZI HUU**

(i) WANANCHI

*NGUVUKAZI – kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji
*FEDHA taslimu – kila KAYA inachangia Tsh 30,000/=

(ii) **WAZALIWA WA KITONGOJI CHA NYASAENGE**

Fedha taslimu zimechangwa kutoka kwa:
*Saguda Paliga 100,000/=
*Madete Washuli 100,000/=
*Gubi Gong'oma 100,000/=
*Maiku Lyangeni 100,000/=

**(iii) MBUNGE WA JIMBO**
*Prof Sospeter Muhongo atachangia MABATI 54.
MBUNGE huyo ametoa MICHANGO mingi kwa SHULE 2 za Kijiji cha KATARYO ambayo ni:

**S/M KATARYO**
*Madawati 76
*Vitabu vya Maktaba

**S/M KATARYO B**
*Saruji Mifuko 60
*Mabati 108
*Madawati 73
*Vitabu vya Maktaba

**MFUKO WA JIMBO umechangia**
*Mabati 54

**(S/M Kataryo B)**
MWENYEKITI wa Kitongoji cha Nyasaenge, Ndugu Kabole Mesogachura ametoa SHUKRANI nyingi kwa WACHANGIAJI wote wakiwemo WANANCHI wa Kitongoji cha NYASAENGE.

KIONGOZI huyo anaomba WADAU wa MAENDELEO waendelee kuwachangia VIFAA ZA UJENZI ili wakamilishe ujenzi wa SHULE SHIKIZI NYASAENGE ambayo itapanuliwa na kuwa SHULE YA MSINGI NYASAENGE.

WANAFUNZI 149 wa ELIMU ya AWALI wa Kitongoji cha NYASAENGE wataacha kusomea CHINI ya MTI baada ya kupata VYUMBA 2 vya Madarasa ya SHULE SHIKIZI NYASAENGE.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAKIJIJI WAUNGWA MKONO NA SERIKALI KUJENGA NYUMBA ZA WALIMU

Posted on December 8, 2020



*Ujenzi wa NYUMBA MOJA ya WALIMU (kuanzia msingi hadi nyumba kukamilika) ya S/M BUIRA ya Kijiji cha Buira, Kata ya Bukumi.*

MWALIMU MKUU wa SHULE ya MSINGI BUIRA, Mwl Yahya Mgika amesema Shule hiyo iliyoanzishwa Mwaka 1992 ina jumla ya WANAFUNZI 747, WALIMU 8, NYUMBA 5 za Walimu, na ina Vyumba 8 vya Madarasa – bado kuna UPUNGUFU wa Vyumba 9 vya Madarasa.

SERIKALI imetoa SHILINGI MILIONI 25 kuchangia ujenzi wa NYUMBA MOJA ya WALIMU kwenye Shule hii. Fedha hizo zimetoka kwenye MRADI wa SERIKALI uitwao, "Primary Education Development Project (PEDP)".

WANAKIJIJI wa Kijiji cha BUIRA, Kata ya BUKUMI wanaishukuru sana SERIKALI yetu kwa kutoa FEDHA hizo, na wao wamechangia NGUVUKAZI kuhakikisha kwamba gharama za ujenzi wa nyumba hiyo zinapungua – wamejitolea kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

MWENYEKITI wa Kijiji cha BUIRA, Ndugu Donald Mafwere ameeleza kwamba, mbali ya MCHANGO wa NGUVUKAZI, Wanakijiji walichangia SARUJI MIFUKO 70, MBAO vipande 101 na MABATI 52 kwenye ujenzi huu.

MWENYEKITI huyo anawashukuru sana WANAKIJIJI hao kwa kuona umuhimu wa KUJITOLEA kwa ajili ya MAENDELEO yao wenyewe wakisaidiana na SERIKALI yetu. Wanavijiji hawa walishajenga NYUMBA 4 za WALIMU wa Shule hiyo.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo anapewa SHUKRANI nyingi kwa kuichangia Shule hiyo MADAWATI 60, VITABU zaidi ya 1,000 vya Maktaba, SARUJI MIFUKO 60, na MABATI 54.

VIONGOZI 2 hao, yaani Mwenyekiti wa Kijiji na Mwalimu Mkuu, kwa pamoja wanaomba WADAU wa MAENDELEO wakiwemo WAZALIWA wa Kata ya BUKUMI wajitokeze kuchangia ujenzi wa Vyumba Vipya vya Madarasa, Nyumba Mpya za Walimu na Maktaba – MPANGOKAZI wa ujenzi umeishatayarishwa.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# CRDB YAUNGANA NA WANAKIJIJI KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SHULE YA MSINGI ILIYOFUNGULIWA MWAKA 1956

Posted on November 27, 2020



*Baadhi ya MAJENGO yaliyokamilika ujenzi na MADARASA ya S/M MURUNYIGO ya Kijiji cha Kiemba, Kata ya Ifulifu.SHULE ya MSINGI MURUNYIGO ya Kijiji cha Kiemba, Kata ya Ifulifu ilianza kutoa ELIMU Mwaka 1956.*

SHULE hii ina WANAFUNZI 949 na WALIMU 12. IDADI ya WANAFUNZI kwenye chumba kimoja cha DARASA ni kati ya 80 na 152. Kwa hiyo, MIRUNDIKANO Madarasani ipo!

AFISA MTENDAJI (VEO) wa Kijiji cha Kiemba. Ndugu Regina Chirabo amesema kuwa UBORESHAJI wa MIUNDOMBINU ya S/M MURUNYIGO umefanywa na:

**WANAKIJIJI:**
Wamechangia NGUVUKAZI kwa kusomba mawe, mchanga, maji na FEDHA taslimu 2,200,000/= za malipo ya Fundi.

**BENKI YA CRDB**
Imechangia Saruji Mifuko 60, Rangi Lita 40, Vifaa vya Mlango 1 na Dirisha 1 – SHUKRANI nyingi sana kwa CRDB.

**PCI (TANZANIA)**
Imefadhili ujenzi wa Choo chenye Matundu 10 (Wasichana 5 na Wavulana 5 – kwenye picha iliyoko ukurasa wa 77 utaona Jengo la rangi ya “light blue”) – SHUKRANI nyingi sana kwa PCI (Tanzania).

**MBUNGE WA JIMBO**
Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo amechangia Saruji Mifuko 60 na Mabati 54.

MICHANGO mingine ya MBUNGE huyo kwenye Shule hiyo ni pamoja na: Madawati 150 na Vitabu vya Maktaba zaidi ya 1,000 (elfu moja).

MWALIMU MKUU huyo amesema Jumla vya Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 18 na vilivyopo ni 9 tu! Mbali ya UPUNGUFU mkubwa huo WANAFUNZI 59 kati ya 64 wamefaulu kujiunga MASOMO ya KIDATO I mwakani!

MWALIMU MKUU huyo anaendelea KUTOA OMBI kwa WADAU wa MAENDELEO kujitokeza na KUCHANGIA uboreshaji na ujenzi wa MIUNDOMBINU kwenye Shule kongwe ya Msingi ya Kijiji cha Kiemba, S/M MURUNYIGO.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SHULE ZA MSINGI ZA MUSOMA VIJIJINI ZAENDELEA KUJENGA NA KUTUMIA MAKTABA

Posted on November 22, 2020



*WANAFUNZI wakijipatia vitabu ndani ya MAKTABA yao.*

SHULE YA MSINGI BUTATA, iliyoko Kijijini Butata, Kata ya Bukima imejenga MAKTABA MPYA kwa muda wa MIEZI 8 na tayari inatumika.

MWALIMU MKUU, Mwl Nancy Lema amesema Shule hiyo iliyoanza Mwaka 1942, ina furaha nyingi sana ya KUPATA MAKTABA ambayo inatumiwa na WANAFUNZI wa Madarasa yote kujisomea na hasa kufanya kazi za ziada walizopewa na Walimu wao (homeworks)

**MICHANGO YA UJENZI WA MAKTABA**

Mwalimu Yohana Dawi, Mwalimu wa MIUNDOMBINU, aliyesimamia ujenzi wa Maktaba hii amesema MICHAGO ilitoka kwa:

*WAKIJIJI wa Kijiji cha Butata walichangia NGUVUKAZI – kusomba mawe, mchanga na maji.

*PCI (Tanzania) inapewa shukrani nyingi sana kwa kutoa Vifaa vingi vya ujenzi wa Maktaba hii. MEZA, VITI na SHUBAKA vimetolewa na PCI (Tanzania)

*MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo alichangia Shule hii SARUJI MIFUKO 100 (50 Maktaba & 50 Vyumba vipya vya Madarasa)
*WAZALIWA 2 wa Kijiji cha Butata, Ndugu Samson Masawa (Tsh 500,000) na Masawa Masawa (Tsh 500,000) walichangia

**VITABU VYA MAKTABA**
Mwl Yohana Dawi amesema VITABU vya MAKTABA hiyo vimetolewa na:
*PCI (Tanzania)
*MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo

**WATUMIAJI WENGINE WA MAKTABA HII**
Mbali ya WANAFUNZI wa S/M Butata, WANAFUNZI wa SHULE za MSINGI na SEKONDARI jirani, na WANANCHI wa Kata ya Bukima na wengine wote WANAKARIBISHWA kutumia MAKTABA ya S/M BUTATA – Karibuni Mjisomee!

JIMBO LA Musoma Vijijini lenye Kata 21, Vijiji 68 na Vitongoji 374 lina jumla ya SHULE za MSINGI 111 (za Serikali), 3 (za Binafsi) na linajenga Shule Mpya 14 za Msingi.

**ELIMU NI INJINI YA MAENDELEO**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SHULE MPYA 11 ZA MSINGI KUKAMILISHWA NDANI YA MIAKA 5 (2020-2025) – CHAGUA CCM, CHAGUA DKT MAGUFULI MIRADI IKAMILIKE

Posted on September 29, 2020




MWAKA jana (2019) SHULE za MSINGI za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC), yenye Jimbo la Musoma Vijijini, ziliongoza (NAMBA MOJA) Mkoa wa Mara kwenye MITIHANI ya Darasa la Nne (Std IV).

WANANCHI wa VIJIJI 11 ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini WAMEAMUA kujenga SHULE MPYA 11 za MSINGI kwa madhumuni ya kuongeza UBORA wa ELIMU itolewayo kwenye SHULE za MSINGI za maeneo yao.

Baadhi ya WANAFUNZI wa Shule za Msingi wanatembea umbali mrefu (kati ya kilomita 2 na 5) kwenda masomoni, na kwenye baadhi ya SHULE za MSINGI kuna MIRUNDIKANO mikubwa MADARASANI.

Kwa hiyo, WANANCHI, kwa kutumia NGUVUKAZI zao na kwa KUSHIRIKIANA na SERIKALI ya CCM, wameamua kutatua matatizo haya!

SHULE SHIKIZI 11 zinajengwa kwenye VIJIJI 11 vya Jimbo hili. Baadhi ya SHULE hizi tayari zina MADARASA ya AWALI na zimeanza kutoa MASOMO ya Darasa la Kwanza na Pili (Std I & II).

Ndani ya MIAKA 5 ya UTEKELEZAJI wa ILANI ya CCM (2020-2025), SHULE hizi 11 zitaendelea kujengwa na kukamilishwa, yaani kuwa SHULE za MSINGI kamili.

**CHAGUA CCM**
**CHAGUA MAENDELEO KWA VITENDO**

**ORODHA YA SHULE SHIKIZI ZINAZOJENGWA**:
(1) Binyango: Kijijini Kabegi, Kata ya Ifulifu
(2) Buanga: Kijijini Buanga, Kata ya Rusoli
(3) Buraga Mwaloni: Kijijini Buraga, Kata ya Bukumi
(4) Egenge: Kijijini Busamba, Kata ya Etaro
(5) Gomora: Kijijini Musanja, Kata ya Musanja
(6) Kaguru: Kijijini Bugwema, Kata ya Bugwema
(7) Karusenyi: Kijijini Mikuyu, Kata ya Nyamradirira
(8) Rwanga: Kijijini Kasoma, Kata ya Nyamradirira
(9) Mwikoko: Kijijini Chitare, Kata ya Makojo
(10) Kiunda: Kijijini Kamguruki, Kata ya Nyakatende
(11) Ziwa: Kijijini Mwiringo, Kata ya Busambara

MGOMBEA Ubunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO ni sehemu ya MAFANIKIO ya UJENZI wa SHULE SHIKIZI hizi. Baada ya UCHAGUZI ataendelea KUSHIRIKIANA na WANANCHI na SERIKALI ya CCM kukamilisha ujenzi wa SHULE hizi.

PICHA zilizoko kurasa za 83 na 84 zinaonyesha baadhi ya SHULE SHIKIZI zinazojengwa ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA.”**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
[www.musomavijijini.or.tz](http://www.musomavijijini.or.tz)


Shule Shikizi BUANGA


Shule Shikizi BURAGA MWALONI


Shule Shikizi KARUSENYI


Shule Shikizi RWANGA


Shule Shikizi KAGURU

## ELIMU & MAFUNZO – MAKTABA ZAJENGWA KWENYE SHULE ZA MSINGI ZA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on September 28, 2020



*Jengo la Tehama – Agape Primary School*

JIMBO la Musoma Vijijini tayari linatekeleza ILANI MPYA ya CCM (2020-2025) kwa SHULE za MSINGI kujenga MAKTABA zao.

**(1) SHULE YA MSINGI RUKUBA**

Hii iko Kisiwani Rukuba Kata ya Etaro. MAKTABA imekamilika na inatumika. Ujenzi wake ni mafanikio ya USHIRIKIANO wa WANANCHI, PCI (Tanzania – vifaa vingi vya ujenzi), PROF MUHONGO (Saruji Mifuko 50) na UONGOZI wa SHULE.

VITABU vya Maktaba vilitolewa na Prof Muhongo na PCI (USA).

**(2) SHULE YA MSINGI BUTATA**

Hii iko Kijijini Butata Kata ya Bukima. Ujenzi wake ni mafanikio ya USHIRIKIANO wa MiCHANGO ya WANANCHI, PCI (Tanzania – vifaa vingi vya ujenzi), PROF MUHONGO (Saruji Mifuko 50) na UONGOZI wa SHULE. VITABU vya Maktaba vitatolewa na Prof Muhongo na PCI (Tanzania).

**(3) SHULE YA MSINGI BUSAMBA**

Hii iko Kijiji cha Busamba Kata ya Etaro na inajengwa kwa USHIRIKIANO wa WANANCHI, PROF MUHONGO (Saruji Mifuko 60) na UONGOZI wa SHULE

(**4) SHULE YA MSINGI BURAGA**

Hii iko Kijiji cha Buraga Kata ya Bukumi. WANANCHI wamemuomba MGOMBEA UBUNGE wa CCM (Prof Muhongo) achangie ujenzi wake baada ya Uchaguzi wa tarehe 28.10.2020. Amepokea OMBI hilo na kukubali kushirikiana na Wananchi hao.

(**5) SHULE YA MSINGI BUIRA**

Hii iko Kijiji cha Buira Kata ya Bukumi. Ujenzi wake unafanana na ule wa S/M BURAGA (soma hapo juu).

**(6) AGAPE PRIMARY SCHOOL**

Hii ni SHULE ya PRIVATE (Binafsi) iliyoko kwenye Kata ya Bukima na inajenga JENGO la TEHAMA (angalia ukurasa wa 85 – Picha za Jengo lenye mabati ya rangi ya kijani).

PROF MUHONGO alishachangia VITABU vya MAKTABA na Saruji Mifuko 50 ya ujenzi wa Jengo la Tehama la Shule hii, na alihaidi kuchangia COMPUTERS.

SHULE NYINGINE za MSINGI za JIMBO la Musoma Vijijini zimeweka MIPANGO ya ujenzi wa MAKTABA zao.

PROF MUHONGO aligawa VITABU vingi vya MAKTABA kwenye SHULE zote za MSINGI za JIMBO hili (111 za Serikali & Agape ya Binafsi).

ILANI MPYA CCM (Elimu & Mafunzo) TAYARI INATEKELEZWA ndani ya JIMBO la Musoma Vijijini

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz



*Jengo la Maktaba Shule ya Msingi Rukuba*

# WANAVIJIJI WASHIRIKIANA NA SERIKALI KUBORESHA MAZINGIRA YA ELIMU – KITONGOJI CHAJENGA SHULE SHIKIZI

Posted on February 17, 2021



*Miundombinu ya SHULE SHIKIZI EGENGE inayojengwa ndani ya Kitongoji cha Egenge, Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro.*

JIMBO la MUSOMA laendelea kushirikiana na SERIKALI kutatua MATATIZO ya muda mrefu yaliyoko kwenye SEKTA ya ELIMU.

MATATIZO hayo ni:
*UMBALI mrefu wanaotembea WANAFUNZI kwenda masomoni
*MIRUNDIKANO ya WANAFUNZI Madarasani

**SULUHISHO:**
*UJENZI wa SHULE karibu na MAKAZI ya WANAVIJIJI
*UJENZI wa VYUMBA VIPYA vya MADARASA kwenye Shule zilizopo.

**TAKWIMU: SHULE ZA MSINGI**
*JIMBO lina KATA 21 zenye jumla ya VIJIJI 68
*SHULE za MSINGI za SERIKALI zipo 111

*SHULE SHIKIZI 12 zinajengwa na kupanuliwa kuwa Shule za Msingi kamili.
*SHULE za MSINGI za Binafsi zipo 3

*VYUMBA VIPYA 395 vya Madarasa vimejengwa ndani ya miaka mitano (2015-2020)

**KITONGOJI CHA EGENGE CHAJENGA SHULE SHIKIZI**
Kitongoji cha EGENGE ni moja kati ya VITONGOJI vinne (4) vya Kijiji cha BUSAMBA.

Kijiji hicho ni moja ya Vijiji 4 vya Kata ya ETARO. Vijiji vingine ni: Mmahare, Rukuba (Kisiwa) na Etaro.

WANAFUNZI wa Kitongoji cha EGENGE wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 7 kwenda masomoni kwenye Shule ya Msingi Busamba.

UMBALI mrefu na MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani ni sababu kuu zilizofanya KITONGOJI cha EGENGE kiamue kujenga SHULE SHIKIZI yake, na ujenzi ulianza rasmi Mwaka 2016.

MRATIBU wa ELIMU wa Kata ya Etaro, Ndugu Samwel Samike ameeleza kwamba Shule Shikizi hiyo ILIFUNGULIWA Mwaka 2019 na inao WANAFUNZI wa Madarasa matatu, yaani, Darasa la Awali hadi Darasa la Pili.

WINGI wa WANAFUNZI wa Shule Shikizi hiyo ni kama ifuatavyo

*Darasa la AWALI, Wanafunzi 50
*Darasa la KWANZA, 40
*Darasa la PILI, 33.

WANAFUNZI wa Darasa la TATU wa Kitongoji hicho bado wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita saba (7) kwenda masomoni kwenye S/M Busamba.

**UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE SHIKIZI**
*Vyumba 2 na Ofisi 1 vimejengwa na SERIKALI kupitia Mradi wake wa EQUIP

*Matundu 4 ya choo cha Wanafunzi (EQUIP)
*Matundu 2 ya choo cha Walimu (EQUIP)
*Vyumba 2 na Ofisi 1, SERIKALI kupitia Mradi wa EP4R
*Vyumba 4 na Ofisi 1 vinajengwa na WANAVIJIJI na VIONGOZI wao.

**MICHANGO INAYOTOLEWA KWENYE UJENZI HUU**
(i) WANAVIJIJI
*Nguvukazi – kusomba mawe, kokoto, maji na mchanga.
*Fedha taslimu – kila KAYA kuchangia Tsh 10,000/=

(ii) SERIKALI – WIZARA ZA ELIMU & TAMISEMI
*Mradi wa EQUIP umechangia Tsh Milioni 60
*Mradi wa EP4R umechangia Tsh Milioni 47.7

(iii) MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo ameanza kutoa MICHANGO yake kwa kuchangia SARUJI MIFUKO 50.

MWENYEKITI wa Kitongoji cha EGENGE, Ndugu Nkuyu Mururi ametoa SHUKRANI nyingi kwa WACHANGIAJI wote ikiwemo SERIKALI yetu.

KIONGOZI huyo anaomba WADAU wa MAENDELEO waendelee kuwachangia VIFAA VYA UJENZI, ambapo MAHITAJI yao kwa sasa ni MABATI 216 na SARUJI MIFUKO 200.

**UFAULU WA WATOTO KUTOKA KITONGOJI CHA EGENGE** (Darasa la VII 2020)

Kati ya Wanafunzi 53 waliofaulu kutoka S/ M Busamba, Watoto kutoka Kitongoji cha EGENGE wamefaulu saba (7) tu.

Hivyo ni muhimu sana kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wa Kitongoji cha Egenge – ujenzi wa SHULE SHIKIZI EGENGE ukamilike!

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA AFYA

## (30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)

**Tarehe 30 Juni 2021: Huduma za Afya Jimboni mwetu:**
*Hospitali ya Wilaya 1: ujenzi unaendelea
*Vituo vya Afya: 3 vinatoa huduma & 2 vinajengwa
*Zahanati: 23 Serikali & 4 Binafsi zinatoa huduma. 15 zinajengwa
*Magari ya Wagonjwa (Ambulances): 5 yanatoa huduma

# [WANAVIJIJI WASHIRIKIANA NA SERIKALI KUJENGA KITUO CHA AFYA CHA KATA YA BUGWEMA]

**Posted on** [November 27, 2020]



*Baadhi ya MAJENGO yanayojengwa kwenye Mradi wa kupanua ZAHANATI ya KIJIJI cha Masinono kuwa KITUO cha AFYA cha KATA ya Bugwema.*

SERIKALI imetoa TSH MILIONI 400 kupanua ZAHANATI ya Kijiji cha MASINONO iwe KITUO cha AFYA cha Kata ya BUGWEMA.

Kata ya BUGWEMA inaundwa na Vijiji vinne (4) ambavyo ni: Bugwema, Kinyang'erere, Masinono na Muhoji. Vijiji vyote hivi vinatumia ZAHANATI moja (1) tu ya Kijijini Masinono.

**UPANUZI WA ZAHANATI KUWA KITUO CHA AFYA**
Michango ya ujenzi inatolewa na:

**SERIKALI**:
Tsh Milioni 400 – SHUKRANI nyingi sana zinatolewa kwa Serikali yetu.

**WANAVIJIJI:**
Wanavijiji kutoka Vijiji vyote 4 na Viongozi wao wa Vijiji na Vitongoji wanachangia NGUVUKAZI zao kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji. Vilevile, wanachangia FEDHA taslimu.

**VIONGOZI WA KATA:**
Diwani Mteule, Mhe Clifford Machumu na Diwani aliyemaliza muda wake, Mhe Ernest Maghembe wanaendelea kuchangia FEDHA taslimu na USAFIRI kwenye ujenzi huu.

**MBUNGE WA JIMBO:**
Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, amechangia leo SARUJI MIFUKO 100 bado ataongezea Saruji Mifuko 300 kukamilisha AHADI yake.

MICHANGO mingine ya Mbunge wa Jimbo kwenye ZAHANATI ya Masinono ni kama ifuatavyo:

(i) Gari 1 la Wagonjwa (Ambulance).

(ii) Nondo, Wavu na Masinki kwa ajili ya ukarabati wa choo cha Zahanati ya Masinono

MSIMAMIZI MKUU wa Mradi huu, Injinia Mrisho Shomari amesema, hadi sasa Mradi huo umetekelezwa kwa Asilimia 75 (75%) na kufikia mwishoni mwa mwezi Disemba, 2020 ujenzi utakuwa umekamilika kwa Asilimia 100 (100%).

Injinia Mrisho ametaja majengo ya KITUO hiki cha AFYA kuwa ni:

(i) Wodi ya Mama na Mtoto
(ii) Maabara
(iii) Jengo la Upasuaji
(iv) Jengo la Kufulia
(v) Jengo la Maiti (mortuary)
(vi) Vyoo vya nje, na
(vii) Miundombinu ya kutolea uchafu.

MGANGA MFAWIDHI wa Zahanati ya Masinono, Ndugu Mzalendo Wambura amewaomba WADAU wa MAENDELEO wakiwemo WAZALIWA wa KATA ya BUGWEMA kuwaunga mkono Wananchi wa Kata ya Bugwema na Serikali ili kukamilisha Mradi huu mapema iwezekanavyo.

**MIUNDOMBINU YA HUDUMA ZA AFYA NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI**

*Zahanati 23 za Serikali
*Zahanati 4 za Binafsi
*Zahanati Mpya 14 zinajengwa
*Vituo vya Afya 2
(Murangi & Mugango)
*Hospitali ya Wilaya inajengwa Kijijini Suguti

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAVIJIJI WAENDELEA NA UJENZI WA ZAHANATI MPYA VIJIJINI MWAO

Posted on May 17, 2021



*Baadhi ya WANANCHI wa Kijiji cha NYABAENGERE, Kata ya MUSANJA, wakishirikiana na MAFUNDI wao kujenga msingi (foundation) wa ZAHANATI ya Kijiji chao.*

HUDUMA za AFYA ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) yenye Jimbo moja la Uchaguzi (Jimbo la Musoma Vijijini) ni hizi zifuatazo:

*Hospitali ya Wilaya ya Serikali: ujenzi unakamilishwa

*Vituo vya Afya 3 vya Serikali vinatoa huduma za Afya. Vituo hivi ni: Murangi, Mugango na Bugwema (Bugwema – ujenzi ni wa upanuzi wa Zahanati ya Masinono kuwa Kituo cha Afya, ujenzi unakamilishwa)

*Zahanati 23 za Serikali zinatoa huduma za Afya

*Zahati 4 za Binafsi zinatoa huduma za Afya.

*Zahanati Mpya 15 zinajengwa na Wanavijiji. Serikali imeanza kuchangia baadhi ya ujenzi wa Zahanati hizo.

JIMBO la Musoma Vijijini lina KATA 21 zenye VIJIJI 68 na VITONGOJI 374.

**KIJIJI CHA NYABAENGERE CHAAMUA KUJENGA ZAHANATI YAKE**

Wananchi wa Kijiji cha Nyabaengere kilichopo Kata ya Musanja wameanza ujenzi wa ZAHANATI yao wakiwa na LENGO KUU la kutatua tatizo lao la kutembea umbali mrefu wa zaidi ya KILOMITA 10 kwenda kutafuta HUDUMA za AFYA zilizoko Kata ya jirani ya Murangi – Kituo cha Afya Murangi.

DIWANI wa Kata ya Musanja, Mhe Ernest Mwira amesema ZAHANATI inayojengwa Kijijini hapo itakuwa na jumla ya VYUMBA 14.

HUDUMA za AFYA zitakazotolewa ni pamoja na:
*Kliniki ya Wajawazito na Huduma za Uzazi wa Mpango
*Huduma za Mama & Mtoto
*Matibabu mbalimbali na huduma nyingine za Afya

Diwani huyo amesema LENGO lao ni kukamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya KIJIJI cha NYABAENGERE ndani ya MWAKA MMOJA.

MAMA Sophia Otieno, Mkazi Kijiji cha Nyabaengere amesema kukamilika kwa Zahanati hiyo kutaondoa adha wanayoipata AKINA MAMA kujifungulia nyumbani na njiani, na wengine kupoteza maisha wakienda kujifungulia mbali kwenye Kituo cha Afya cha Murangi.

**MICHANGO YA UJENZI**

MTENDAJI wa Kata ya Musanja, Ndugu Michael Tafuna amesema ujenzi wa Zahanati hiyo utafanikishwa kwa MICHANGO ifuatayo:
*NGUVUKAZI za Wanakijiji za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi.
*Tsh 24,000 kutoka kwa kila Mwanakijiji mwenye nguvu za kufanya kazi
*MAPATO ya Kijiji yatokanayo na uuzaji wa rasilimali zao ambazo ni mchanga, mawe na kifusi.
*MAPATO kutoka kwenye ushuru wa mifugo.

*MICHANGO ya DIWANI, Mhe Ernest Mwira – atachangia SARUJI MIFUKO 20. Ameanza kwa kuchangia Saruji Mifuko 5.

*MICHANGO ya Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo.
Mbunge huyu atatumia mtindo wake wa kuchangia hatua zote za ujenzi kama afanyavyo kwingine Jimboni mwao, na kwa Zahanati hii ameanza kwa kuchangia ujenzi wa msingi kwa kutoa SARUJI MIFUKO 50.

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA NYABAENGERE**

Diwani na Wananchi wa Kijiji cha Nyabaengere wanawaomba WAZALIWA wa KIJIJI hicho na KATA ya MUSANJA kwa ujumla waungane na ndugu zao kuchangia ujenzi wa ZAHANATI hii. WADAU wengine wa MAENDELEO nao wanakaribishwa kutoa MICHANGO yao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## UBORESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA MUSOMA VIJIJINI UNAENDELEA – KIJIJI CHA NYABAENGERE CHAANZA KUJENGA ZAHANATI YAKE

Posted on February 22, 2021



*WANAVIJIJI wakisomba mawe kwa ajili ya ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao cha NYABAENGERE, Kata ya Musanja.*

WANAVIJIJI wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kushirikiana na SERIKALI, wameamua kujenga na kuboresha MIUNDOMBINU ya HUDUMA za AFYA ndani ya Vijiji vyao na Kata zao.

Mbunge wa Jimbo, Madiwani na Wazaliwa wa baadhi ya Vijiji wanachangia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu hiyo.

**ZAHANATI ZILIZOPO NA ZINATOA HUDUMA**
*Zahanati 23 za Serikali
*Zahanati 4 za Binafsi

**ZAHANATI MPYA ZINAZOJENGWA**
*Zahanati 15 zinajengwa

**WODI ZA MAMA & MTOTO ZINAZOJENGWA**
*Wodi 3 za Mama & Mtoto zinajengwa kwenye Zahanati za Bukima, Kisiwani Rukuba na Nyegina.

**VITUO VYA AFYA VINAVYOTOA HUDUMA**
*Vituo 2 vya Afya vya Murangi na Mugango vinatoa huduma.
*Zahanati ya Masinono inapanuliwa iwe Kituo cha Afya cha Kata hiyo ya Bugwema.

**HOSPITALI YA WILAYA INAJENGWA**
*Hospitali ya Wilaya inajengwa kwenye Kitongoji cha Kwikonero, Kijijini Suguti.

**KIJIJI CHA NYABAENGERE CHAAMUA KUJENGA ZAHANATI YAKE**

DIWANI wa Kata ya MUSANJA, Mhe Ernest Mwira amesema VIJIJI 3 vya Kata hiyo havina ZAHANATI hata moja na vyote vinahudumiwa na KITUO cha AFYA cha Kata jirani ya Murangi.

KIONGOZI huyo ameendelea kueleza kwamba baadhi ya WAGONJWA wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 10 kwenda kupata matibabu kwenye Kituo hicho cha Afya.

Kwa hiyo, Kijiji cha NYABAENGERE kimeamua kujenga ZAHANATI yake ambayo imepangwa ikamilike ndani ya mwaka mmoja.

MTENDAJI wa Kijiji (VEO) cha Nyabaengere, Ndugu Emmanuel Eswaga amesema utekelezaji wa MPANGOKAZI wa Mradi huo, unamtaka KILA MWANAKIJIJI mwenye uwezo wa kufanya kazi, ATACHANGIE Tsh 24,000, na kila KITONGOJI kitasomba mawe, mchanga na maji.

**MCHANGO WA DIWANI**
Diwani, Mhe Ernest Mwira ataanza kutoa MICHANGO yake kwa kuchangia SARUJI MIFUKO 20

**MCHANGO WA MBUNGE WA JIMBO**
Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, AMEKUBALI kuanza kuchangia ujenzi huo na ataanza kwa kuchangia SARUJI MIFUKO 100.

**OMBI KWA WAZALIWA WA KATA YA MUSANJA**

Zahanati inayoanza kujengwa Kijijini Nyabaengera itatoa HUDUMA za Afya kwa Vijiji jirani vya Mabui Merafuru na Musanja vyote vya Kata hiyo.

Kwa hiyo, WAZALIWA wa Kata ya MUSANJA wanaombwa wachangie MRADI huu kwa kutuma MICHANGO yao kwa DIWANI au VIONGOZI wengine wa Kata hiyo.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## ZAHANATI ZA MUSOMA VIJIJINI ZAPANULIWA KWA KUONGEZA WODI ZA MAMA & MTOTO

Posted on February 2, 2021



*BOMA la Jengo la Mama & Mtoto la Zahanati ya Kisiwani Rukuba, Musoma Vijijini.*

HALMASHAURI ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) yenye Jimbo la Musoma Vijijini (Kata 21, Vijiji 68) lina:

*Magari ya Wagonjwa (Ambulances) 5
*Zahanati 23 za Serikali zinazotoa huduma za Afya
*Zahanati 4 za Binafsi zinazotoa huduma za Afya
*Zahanati mpya 15 zinajengwa
*Vituo vya Afya 3 vinatoa huduma za Afya
*Hospitali ya Wilaya 1 – ujenzi unakamilishwa

WANAVIJIJI wa Jimbo la Musoma Vijijini wameamua kuboresha HUDUMA za AFYA zitolewazo kwenye ZAHANATI zao kwa kujenga WODI za Mama & Mtoto.

UJENZI wa MIUNDOMBINU hii mipya unachangiwa na:
*Serikali
*Wanavijiji
*Mbunge wa Jimbo
*Madiwani

*Wazaliwa wa Musoma Vijijini
*Wadau wengine wa Maendeleo

**UJENZI WA WODI ZA MAMA & MTOTO**
Baadhi ya ZAHANATI zilizojengwa zamani zimeanza kuboresha HUDUMA za AFYA wanazozitoa kwa kujenga WODI za Mama & Mtoto.

KISIWA cha RUKUBA ni Kijiji cha Kata ya Etaro. Kijiji hiki kimeamua kujenga WODI ya Mama & Mtoto inayotarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 1 Machi 2021.

Zahanati nyingine zilizoanza ujenzi wa Wodi za Mama & Mtoto ni Zahanati za Bukima na Nyegina.

JENGO la WODI ya Mama & Mtoto la Zahanati ya Kisiwani Rukuba lina VYUMBA 13. Michango ya ujenzi imetolewa na:

*WANAVIJIJI – nguvukazi
*FEDHA zinazorudishwa (20% ya Makusanyo ya ushuru) kutoka Halmashauri yetu
*MBUNGE wa JIMBO – ameanza kwa kuchangia SARUJI MIFUKO 200.

WADAU wa MAENDELEO wanaombwa kuanza kuchangia VIFAA vinavyohitajika kwenye WODI hiyo, vikiwemo, vitanda, magodoro, n.k.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## UJENZI WA WODI YA MAMA NA MTOTO KISIWANI RUKUBA

Posted on July 10, 2020



*Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto kwenye Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba – hatua hiyo ya ujenzi imefikiwa ndani ya muda wa wiki 2 (kasi kubwa)*

Jumamosi, tarehe 4.7.2020, Prof Sospeter Muhongo, alikamilisha AHADI yake ya KUCHANGIA SARUJI MIFUKO 200 (mia mbili) kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Mama & Mtoto kwenye Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba. Prof Muhongo alitoa AHADI hiyo kabla muda wake wa UBUNGE kufikia tamati.

**HALI YA HUDUMA YA AFYA MUSOMA VIJIJINI**

*Zahanati 23 za Serikali

*Zahanati 4 za Binafsi

*Zahanati 15 zinajengwa kwa nguvu za WANANCHI kwa kushirikiana na Serikali

*Wodi za Mama na Mtoto zinajengwa kwenye Zahanati za Bukima, Nyegina na Kisiwa cha Rukuba.

*Vituo vya Afya 2 (Murangi & Mugango)

*Kituo cha Afya Bugwema – Zahanati ya Kijiji cha Masinono inapanuliwa iwe Kituo cha Afya cha Kata ya Bugwema.

*Hospitali ya Wilaya inajengwa Kijijini Suguti, Kitongoji cha Kwikonero.

**MAGARI YA WAGONJWA (Ambulances):**
Mbunge wa Jimbo Prof. Sospeter Muhongo ametoa mchango mkubwa wa magari matano (5) ya wagonjwa ambayo yako kwenye Zahanati za Masinono, Kurugee na Nyakatende, na kwenye Vituo vya Afya vya Murangi na Mugango.

**KARIBUNI TUCHANGIE UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA AFYA MUSOMA VIJIJINI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI

**(30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)**

# VIKUNDI VYA KILIMO VYAENDELEA KUNEEMEKA KWA KILIMO CHA UMWAGILIAJI NA KWA KUTUMIA PLAU

Posted on April 22, 2021



*WANACHAMA wa Kikundi cha JIPE MOYO cha Kijijini Kome, Kata ya Bwasi, wakitayarisha SHAMBA lao la MIHOGO.*

KIKUNDI cha KILIMO cha JIPE MOYO cha Kijijini Kome, Kata ya Bwasi kinajishughulisha na KILIMO cha UMWAGILIAJI.

KATIBU wa Kikundi hiki, Ndugu Deborah Isaack, amesema kuwa KIKUNDI chao kina WANACHAMA 35 na kilianzishwa Mwaka 2015.

KIKUNDI hiki (JIPE MOYO) kinaundwa na WANAWAKE tu na wanajishughulisha na KILIMO kwa MPANGILIO ufuatao:
MAZAO YA UMWAGILIAJI (bustani): wanalima matikiti, nyanya, vitunguu na kabeji

MAZAO YA KUTEGEMEA MVUA: wanalima mahindi, mihogo, maharage na alizeti (majaribio)

**ZANA & MBEGU ZA KILIMO**
Kikundi cha JIPE MOYO kimepewa misaada na mikopo kutoka kwa : HALMASHAURI yetu (Musoma DC) imetoa MIKOPO kwa awamu mbili, yaani, SHILINGI MILIONI tano (5) na SHILINGI MILIONI saba (7).

**PCI (TANZANIA) imechangia:**
*MASHINE ya UMWAGILIAJI,
*MBEGU za mahindi na mihogo

**MBUNGE wa Jimbo lao, Prof Sospeter Muhongo amechangia:**
*Jembe la kukokotwa na ng'ombe (PLAU)
*MBEGU za mihogo, mtama na alizeti.

**MAFANIKIO YA KIKUNDI CHA JIPE MOYO**
MWANACHAMA, Ndugu Bilenjo Mangano, amesema tayari yeye AMEJENGA NYUMBA BORA na anasomesha vizuri WATOTO wake kutokana na MAPATO mazuri ya Kikundi chao.

Vilevile, MWANACHAMA huyo amesema wenzake wengine wamefanikiwa kufungua MADUKA kutokana na MAPATO mazuri ya Kikundi chao.

**SHULE YA MSINGI KOME YAPEWA CHAKULA**
Kikundi cha JIPE MOYO kimegawa sehemu ya MAVUNO yake ya hivi karibuni na kuipatia S/M Kome:
*MAHINDI Magunia 4
*MAHARAGE kilo 80

AFISA KILIMO wa Kata ya Bwasi, Ndugu Alex Mihambo, amekuwa akifuatilia kazi za KILIMO za Kikundi hiki na kuhakikisha kuwa SOKO la MAZAO yao linapatikana bila usumbufu.

AFISA Kilimo huyo amesema kwamba WANAVIJIJI wengine wamehamasika sana na KUANZISHA VIKUNDI vya KILIMO na kwa sasa kuna VIKUNDI vipya 15 Kijijini Kome.

**KIKUNDI CHA JIPE MOYO CHATAYARISHA MIRADI MIPYA**

Kwa siku za usoni, Kikundi hiki kimepanga kufanya yafuatayo:
*Kuongeza HISA za MFUKO wao wa FEDHA za kukopeshana
*Uoteshaji wa MITI ya msitu
*Ufugaji wa NYUKI kwa ajili ya biashara ya ASALI
*Kuanzisha KIWANDA kidogo cha kukamua MAFUTA ya ALIZETI.

DC, MBUNGE, MADIWANI na VONGOZI wengine wanawashawishi WANAVIJIJI wa Jimbo la Musoma Vijijini KUANZISHA VIKUNDI VYA UCHUMI, yaani, vya Kilimo cha Umwagiliaji, Uvuvi wa samaki, Ufugaji wa nyuki, n.k.

MWITIKIO wa uanzishwaji wa VIKUNDI vya UCHUMI ni mzuri na Mbunge wa Jimbo anaendelea kugawa bure MAJEMBE ya kukokotwa na ng'ombe (PLAU) kwenye VIKUNDI vya KILIMO.

Taratibu za VIKUNDI vya UVUVI kupewa MIKOPO ya RIBA NAFUU unaendelea kutayarishwa.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## VIKUNDI VYA WANAVIJIJI VYA KUKUZA UCHUMI VINAZIDI KUSHAMIRI MUSOMA VIJIJINI

Posted on December 23, 2020



*Baadhi ya Wanachama wa Kikundi cha TUMETAMBUA wakipalilia MIHOGO shambani mwao, Kijijini KASTAM, Kata ya Bukima.*

WANAVIJIJI ndani ya VIJIJI 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kuanzisha VIKUNDI vya kustawisha na kukuza UCHUMI wao. VIKUNDI hivyo ni vya KILIMO, UVUVI, UFUGAJI na VICOBA.

KIKUNDI cha TUMETAMBUA kilichopo Kijiji cha Kastam, Kata ya Bukima kilianzishwa Mwaka 2017 na kina Wanachama 29.

KIKUNDI hiki kinajishughulisha na KILIMO, uoteshaji wa MITI, na KUKOPESHANA fedha.

MWENYEKITI wa Kikundi hiki, Ndugu Nyamisi Daniel anasema wao wamejikita zaidi kwenye KILIMO cha mihogo, mahindi, maharage na viazi lishe. Kwa hiyo, WANACHAMA wote wanacho CHAKULA cha kutosha kwa familia zao, na wanapeleka 20% ya MAVUNO yao ya mazao ya chakula kwenye S/M Mkapa ya Kijijini mwao.

Vilevile, Kikundi hiki chenye MAFANIKIO makubwa kinatoa msaada wa VIFAA vya SHULE kwa Wanafunzi wanaosoma wakiwa kwenye mazingira magumu.

**MBEGU YA MIHOGO YA AINA YA MKOMBOZI YATOA MAVUNO MAZURI**

MZALISHAJI MBEGU za MIHOGO, Ndugu Festo Obed ambae pia ni Mwanachama wa Kikundi cha TUMETAMBUA amepata MAFUNZO ya kuzalisha mbegu bora za mihogo kutoka Shirika la MEDA ambalo kwa sasa linafanya kazi kwenye Kata za Bugoji, Bukima, Kiriba, Murangi, Nyamrandirira, Rusoli na Suguti.

Ndugu Obed anasema alipanda VIJITI 4,000 vya mbegu ya MKOMBOZI akafanikiwa kuvuna VIJITI 38,400 ndani ya Miezi 12. Kwa sasa, yeye amekuwa Mfanyabiashara wa MBEGU (Vijiti) ya mihogo ya aina ya MKOMBOZI ambapo kila KIJITI anauza Shilingi 30.

MTAALAMU wa MEDA, Ndugu Isaack Musa amesema lengo kuu la Shirika lao ni kuendeleza mbegu bora za mihogo zinazostahimili magonjwa.

Baada ya kupata MAFANIKIO kwa Mbegu ya MKOMBOZI, MEDA imeanzisha MASHAMBA DARASA ya mbegu nyingine za mihogo za aina ya MKUMBA, MKURANGA 1, T130, ORERA, KIROBA, EYOPE na F-10-30R katika Kata za Ifulifu, Mugango, Nyambono na Rusoli.

KIKUNDI cha TUMETAMBUA kinakusudia kupanua MASHAMBA yake ya MIHOGO ili wapate MAVUNO ya ziada ya biashara.

Aidha, mbali na MAFANIKIO hayo KIKUNDI hiki kinatarajia kuanzisha Mradi wa MASHINE ya KUSAGA, kununua CHAREHANI za kushona nguo, na kununua VIFAA vya USEREMALA.

WANACHAMA wa Kikundi cha TUMETAMBUA wanatoa SHUKRANI kwa WADAU wa MAFANIKIO yao ambao ni:

*PCI Tanzania kwa kuwapatia mbegu za mahindi, maharage, alizeti na magunia ya kuhifadhia chakula.

*Jamii Impact kwa kuwapatia MKOPO wa Shilingi Milioni 5 (awamu ya kwanza), na awamu ya pili walikopeshwa Shilingi Milioni 8.

*SHIMAKIUMU kwa kuwapatia mbegu za mahindi, dawa za mimea na viroba vya kupandia miche.

*MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo kuwapatia mbegu za mihogo, mtama na alizeti.

Prof Muhongo aligawa bure Jimboni mwao MAGUNIA 796 ya MBEGU (Vijiti) ya mihogo aina ya MKOMBOZI kama ifuatavyo:
Mwaka 2016/2017: Magunia 446
Mwaka 2017 /2018: Magunia 350

MFUKO wa JIMBO kwa kuwapatia mashine na mipira ya umwagiliaji, na mbegu za bustani za mbogamboga.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## PROGRAMU YA WAKULIMA KUPUNGUZA MATUMIZI YA JEMBE LA MKONO INAENDELEA MUSOMA VIJIJINI

Posted on November 29, 2020



*Kikundi cha Wakulima wa Kijiji cha Buanga, Kata ya Rusoli, kiitwacho "NGUVUKAZI" kikiwa katika shamba lao walilolima kwa kutumia PLAU waliyopewa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini.*

MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo anaendelea KUGAWA bure PLAU (majembe ya kukokotwa na ng'ombe au punda) kwa VIKUNDI vya WAKULIMA wa Jimbo la Musoma Vijijini. MGAO mwingine utakuwa wa ZAWADI ya KRISMASI & MWAKA MPYA utafanyika tarehe 24 Disemba 2020.

Kikundi kiitwacho, "NGUVUKAZI", cha Kijiji cha Buanga, Kata ya Rusoli ni moja ya VIKUNDI vilivyokwishapewa PLAU na MBEGU kutoka kwa Mbunge huyo.

Kikundi cha NGUVUKAZI kilianzishwa Mwaka 2015 na kina WANACHAMA 30 wanaolima MAZAO ya CHAKULA na BIASHARA. Kikundi hiki kinagawia SHULE za MSINGI Bwenda A & B 50% ya MAVUNO ya Mazao yake ya CHAKULA.

MWENYEKITI wa Kikundi hicho, Ndugu Tore Masamaki anasema MISAADA ya NYEZO zao za Kilimo imetolewa na PCI (Tanzania) na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo.

PCI (Tanzania) imewapatiwa MASHINE ya UMWAGILIAJI, MBEGU za viazi lishe, mahindi na alizeti.

Mbunge Prof Muhongo amewapatia PLAU 1 na MBEGU za mihogo, mtama, ufuta na alizeti

Vilevile, kwa Kata ya Rusoli, Mbunge huyo aligawa PLAU 1 kwa Kikundi kingine kiitwacho “MKULIMA JEMBE”.

Ndugu Anna Masange, MWANAKIKUNDI cha NGUVUKAZI amesema kwamba ameweza kujenga NYUMBA, ANASOMESHA WATOTO wake na kufungua BIASHARA ya DUKA dogo kutokana na MAPATO ya Kilimo cha Kikundi chao. Kwa hiyo, anawashawishi WANAWAKE na VIJANA wajiunge kwenye VIKUNDI vya KILIMO vina manufaa sana.

AFISA KILIMO wa Kata ya Rusoli, Ndugu Gervas Ngova amesema WANAVIJIJI wa Kata hiyo wamechangamkia fursa za kuanzisha VIKUNDI vya KILIMO kwani vinawarahisishia kupata MAFUNZO na MISAADA ya Kilimo kutoka kwa WADAU wa MAENDELEO ikiwemo SERIKALI yetu.

Vilevile, hapo shambani (picha ukurasa wa 112) Afisa Kilimo wa Kata hiyo anatoa MAELEKEZO ya Kilimo bora kwa Kikundi cha “NGUVUKAZI”.

**KILIMO NI UHAI**
**KILIMO NI AJIRA**
**KILIMO NI UCHUMI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# PLAU NYINGINE 50 KUGAWIWA KWA VIKUNDI VINGINE 50 VYA WAKULIMA WA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on July 16, 2020



*Wakulima wakitumia PLAU walizopewa bure na Prof Sospeter Muhongo*

Jumatatu, tarehe 13 Julai 2020, Prof Sospeter Muhongo alinunua PLAU 50 (majembe ya kukokotwa na ng'ombe) kwa ajili ya kuzigawa siku ya Sherehe za WAKULIMA (8.8.2020, NANE NANE).

Prof Muhongo amefanya hivyo kwa kuzingatia TARATIBU za UCHAGUZI ambapo tarehe 13 Julai 2020 ndiyo siku ya mwisho ya kutekeleza AHADI za waliokuwa WABUNGE wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. PLAU hizo zitagawiwa tarehe 8.8.2020 (NANE NANE) na Mkuu wa Wilaya (DC) ya Musoma.

**PROGRAMU YA KUPUNGUZA MATUMIZI MAKUBWA YA JEMBE LA MKONO**

Prof Muhongo AMEANZISHA PROGRAMU hiyo ikiwa ni sehemu ya LENGO kuu la KUBORESHA KILIMO ndani ya VIJIJI 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini.

JUMLA YA PLAU 85 zimeishagawiwa kwa VIKUNDI 85 vya WAKULIMA wa Jimbo la Musoma Vijijini. LENGO KUU ni kuwa na angalau PLAU 20 kwa kila Kijiji.

WAKULIMA wameelezwa mara kadhaa namna ya kupata MIKOPO ya KUNUNUA MATREKITA. Ofisi ya Kilimo ya HALMASHAURI yetu (Musoma DC) ipo tayari kuwasaidia kutuma MAOMBI ya MIKOPO yao.

MBEGU BORA zimeishagawiwa kwa WAKULIMA wa Jimbo la Musoma Vijijini. Hizo ni: Mbegu za ALIZETI (tani 20), MIHOGO, MTAMA na UFUTA.

**KARIBUNI TUCHANGIE UBORESHAJI wa KILIMO ndani ya VIJIJI 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# EQUITY BANK YAINGIA MUSOMA VIJIJINI: WAVUVI WAJIUNGA KWENYE VIKUNDI KUOMBA MIKOPO

Posted on December 18, 2020



*UHAMASISHAJI wa uundwaji wa VIKUNDI vya UVUVI ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.*

WAVUVI walioko katika Mialo minne ya Busekera (Kata ya Bukumi), Bwai Kumusoma (Kata ya Kiriba) na Visiwa vya Iriga na Rukuba (Kata ya Etaro) wamepokea ELIMU ya kujiunga kwenye VIKUNDI vya UVUVI ili kutekeleza shughuli zao za UVUVI kwa UFANISI mkubwa zaidi, na uwezekano wa kupata MITAJI kupitia MIKOPO mbalimbali.

VIONGOZI WA HALMASHAURI YA WILAYA ya MUSOMA waliwatembelea WAVUVI wa Kata hizo 3 na kufanya uhamasishaji huo kwa muda wa siku mbili mfululizo.

AFISA UVUVI wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Ndugu Augustine Constatine alisisita suala la UVUVI BORA unaozingatia SHERIA na KANUNI zake.

AFISA MAENDELEO ya JAMII wa Halmashauri hiyo, Ndugu Tanna Nyabange na Msaidizi wake Ndugu Nyanjara Majura walielezea umuhimu wa uundwaji wa VIKUNDI vya UVUVI kwa ajili ya kupata na MIKOPO kutoka kwenye HALMASHAURI yao na kutoka kwenye TAASISI za FEDHA, zikiwemo BENKI mbalimbali. Suala la upatikanaji wa SOKO ya UHAKIKA kupitia Vikundi vya Uvuvi lilisisitizwa.

WASAIDIZI 3 wa MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu Fedson Masawa, Ndugu Verediana Mgoma na Ndugu Hamisa Gamba WALISHIRIAKANA na VIONGOZI wa Halmashauri hiyo kuorodhesha VIKUNDI vya UVUVI vyenye nia ya kuomba MIKOPO kutoka Equity Bank.

**EQUITY BANK NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI**

BANK hiyo imewakilishwa na Ndugu Bahati Dollo, Kemilembe Kabigumila na Peter Chuchu, kwenye ZIARA ya KIKAZI ya siku 2 na kuongea na VIKUNDI vya UVUVI vya Kata hizo tatu.

**IDADI YA VIKUNDI**

Vilivyojitokeza kuomba MIKOPO kutoka Bank hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) Kata Bukumi (Vijiji 4)
  *Vikundi 17, Wanachama 203
(ii) Kata ya Kiriba (Vijiji 3)
  *Vikundi 25, Wanachama 327
(iii) Kata ya Etaro (Vijiji 3)
  *Kisiwa cha Rukuba Vikundi 31, Wanachama 425
  *Kisiwa cha Iriga Vikundi 6, Wanachama 80

EQUITY BANK itaanza na VIKUNDI vya UVUVI 79, vyenye WANACHAMA 1,035

LEO, Jumatano, 16.12.2020, MAAFISA 3 wa EQUITY BANK wameonana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vicent Naano Anney, na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo KUJADILI FURSA hiyo ya upatikanaji wa MIKOPO ya

EQUITY BANK kwa VIKUNDI vya UVUVI vya Jimbo la Musoma Vijijini.

EQUITY BANK iko tayari kutoa MIKOPO kwa VIKUNDI vya UVUVI vya Jimbo la Musoma Vijijini – matayarisho yanaendelea.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KAMPENI YA UHIMILISHAJI (ARTIFICIAL INSEMINATION) YAZINDULIWA MUSOMA VIJIJINI

Posted on November 21, 2020



*Matukio mbalimbali ya UZINDUZI wa UHIMILISHAJI wa ng'ombe wa kienyeji uliofanyika Kijijini Bugwema tarehe 18.11.2020.*

KATIBU MKUU wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Idara ya MIFUGO, Prof Elisante Ole Gabliel amezindua Kampeni ya UHIMILISHAJI wa NG'OMBE (Artificial Insemination) kwa WAFUGAJI wa Musoma Vijijini.

Tukio hilo lililofanyika Kijijini Bugwema, lilihudhuriwa na WAFUGAJI na VIONGOZI mbalimbali wakiwemo Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney, Madiwani Wateule na Wasaidizi wa Mbunge. WANANCHI wasio Wafugaji nao walihudhuria uzinduzi huo.

Prof Elisante ole Gabriel alieleza kwamba LENGO KUU la UHIMILISHAJI ni UPANDIKIZAJI wa MIMBA kwenye NG'OMBE (wakiwemo wa kienyeji) kwa kuweka MBEGU ya NG'OMBE wa KISASA kwa njia ya MRIJA ili kuongeza UBORA na WINGI wa MIFUGO (ng'ombe) hiyo.

KATIBU MKUU huyo alisisitiza kuwa MIFUGO ni UTAJIRI, na kwamba WAFUGAJI wanapaswa kuwa tayari kutoa USHIRIKIANO mkubwa kwa WIZARA ili kuanzisha Miradi ya UFUGAJI wa

KISASA wenye NG’OMBE BORA (maziwa mengi, nyama laini, ngozi nzuri, n.k.).

WAFUGAJI wa Kata ya Bugwema, kwa niaba ya Wafugaji wa Musoma Vijijini, wameishukuru sana SERIKALI kwa kuwasogezea huduma hiyo ya UHIMILISHAJI na wameahidi kutoa USHIRIKIANO mkubwa wa kuboresha UFUGAJI wao kwa njia hii ya UHIMILISHAJI wa ng’ombe wa kienyeji.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UFUGAJI WA NYUKI WAANZA KUCHANGAMKIWA MUSOMA VIJIJINI

Posted on December 18, 2020



*KIKUNDI cha JIPE MOYO cha Kijijini Buanga, Kata ya Rusoli kikiwa kwenye SHAMBA lao lenye MIZINGA ya NYUKI.*

KIKUNDI cha JIPE MOYO cha Kijiji cha Buanga, Kata ya Rusoli kimeanzisha MRADI wa UFUGAJI NYUKI kwa ajili ya kupanua wigo wa shughuli za ki-uchumi za KIKUNDI hicho.

Kikundi hicho kimepata UTAALAMU wa UFUGAJI wa NYUKI kutoka kwenye MAFUNZO waliyopewa na SHIRIKA la SWISSCONTACT.

MWENYEKITI wa Kikundi cha JIPE MOYO, Ndugu Masamaki Girishom, amesema kwamba Kikundi chao kilianzishwa Mwaka 2018 na kina Wanachama 24. Kikundi hiki linashughulisha na KILIMO, na sasa kimeanza KUFUGA NYUKI.

Shirika la SWISSCONTACT limewapatia VIFAA vya awali vya Mradi huu ambavyo ni MIZINGA 10 na VAZI 1 la kuvunia ASALI.

MRATIBU wa Swiss Contact, Ndugu Nelson Bento amesema kwamba hadi sasa, JIMBONI mwetu, kuna VIKUNDI 7 vya UFUGAJI wa NYUKI, na WANAVIJIJI wengi wanaanza kupenda kufuga nyuki kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya mapato yao.

MRATIBU huyo amesema SOKO la ASALI itakayovunwa Vijijini mwetu lipo.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo anaendelea kuhimiza WANAVIJIJI waanzishe VIKUNDI vya UCHUMI, vikiwemo vya kilimo cha umwagiliaji, uvuvi na ufugaji wa nyuki.

**KARIBUNI TUFUGE NYUKI VIJIJINI MWETU**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI

**(30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)**

# MAJI SAFI NA SALAMA YA BOMBA NA SHEREHE ZA PASAKA NDANI YA VIJIJI VITATU

Posted on April 8, 2021



*WANANCHI wa Vijiji vya Busungu (Kata ya Bulinga) na Kwikerege (Kata ya Rusoli) wakiteka MAJI ya BOMBA kutoka Ziwa Victoria.*

WANANCHI wa Vijiji vya Busungu (Kata ya Bulinga), Bukima (Kata ya Bukima) na Kwikerege (Kata ya Rusoli) WAMEFURAHI sana kuanza kupata MAJI ya BOMBA ya Ziwa Victoria.

WANANCHI hao, hasa akina MAMA na WATOTO wamefurahishwa sana na upatikanaji wa maji katika maeneo yao, kwani hapo awali walilazimika kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi kutafuta maji kutoka kwenye visima vya asili.

Mama Nyamburi Mafuru, Mkazi wa Kijiji cha Busungu amesema kuwa amefurahishwa sana na neema ya upatikanaji wa maji kijijini mwao maana walitumia muda mwingi kutafuta maji na kupelekea shughuli za kujitafutia kipato kuzorota.

Mama huyo amesema, “Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kutuondolea kero hii hasa sisi wanawake.”

MKANDARASI wa Mradi huu, EDM NETWORK LTD, Ndugu Adiel Mushi amethibitisha kukamilika kwa mradi huo kwa zaidi ya 90% na VITUO 23 vimeanza kutumika ambavyo ni:
*Vioski 2
*Maltwater 1
*Vituo 2 vya kunyweshea mifugo
*Vituo 18 vya kuchotea maji.

Mkandarasi huyo ameeleza kwamba TANKI la BUSUNGU lina uwezo wa kujaza LITA 225,000 za kuhudumia Vijiji 3 hivyo.

DIWANI wa Kata ya Bulinga, Mhe Abel Mafuru amewataka WANANCHI kutunza vizuri MIUNDOMBINU ya usambazaji wa maji ya bomba kwenye Vijiji vyao.

DIWANI huyo ametoa SHUKRANI nyingi sana kwa SERIKALI yetu kwa kuwapatia MAJI SAFI na SALAMA ya BOMBA, na vilevile amemshukuru Mbunge wao, Prof Sospeter Muhongo kwa UFUATILIAJI mzuri wa Miradi ya Maji na Miradi mingine ndani ya Jimbo lao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijni.or.tz

# MUSOMA VIJIJINI – RUWASA YAONGEZA KASI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA USAMBAZAJI MAJI YA ZIWA VICTORIA

Posted on February 2, 2021



*Jumamosi, 30.1.2021 RUWASA (W) ilifanya majaribio ya MRADI wa MAJI wa BULINGA-BUJAGA kwenye KITUO cha SWEDI*

INJINIA Saidi Nyamlinga, Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Musoma amesema kwamba kwenye Mradi huu wamejenga MATENKI 2:

(i) Tenki la Kijijini BULINGA lina uwezo wa kujaza LITA 150,000. VITUO 14 vimejengwa na leo (30.1.2021) majaribio yamefanywa kwenye KITUO cha Swedi – PICHA ya hapo juu inaonesha WANAVIJIJI wakiteka MAJI kutoka Kituo cha Swedi. Hili ni BOMBA la MAJI la Bujaga-Bulinga ndani ya Kata ya Bulinga

(ii) Tenki la Kijijini BUSUNGU lina uwezo wa kujaza LITA 225,000. Ujenzi wa VITUO 15 vya Vijiji 3 vya Busungu, Bukima na Kwikerege unakamilishwa na majaribio yatafanywa ndani ya wiki 2 zijazo. Hili ni BOMBA la MAJI la Busungu-Bukima-Kwikerege ndani ya Kata za Bulinga, Bukima na Rusoli.

MAJARIBIO yakikamilika, WANAVIJIJI watakaribishwa kutuma MAOMBI ya kufungiwa maji majumbani mwao au kwenye maeneo ya biashara zao.

**HONGERENI SANA RUWASA**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## MIRADI MINGINE YA RUWASA – KATA ZA SUGUTI NA NYAMBONO ZAKARIBIA KUANZA KUTUMIA MAJI YA ZIWA VICTORIA

Posted on December 14, 2020



*MIUNDOMBINU inajengwa kwa ajili ya usambazaji wa MAJI SAFI na SALAMA (maji ya bomba) kwenye KATA za SUGUTI na NYAMBONO.*

Kata ya SUGUTI ina Vijiji 2 (Suguti na Kusenyi) vyenye ufukwe wa ZIWA VICTORIA, na vingine viwili (Wanyere na Chirorwe) viko mbali na Ziwa hilo.

Kata ya NYAMBONO, yenye Vijiji 2, yaani Nyambono na Saragana iko umbali wa zaidi ya kilomita 10 kutoka Ziwa Victoria.

SERIKALI imetoa Shilingi MILIONI 356 kwa Mradi wa MAJI wa Kata ya Suguti na Shilingi MILIONI 230 kwa Mradi wa MAJI wa Kata ya Nyambono – hii ni MIRADI mingine ya RUWASA inaotekelezwa ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa Mwaka huu wa Fedha (2020/2021).

MIUNDOMBINU inajengwa kuvuta na kusambaza MAJI kutoka ZIWA VICTORIA (Kijijini Suguti) ambapo PAMPU yenye uwezo wa kusukuma LITA 67,000 kwa saa itajengwa. VIFAA vyote vimeishanunuliwa.

MAJI ya kutoka Kijijini Suguti yatasambazwa kwenye Vijiji vya Kusenyi, Chirorwe na Wanyere (Kata ya Suguti).

TENKI la ujazo wa LITA 200,000 linajengwa Kijijini Chirorwe ambapo MAJI ya Kata ya Nyambono yatachukulia kupitia Mlima Nyabherango.

TENKI jingine la ujazo wa LITA 200,000 linajengwa Mlimani Nyabherango kwa ajili ya MAJI ya Vijiji vya Nyambono na Saragana.

Kwa hiyo, RUWASA kwa sasa inakamilisha ujenzi wa MIUNDOMBINU ya kusambaza MAJI SAFI na SALAMA kwenye Kata za SUGUTI na NYAMBONO. Hapo baadae, Kata ya BUGOJI yenye Vijiji 3 (Bugoji, Kaburabura na Kanderema) nayo itafikishiwa MAJI kutoka kwenye TENKI la Mlimani Nyabherango.

MENEJA wa MRADI huu wa RUWASA, Injinia Mohamed Said Yamlinga amesema kuwa MIRADI ya Kata za Suguti na Nyambono itakamilika Januari 2021.

WANAVIJIJI wa Kata za SUGUTI na NYAMBONO, na VIONGOZI wao, wanaishukuru sana SERIKALI yetu kwa kutoa FEDHA za kutekeleza MIRADI ya kusambaza MAJI ya BOMBA Vijijini mwao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## RUWASA YAANZA KUTEKELEZA KWA KASI KUBWA MRADI WA USAMBAZAJI MAJI KWENYE KATA YA NYAKATENDE

Posted on December 12, 2020



*UTEKELEZAJI wa MRADI wa RUWASA wa kusambaza MAJI ya ZIWA VICTORIA kwenye Kata ya Nyakatende.*

RUWASA imeanza kujenga MIUNDOMBINU ya USAMBAZAJI wa MAJI ya ZIWA VICTORIA kwa Kata ya NYAKATENDE.

Kata ya NYAKATENDE ina Vijiji 4 ambavyo ni Kakisheri, Kamguruki, Kigera na Nyakatende. Vijiji 2 (Kigera na Kakisheri) viko kwenye mwambao wa ZIWA VICTORIA na ndivyo vitaanza kusambaziwa MAJI ya Mradi huu, baadae Vijiji vya Kamguruki na Nyakatende vitafuata.

MITAMBO ya kuvuta na kusafisha MAJI ya ZIWA inajengwa kwenye Kitongoji cha Kusenyi, Kijijini Kigera.

Sehemu ya Kijiji cha KURUKEREGE cha Kata jirani ya NYEGINA itapata MAJI ya Mradi huu, na sehemu nyingine ya Kijiji hicho itapewa MAJI ya MRADI wa MUWASA.

MENEJA wa MRADI huu wa RUWASA, Injinia Mohamed Said Yamlinga amesema MIUNDOMBINU inayojengwa kwa sasa ni:
*TENKI la MAJI lenye ujazo wa LITA 300,000 (laki tatu)
*OFISI ya Mradi
*VIOSKI vya kuuzia maji
*Kutandaza MABOMBA kwenye mitaro inayochimbwa.

MENEJA huyo amesema kuwa MRADI huu utakamilika Januari 2021.

WANANCHI na VIONGOZI wao wa Kata ya Nyakatende WANAISHUKURU sana SERIKALI yao kwa kutekeleza AHADI yake ya usambazaji wa MAJI SAFI na SALAMA vijijini mwao.

Kata za jirani za ETARO, NYEGINA na IFULIFU zitapewa MAJI ya kutoka kwenye Mitambo ya MUWASA iliyoko Bukanga, Musoma Mjini. MRADI umeanza kutekelezwa.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI
# YA
# UJENZI WA BARABARA

## (30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)

**Tarehe 30 Juni 2021:**

Ujenzi wa barabara ya lami ya Musoma – Makojo Busekera (km 92) umeanza

# KASI IONGEZEKE KWENYE UJENZI WA BARABARA YA LAMI YA MUSOMA-MAKOJO-BUSEKERA

Posted on March 2, 2021



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini akiwa na WATAALAMU wa TANROADS na MKANDARASI Kijijini Kusenyi kwenye ukaguzi wa barabara ya Musoma-Makojo-Busekera inayojengwa kwa kiwango cha LAMI.*

Jumatatu, tarehe 1.3.2021, MBUNGE wa JIMBO la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alikagua ujenzi wa BARABARA KUU ya Jimbo hilo inayojengwa kwa kiwango cha LAMI – barabara ya KILOMITA 92 ya Musoma-Makojo-Busekera.

Mbunge huyo alifuatana na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mara, Injinia Felix Ngaile na MKANDARASI wa Mradi, Injinia Getanyeri Nyantori.

Wataalamu wengine wa TANROADS walikuwepo na VIONGOZI wa Kijiji cha KUSENYI nao walikuwepo.

## USHAURI ULIOTOLEWA

(1) Kasi ya ujenzi iongezeke na AGIZO la RAIS Mhe Dkt John Joseph Pombe Magufuli LITEKELEZWE, yaani ujenzi wa awali wa KILOMITA 40.

(2) Kazi kubwa ya awali kwenye kipande cha Kusenyi-Kwikonero imefanyika, yaani kunyanyua tuta na kudhibiti udongo mweusi uliochukua sehemu kubwa ya kipande hiki ambacho ni mkondo wa maji yaingiayo Ziwa Victoria.

Vilevile, ujenzi wa madaraja kwenye maeneo korofi umekaribia kukamilika, kwa hiyo kasi ya ujenzi wa barabara hii MUHIMU SANA kwa UCHUMI wa Jimbo letu na kwa Taifa letu kwa ujumla (madini, samaki, pamba, mihogo, maziwa, n.k.) iongezeke.

(3) Fedha za Mradi zitolewe kwa wakati baada ya maombi yote kutimiza masharti yaliyowekwa.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KAMPENI ZA UCHAGUZI
# &
# UELIMISHAJI
# WA
# VIPAUMBELE
# VYA
# JIMBO LETU

**(30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)**

## KAMPENI ZA CCM – PROF MUHONGO ARUDI VIJIJINI KUSISITIZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA CHAGUO LAO

Posted on October 26, 2020



*Jumamosi, 24.10.2020, MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO amerudi kwenye Kata ya MAKOJO na kupiga KAMPENI kwenye Vijiji vya CHITARE na CHIMATI.*

### UTEKELEZAJI WA ILANI MPYA YA CCM (2020-2025) NDANI YA KATA YA MAKOJO

**(1) MAJI VIJIJINI**

Miradi wa MAJI kutoka ZIWA VICTORIA unatekelezwa ndani ya Kata hii – kukamilisha Mradi wa Bomba la Maji la Chitare-Makojo na baadae kusambaza Maji ya Bomba hili hadi Kijiji cha Chimati

**(2) UMEME VIJIJINI**

Vijiji vyote 3 vya Kata hii (Chimati, Chitare & Makojo) vinayo MIUNDOMBINU ya usambazaji wa UMEME, na baadhi ya Vitongoji vyake tayari vimepewa UMEME wa REA. Vitongoji vilivyosalia vitapewa UMEME, kama ilivyoelezwa ndani ya ILANI ya UCHAGUZI ya CCM (2020-2025)

**VIPAUMBELE VYA KILA KIJIJI**

**(1) KIJIJI CHA CHIMATI**

*Kukamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao
*Kujenga SEKONDARI ya Kijiji chao kwani SEKONDARI ya Kata iko mbali Kijijini Makojo.

**(2) KIJIJI CHA CHITARE**

*Kujenga SEKONDARI ya Kijiji chao kwani SEKONDARI ya Kata iko mbali Kijijini Makojo
*WODI ya MAMA & MTOTO kujengwa kwenye ZAHANATI yao

**(3) KIJIJI CHA MAKOJO**

*Kujenga ZAHANATI ya Kijiji chao

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

KATA YA MAKOJO imeahidi KUTOA KURA ZOTE kwa CCM – sababu – ILANI ya UCHAGUZI ya CCM (2020-2025) ina VIPAUMBELE vya MIRADI ya MAENDELEO yao

**"TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA"**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# WANAVIJIJI WA KATA YA NYEGINA WAAINISHA VIPAUMBELE VYAO VYA UTEKELEZAJI WA ILANI MPYA YA CCM

Posted on October 17, 2020



*MIKUTANO ya KAMPENI za CCM ndani ya Kata ya Nyegina.*

Alhamisi, 15.10.2020, MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO, amefanya MIKUTANO 3 ya KAMPENI za CCM ndani ya Kata ya Nyegina.

MIKUTANO 3 imefanywa kwenye VIJIJI vya Kurukerege, Nyegina na Mkirira.

WANAVIJIJI wa Kata hii wamesema KURA ZOTE watazipeleka CCM kwenye nafasi ya URAIS, UBUNGE na UDIWANI.

WANAVIJIJI wameamua hivyo baada ya kuvutiwa na ILANI MPYA ya CCM ya 2020-2025 na VIPAUMBELE vyao vya MAENDELEO vimo ndani ya ILANI hii.

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

**VIPAUMBELE VYA KIJIJI CHA KURUKEREGE**
*Kukamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao

*Kukamilisha ujenzi wa Vyumba Vipya vya Madarasa vya SHULE ya MSINGI BUKWAYA ambayo ni mpya yenye Madarasa 5.

**VIPAUMBELE VYA KIJIJI CHA NYEGINA**

*Kukamilisha WODI ya Mama & Mtoto inayojengwa kwenye ZAHANATI ya Nyegina.

**VIPAUMBELE VYA KIJIJI CHA MKIRIRA**

*Kukamilisha ZAHANATI ya Kijiji chao

**VIPAUMBELE VYA KATA (Vijiji vyote 3)**

*ELIMU: Kukamilisha ujenzi wa SEKONDARI ya PILI (Bukwaya Secondary School) itakayofunguliwa Januari 2021. Inajengwa Kijijini Nyegina

*MAJI VIJIJINI: Kata iko kwenye MIRADI 2 ya MAJI kutoka Ziwa Victoria –

**(i) MAJI YA MUWASA**

Maji ya Mji wa Musoma YAMEANZA kusambazwa kwenye VIJIJI jirani na Mji huo vikiwemo VIJIJI vyote vya Kata za Etaro, Nyegina, Nyakatende na Ifulifu.

**(ii) MRADI WA MAZIWA MAKUU**

*Vijiji vyote 3 vya Kata hii ni miongoni mwa VIJIJI 33 vya Jimboni mwetu vilivyoko kwenye Mradi huu.

*UMEME VIJIJINI: Baadhi ya Vitongoji vya Vijiji vyote 3 vimeishapatiwa umeme na USAMBAZAJI unaendelea hadi kukamilisha upelekaji wa UMEME kwenye Vitongoji vyote.

**UTAMADUNI, MICHEZO NA SANAA**

*ILANI mpya ya CCM ya 2020-2025 inaeleza umuhimu wa Utamaduni, Michezo na Sanaa kwa TAIFA letu

*Jimbo letu LINAENDELEA kustawisha ukuaji na uimarikaji wa KWAYA na NGOMA zetu za ASILI.

MICHANGO ya PROF MUHONGO kwenye MIRADI yote ya MAENDELEO ya Kata hii inatambuliwa na kutolewa shukrani nyingi.

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# MIRADI YA MAENDELEO YAING'ARISHA CCM NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on October 17, 2020



*Wana Musoma Vijijini wakisikiliza kwa makini kwenye mkutano mmojawapo wa Kampeni.*

MALENGO ya KAMPENI za CCM ndani ya Vijiji 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini ni MAENDELEO (kwa ujumla wake) & USTAWI wa JAMII. Hivyo, USHINDI wa kishindo kizito.

WANANCHI wa kila KIJIJI na kila KATA, kwa kutumia ILANI ya UCHAGUZI ya CCM (2020-2025), wanabainisha VIPAUMBELE vyake vya MIRADI ya MAENDELEO.

**KATA YA BUSAMBARA**

Kata hii ina VIJIJI 3 (Kwikuba, Maneke na Mwiringo) na VIPAUMBELE vyake ni:

**(1) ELIMU & MAFUNZO**

Kata ya Busambara inayo SEKONDARI MPYA (Busambara Secondary School) iliyofunguliwa Januari 2020.

Ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa, Maabara, Maktaba, Nyumba za Walimu, n.k. unaendelea.

MICHANGO ya ujenzi wa SEKONDARI hii inatolewa na WANANCHI, SERIKALI, PROF MUHONGO na WAZALIWA wa Kata hii.

**(2) MAJI VIJIJINI**
MIRADI 2 ya MAJI ya kutoka Ziwa Victoria itatekelezwa ndani ya Kata hii:

(i) Vijiji vyote vitatu vimo ndani ya Mradi wa Maziwa Makuu
(ii) Vijiji vyote vitatu vimo ndani ya Mradi wa Mugango-Kiabakari-Butiama.

**(3) UMEME VIJIJINI**
Vijiji vyote vitatu vinayo miundombinu ya umeme na baadhi ya Vitongoji vimeishapatiwa umeme. Vitongoji vilivyosalia navyo vitapewa umeme kama inavyoelezwa ndani ya ILANI ya CCM ya 2020-2025

**KIJIJI CHA MWIRINGO**
* Kukamilisha ujenzi wa SHULE SHIKIZI iliyoko Kitongoji cha Ziwa. Shule itapanuliwa hadi kufikia Darasa la VII (Shule ya Msingi kamili).

**KIJIJI CHA KWIKUBA**
*Nyumba za Wafanyakazi wa ZAHANATI yao.

**KIJIJI CHA MANEKE**
*Kukamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao

UTEKELEZAJI wa MIRADI hiyo hapo juu unaanza tarehe 1.11.2020
WANANCHI wa Kata ya BUSAMBARA wanasema KURA ZOTE watapewa WAGOMBEA WATATU wa CCM (Urais, Ubunge na Udiwani)

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

## KAMPENI ZA CCM NI ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO: KATA YA NYAKATENDE INAYO MIRADI 5 YA KIPAUMBELE

Posted on October 14, 2020



*Jumatatu, 12.10.2020 MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO amefanya KAMPENI 3 na kukamilisha UOMBAJI wa KURA kwenye VIJIJI vyote 4 vya Kata ya Nyakatende (Kakisheri, Kamguruki, Kigera na Nyakatende).*

MIRADI yote ya KIPAUMBELE ya Kata ya Nyakatende CHIMBUKO LAKE ni ILANI za CCM za 2015-2020 na 2020-2025

**(1) MAJI VIJIJINI**

*Vijiji vyote 4 vya Kata hii vitapata MAJI kutoka Ziwa Victoria. Ipo MIRADI 3 ya Ziwa Victoria na unaotekelezwa SASA HIVI ni wa MAJI kutoka MUWASA (Maji ya Mji wa Musoma). SERIKALI ya CCM inatekeleza AHADI yake ya kusambaza MAJI VIJIJINI.

**(2) UMEME VIJIJINI**

*Vijiji vyote 4 vinayo Miundombinu ya kuendelea na usambazaji wa UMEME VIJIJINI kwenye Vitongoji vilivyosalia.

**MIRADI INAYOHITAJI MICHANGO YA WANANCHI & KUTOKA SERIKALINI**

**(3) ELIMU & MAFUNZO**

*SEKONDARI ya PILI (Kigera Secondary School) inajengwa na Vijiji 2 itafunguliwa JANUARI 2021. MICHANGO inatoka kwa Wanavijiji, Wazaliwa wa Vijiji 2 (Kakisheri & Kigera) na Prof Muhongo.

*SHULE SHIKIZI KIUNDA inajengwa Kijijini Kamguruki kwa kutumia MICHANGO ya Wananchi na ya Prof Muhongo

**(4) HUDUMA ZA AFYA**

*ZAHANATI mpya ya Kijiji cha Kakisheri tayari imeanza kujengwa

*ZAHANATI mpya ya Kijiji cha Kamguruki itaanza kujengwa baada ya tarehe 28.10.2020

*KITUO cha AFYA cha Kata ya Nyakatende kitajengwa Kijijini Kigera.

KAMPEZI za CCM ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ni KAMPENI za UTEKELEZAJI wa ILANI MPYA ya CCM ya 2020-2025

WAPIGA KURA WA KATA YA NYAKATENDE wanasema:
*Dkt Magufuli: 100%
*Prof Muhongo: 100%
*Ndugu Kishe: 100%

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# KISIWA CHA RUKUBA CHAIKUBALI ILANI MPYA YA CCM NA KUAMUA KUJENGA KITUO CHA AFYA

Posted on October 12, 2020



*Kisiwa cha RUKUBA kiko ndani ya Kata ya ETARO yenye VIJIJI 4 (Busamba, Etaro, Mmahare na Rukuba).*

Jumapili, tarehe 11.10.2020 MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO, alifanya MIKUTANO 4 ya KAMPENI za CCM ndani ya Kata hiyo – akianzia Kisiwani RUKUBA.

**VIPAUMBELE VIKUU VYA UTEKELEZAJI WA ILANI MPYA YA CCM NDANI YA KATA YA ETARO**

**(1) MAJI SAFI & SALAMA**

*Vijiji vya Mmahare, Etaro na Busamba vinasambaziwa MAJI ya MUWASA (Maji ya Mji wa Musoma kutoka Ziwa Victoria) na tayari uchimbaji wa mitaro na utandikaji wa mabomba umeanza. SERIKALI ya CCM inatekeleza AHADI yake ya USAMBAZAJI wa MAJI VIJIJINI.

*Kisiwa cha RUKUBA kiko kwenye Mradi wa Maziwa Makuu – kutumia Maji ya Ziwa Victoria.

**(2) UMEME VIJIJINI**

*Kisiwa cha RUKUBA kimeanza kutumia UMEME wa JUA (solar)

*VITONGOJI vya Vijiji 3 vilivyosalia vitapewa UMEME wa REA kama ilivyoainishwa ndani ya ILANI MPYA ya CCM ya 2020-2025.

**(3) ELIMU & MAFUNZO**

*Kata ya ETARO inayo SEKONDARI MOJA inayotumiwa na Vijiji 4. Haitoshi! SEKONDARI ya PILI ya Kata hiyo itajengwa Kijijini Busamba.

**(4) HUDUMA ZA AFYA**

*Kisiwa cha RUKUBA kitapanua ZAHANATI yake na kuwa KITUO cha AFYA. WODI ya MAMA & MTOTO inayojengwa Kisiwani hapo kwa kutumia MICHANGO ya WANANCHI & PROF MUHONGO, litakuwa (WODI) sehemu ya KITUO cha AFYA hicho.

*Kijiji cha MMAHARE kitakamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chake. WADAU wengi wa MAENDELEO, akiwemo PROF MUHONGO, wanachangia ujenzi wa ZAHANATI hii.

KURA ZA KATA YA ETARO – Wananchi wanasema:

*Dkt Magufuli: 100%
*Prof Muhongo:100%
*Ndg Kigwa: 100%

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

## ARI KUBWA YA WANAVIJIJI KUCHANGIA MAENDELEO YAO WAIWEKA PAZURI KATA YA MUGANGO – WANAANZA UJENZI WA MABWENI WAWE NA "HIGH SCHOOL" MWAKANI

Posted on October 12, 2020




*Tarehe 8.10.2020, MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO, alifanya MIKUTANO 2 ya KAMPENI ndani ya Kata ya Mugango.*

Mbali ya kunadi SERA za CCM, Prof Muhongo alijadili UTEKELEZAJI wa MIRADI ya KIPAUMBELE ya Kata hiyo – hii ikiwa ni sehemu ya matayarisho ya UTEKELEZAJI wa ILANI MPYA ya CCM baada ya UCHAGUZI wa tarehe 28.10.2020.

**KIPAUMBELE CHA ELIMU:**
KATA ya MUGANGO yenye Vijiji 3 (Kwibara, Kurwaki, Nyang'oma) inaanza KUTEKELEZA ILANI MPYA ya CCM (2020-2025) kwa KUJENGA MABWENI 3 ili mwakani (Julai 2021) iwe na Kidato cha V & VI.

Vilevile, Kata hiyo imeamua kujenga SEKONDARI ya PILI kwenye eneo la katikati ya Vijiji vya Kurwaki na Nyang'oma.

MAFANIKIO makubwa ya WANANCHI kukubali KUCHANGIA MAENDELEO YAO (nguvukazi & michango ya fedha taslimu) yako dhahiri:
*Vyumba vya Madarasa ya Shule zao za Msingi na Sekondari ya Mugango havina mirundikano ya Wanafunzi.
*MAABARA za Mugango Sekondari zinajengwa
*Vyoo vya kutosha vipo mashuleni
*Bustani za shule zipo

**KIPAUMBELE CHA AFYA:**
*KITUO cha AFYA cha Mugango tayari kimekamilika kwa USHIRIKIANO MZURI wa WANANCHI, Prof Muhongo na SERIKALI yao ya CCM

*ZAHANATI ya Kijiji cha Kurwaki itakamilishwa ikiwa ni moja ya MAFANIKIO ya UTEKELEZAJI wa ILANI MPYA ya CCM.

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

**ILANI MPYA YA CCM YAKUBALIKA SANA**

**MAJI VIJIJINI:**
Kata ya Mugango yenye CHANZO (Ziwa Victoria) cha BOMBA la MAJI ya Kiabakari na Butiama, itaendelea kupata MAJI kutoka kwenye BOMBA hilo la zamani ambalo limechakaa!

MRADI mkubwa wa Tsh Bilioni 70.5 wa BOMBA la MAJI la Mugango – Kiabakari – Butiama utaanza kutekelezwa hivi karibuni na VIJIJI vya Kata za MUGANGO na TEGERUKA vitapewa MAJI safi na salama kutoka kwenye BOMBA hili jipya.

**UMEME VIJIJINI**:
Kama ilivyoandikwa ndani ya ILANI MPYA ya CCM, WANANCHI wa Kata ya Mugango wana imani kubwa sana na SERIKALI ya CCM kukamilisha USAMBAZAJI wa UMEME kwenye Vitongoji vilivyosalia.

**IDADI YA KURA KUTOKA KATA YA MUGANGO**
*Dkt Magufuli: 100%
*Prof Muhongo: 100%
*Ndg Charles Magoma: 100%

**"TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA"**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# ILANI MPYA YA CCM INATOA MAJIBU YA KERO & VIPAUMBELE VYA WANANCHI WA KATA YA NYAMRANDIRIRA

Posted on October 12, 2020



*Kata ya Nyamrandirira ina Vijiji 5 (Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka) na kila KIJIJI kinakiri kwamba ILANI MPYA ya UCHAGUZI ya CCM (2020-2025) ndiyo pekee inatoa MAJIBU ya Kero na Vipaumbele vya MAENDELEO na USTAWI wa Vijiji vyao.*

Hayo yamebainika wakati wa MIKUTANO 4 ya KAMPENI ya Mgombea Ubunge wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO.

## ELIMU – SEKONDARI MPYA YA KATA

Vijiji vyote 5 vinachangia ujenzi wa SEKONDARI ya PILI ya Kata yao. SEKONDARI hii (Seka Secondary School) itafunguliwa Januari 2021.

## KIJIJI CHA MIKUYU

VIPAUMBELE vya Kijiji hiki ni MAJI, UMEME na ZAHANATI.
Ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao utaanza baada ya UCHAGUZI wa tarehe 28.10 2020 kwa kutumia NGUVUKAZI na MICHANGO ya Wanakijiji na Viongozi wao.

MAJI – Kijiji hiki kiko kwenye Mradi wa BOMBA la Maji ya kutoka Ziwa Victoria (Kijijini Chumwi) kwenda Mabui Merafuru na Mikuyu.

USANIFU wa awali unapitiwa upya na RUWASA kwani awali Vijiji vya Nyambono na Saragana vilikuwa ndani ya Mradi huu. Kwa sasa vijiji hivyo vimepelekwa kwenye Mradi wa Suguti – Wanyere/Chirorwe.

UMEME-Miundombinu ya usambazaji wa UMEME ipo na baadhi ya Wanavijiji tayari wameunganishiwa umeme. Kazi inaendelea na itakamilika kama isemavyo ILANI MPYA ya CCM.

**KIJIJI CHA CHUMWI**

VIPAUMBELE vya Kijiji hiki vinafanana na vile vya Kijiji cha Mikuyu kasoro Zahanati. UTEKELEZAJI wa Miradi yake ya MAJI & UMEME unafanana na ule wa Kijiji cha Mikuyu.

**KIJIJI CHA KASOMA**

MAJI ya Kijiji hiki yatatolewa Ziwa Victoria. Kijiji hiki kiko kwenye orodha ya Vijiji 33 vya Jimboni mwetu vilivyo kwenye Mradi wa MAZIWA MAKUU.

UMEME - ni kama ilivyoelezwa hapo juu kwenye Kijiji cha Mikuyu.

**VIJIJI VYA KABONI & SEKA**

MAJI ya Vijiji hivi yatatolewa kwenye BOMBA la MAJI la MGODI wa SEKA ambalo chanzo chake kiko Kijijini Kaboni. Baadhi ya Wanavijiji tayari wanahudumiwa na Bomba hili.

UMEME – Baadhi ya Wanaviviji ndani ya Vijiji hivi viwili tayari wameunganishiwa umeme. Vitongoji vilivyosalia vitapewa UMEME na kazi ya usambazaji inaendelea.

ELIMU – Kijiji cha KABONI kinashughulikia suala ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa SHULE ya MSINGI yao. Kijiji hakina Shule ya Msingi.

MGOMBEA URAIS WA CCM (DKT MAGUFULI) ameahidiwa KURA ZOTE (100%) kutoka Kata Nyamrandirira

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# ILANI MPYA YA CCM IMEBEBA VIPAUMBELE VYA MAENDELEO YA KATA YA TEGERUKA

Posted on October 12, 2020




Tarehe 9.10.2020, MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO, alikuwa na MIKUTANO ya KAMPENI kwenye VIJIJI 2 (Mayani & Tegeruka) vya Kata ya TEGERUKA. Hapo awali alishafanya MKUTANO wa KAMPENI kwenye KIJIJI cha Kataryo.

VIPAUMBELE vya MAENDELEO ya Vijiji hivyo 3 vya Kata hiyo vimo kwenye ILANI MPYA ya UCHAGUZI ya CCM ya 2020-2025. Kwa hiyo, UTEKELEZAJI unaanza mara moja baada ya UCHAGUZI wa tarehe 28.10.2020.

**MAJI KWA VIJIJI VYOTE VYA KATA YA TEGERUKA**

*SERIKALI ya CCM inao MRADI wa Tsh BILIONI 70.5 wa MAJI ya BOMBA ya Ziwa Victoria – Mugango – Kiabakari – Butiama. VIJIJI vyote 3 vya Kata ya TEGERUKA nitapata MAJI kutoka kwenye Bomba hili.

*FEDHA za MRADI huu zimetolewa na Serikali ya Saudi Arabia, BADEA (Khartoum, Sudan) na Serikali yetu. Mradi utaanza Januari 2021 au kabla.

**UMEME KWA VIJIJI VYOTE VYA KATA YA TEGERUKA**

*Kwa kuwa UMEME tayari unatumiwa na baadhi ya WAKAZI wa VIJIJI 3 vya Kata hii, WANANCHI wana imani kubwa na SERIKALI ya CCM kukamilisha USAMBAZAJI uliosalia – na hili nalo limo ndani ya ILANI MPYA ya CCM.

**KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SEKONDARI YA KATA**

*Ujenzi wa MAABARA, MAKTABA, n.k kwenye Tegeruka Sekondari unaendelea.

**KIJIJI CHA KATARYO:**

WANANCHI wameamua kujenga:
*ZAHANATI ya Kijiji chao
*SHULE SHIKIZI Nyasaenge

**VIJIJI VYA MAYANI & KATARYO:**

*WANANCHI wameamua kujenga SEKONDARI ya PILI ya Kata itakayojengwa katikati ya Vijiji hivyo viwili. Ujenzi unaanza tarehe 1.11.2020

KAMPENI ZA UCHAGUZI za Jimbo la Musoma Vijijini ni KAMPENI za MATAYARISHO ya UTEKELEZAJI wa ILANI MPYA ya CCM (2020-2025)

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

KURA ZA KATA YA TEGERUKA – Wananchi wamesema:
*Dkt Magufuli: 100%
*Prof Muhongo: 100%
*Ndg Mashauri: 100%

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# MIKUTANO 3 YA KAMPENI NDANI YA KATA YA NYAMBONO YAMKUBALI SANA DKT MAGUFULI

Posted on October 7, 2020




*Leo, Jumanne, 6.10.2020 MGOMBEA UBUNGE wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini, PROF MUHONGO ameenda Kijijini Nyambono, Kijijini Saragana na kwenye Kitongoji cha Nyabherango KUOMBA KURA za WAGOMBEA wa CCM wa nafasi za Urais, Ubunge na Udiwani.*

DKT MAGUFULI anakubalika kwa asilimia mia moja (100%). SABABU KUU zikiwa:

**(i) MAJI YA ZIWA VICTORIA**

Vijiji 2 vya Kata ya Nyambono (Saragana & Nyambono) viko mbali na Ziwa Victoria na hivi karibuni vitapata MAJI ya Ziwa hilo kupitia MRADI wa BOMBA la MAJI wa Suguti-Wanyere/Chirorwe ambapo BOMBA hilo litapaleka MAJI kwenye Vijiji hivyo. Ujenzi wa TENKI kubwa la MAJI kwenye Mlima Nyabherango utaanza hivi karibuni (Bajeti ya Mwaka huu).

**(ii) UMEME WA REA:**

Vitongoji vya Kata hiyo vilivyosalia vitapewa umeme – ILANI MPYA ya CCM (2020-2025) imebainisha hivyo.

## VIPAUMBELE MAALUM

### KIJIJI CHA NYAMBONO

WANANCHI wa Kijiji hiki WAMEAMUA kwa KAULI moja kwamba kwa MIAKA 5 ya UTEKELEZAJI wa ILANI ya CCM (2020-2025) watajenga SEKONDARI yao. Kwa sasa WATOTO wao wanatembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 6 kwenda masomoni kwenye SEKONDARI ya NYAMBONO iliyoko Kijijini Saragana.

Vilevile, WANANCHI hawa na WADAU wao wa MAENDELEO watakamilisha ujenzi wa ZAHANATI ya Kijiji chao.

WATOTO wa Kitongoji cha Nyabherango wanaenda masomoni kwenye SHULE za MSINGI za mbali na kwao (zaidi ya kilomita 5). Kitongoji hicho kinatafuta ardhi kianze kujenga SHULE SHIKIZI.

### KIJIJI CHA SARAGANA

Kitongoji cha Kabise kitajenga SHULE SHIKIZI kutatua tatizo sugu la mwendo mrefu ambao WATOTO wao wanaotembea kwenda masomoni kwenye SHULE za MSINGI za vitongoji vingine.

*MIRADI MINGINE ni kama ilivyoainishwa kwenye ILANI MPYA ya CCM ya 2020-2025.

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# WANANCHI WA KATA YA MUSANJA WATOA VIPAUMBELE VYAO KWA MIAKA 5 YA UTEKELEZAJI WA ILANI MPYA YA CCM (2020-2025)

Posted on October 5, 2020



*Ijumaa, tarehe 2.10.2020, KATA ya MUSANJA yenye VIJIJI 3 (Mabui Merafuru, Musanja na Nyabaengere) ilikuwa kwenye KAMPENI za UCHAGUZI za Chama cha Mapinduzi (CCM)*

WAGOMBEA UBUNGE (Prof Sospeter Muhongo) na UDIWANI (Ndugu Ernest Mwira) wa CCM walinadi SERA na MIRADI ya MAENDELEO iliyoko kwenye ILANI MPYA (2020-2025) ya Chama chao.

MIKUTANO 2 ya KAMPENI ilifanywa kwenye VIJIJI 2 (Musanja & Mabui Merafuru).

WANANCHI WALIVUTIWA SANA na SERA za CCM na kuahidi kutoa KURA ZOTE kwa WAGOMBEA wa CCM kwa nafasi ya URAIS (Dkt Magufuli), UBUNGE (Prof Muhongo) na UDIWANI (Ndg Ernest John Mwira).

**MIRADI YA KIPAUMBELE YA KATA YA MUSANJA NI:**
*Kukamilishwa kwa usambazaji wa UMEME kwenye Vitongoji vilivyosalia

*Kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa MAJI ya kutoka Ziwa Victoria (Chumwi, Kata ya Nyamrandirira) hadi Mabui Merafuru (Kata ya Musanja). Wataalamu walishakamilisha USANIFU wa Mradi huu.

*Ukamilishaji wa ujenzi wa SHULE Shikizi Gomora na kuipanua iwe Shule ya Msingi inayojitegemea.

*Kujenga ZAHANATI 1 kwenye Kijiji 1 kati ya Vijiji 3. Kwa sasa Kata ya Musanja inatumia Kituo cha Afya ya Murangi.

*Kujenga SEKONDARI kwenye Kijiji cha Musanja ambacho kiko mbali na Sekondari ya Kata iliyoko Kijiji cha Mabui Merafuru

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

**“TUMETEKELEZA KWA KISHINDO, TUNASONGA MBELE KWA PAMOJA”**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

## CHAGUENI CCM NCHI IZIDI KUNG'ARA – SHAIRI KUTOKA KIJIJI CHA KASOMA

Posted on September 26, 2020



*WANANCHI wa Kata ya Nyamrandirira yenye VIJIJI 5 wamewaomba Prof SOSPETER MUHONGO (Mgombea Ubunge) na Mwl NYEOJA WANJARA (Mgombea Udiwani) waungane nao tarehe 5 Novemba 2020 kukamilisha MAJENGO ya AWALI yanayohitajika ili SEKA SEKONDARI ifungiliwe Januari 2021.*

VIJIJI 5 (Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka) vya Kata ya Nyamrandirira vinayo SEKONDARI MOJA (Kasoma Secondary School) ambayo kwa sasa imeelemewa na WINGI wa WANAFUNZI kutoka kwenye vijiji hivyo. WANAFUNZI wengine wanatembea mwendo wa zaidi ya kilomita 10 kwenda masomoni Kasoma Sekondari.

Kwa hiyo, KATA hiyo imeamua kuanza KUTEKELEZA ILANI MPYA YA CCM (2020-2025) kwa KUKAMILISHA UJENZI wa MIUNDOMBINU INAYOHITAJIKA kwa ufunguzi wa SEKONDARI yao mpya (Seka Secondary School) inayojengwa Kijijini Seka.

Shairi kutoka Kijiji cha Kasoma lilitoa burudani kubwa kwenye kampeni hii.

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# MIRADI YA MAENDELEO YA KATA YA NYAKATENDE ITAKAMILISHWA NA CCM

Posted on September 25, 2020



*Kampeni za CCM kwenye Kata ya Nyakatende.*

Jumanne, 22.9.2020, WANANCHI wa Kata ya NYAKATENDE waliamua wazi wazi kwamba kwenye Kata yao yenye VIJIJI VINNE (Kakisheri, Kamuguruki, Kigera na Nyakatende) KURA zote zitaenda CCM.

SEKONDARI ya PILI (Kigera Secondary School) inayojengwa Kijijini Kigera imepangwa ifunguliwe mwakani (Januari 2021). MAJENGO muhimu ya awali yanaezekwa na WANANCHI wanayo imani kubwa sana na WAGOMBEA wa CCM wa nafasi za URAIS, UBUNGE na UDIWANI kwamba ndio wenye uwezo na kutoa ushirikiano wa SEKONDARI hiyo mpya ifunguliwe Januari 2021.

KIJIJI cha Kakisheri kinajenga ZAHANATI yake. HALMASHAURI ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) imepanga kujenga KITUO cha AFYA kwenye Kata hiyo kwa kutumia MICHANGO na NGUVUKAZI ya WANANCHI wa Kata hiyo.

WANANCHI wanasema MIRADI hii na mingine ya MAENDELEO (k.m. usambazaji wa MAJI na UMEME) itakamilishwa kwa ushirikiano na SERIKALI ya CCM.

UAMUZI wa KATA ya NYAKATENDE ni huu – “KURA ZOTE kwa MAGUFULI (Urais), MUHONGO (Ubunge) na MARERE (Udiwani).”

**VITENDO KWANZA**
**MAENDELEO KWANZA**

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# CCM YAENDELEA KUNG'ARA NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on September 22, 2020



*Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa akiteta jambo na Prof Muhongo*

Jumatatu, 21.9.2020, Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa MAJALIWA amepiga KAMPENI yenye MAFANIKIO MAKUBWA ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Mhe Waziri Mkuu ameelezea MAFANIKIO MAKUBWA yaliyopatikana kwenye UTEKELEZAJI wa ILANI ya CCM ya 2015-2020 chini ya UONGOZI na USIMAMIZI wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt John Joseph Pombe MAGUFULI

Mhe Waziri Mkuu ametoa maelezo ya kina juu ya UTEKELEZAJI wa ILANI mpya ya CCM ya 2020-2025 na kuwadhibitishia WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini kwamba MIRADI ya MAENDELEO ya Jimbo hilo ITATEKELEZWA na KUKAMILISHWA na SERIKALI ya CCM chini ya UONGOZI wa Mhe Dkt John Joseph Pombe MAGUFULI.

MIRADI ya MAENDELEO ya Jimbo la Musoma Vijijini INAYOTEKELEZWA kwa USHIRIKIANO wa SERIKALI na WANANCHI wa Jimbo hilo ni mingi mno ikiwemo ya ujenzi wa barabara ya lami ya Musoma-Makojo-Busekera, Hospital ya Wilaya, Zahanati mpya na Vituo vya Afya vipya, Sekondari mpya, ukamilishaji wa usambazaji wa MAJI na UMEME vijijini, upanuzi

wa kilimo cha umwagiliaji, n.k. MIRADI mipya imo ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri Kijijini Suguti, n.k.

Waziri Mkuu amekabidhi ILANI ya UCHAGUZI ya CCM ya 2020-2025 kwa Mgombea Ubunge (Prof Muhongo) wa CCM wa Jimbo la Musoma Vijijini.

Prof Muhongo amesema kwamba WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini, kwa KUSHIRIKIANA na SERIKALI yao ya CCM, wataanza KUTEKELEZA ILANI mpya ya CCM ya 2020-2025 kuanzia tarehe 1.11.2020. Muhtasari wa MIRADI ya Jimbo hilo imekabidhiwa kwa Mhe Waziri Mkuu.

Mhe Waziri Mkuu ameshuhudia UTAYARI na MWITIKIO mkubwa wa WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini wa KUTOA KURA NYINGI SANA kwa MGOMBEA URAIS wa CCM, Mhe Dkt John Joseph Pombe MAGUFULI.

SHUKRANI nyingi zimetolewa kwa WAZIRI MKUU, Mhe Kassim Majaliwa MAJALIWA kwa kuwahutubia WANANCHI Kijijini Bukima, Kijijini Suguti (Kusenyi), Kijijini Kwikuba, Kijijini Mugango na Kijijini Mkirira. AMEFANIKIWA SANA kuwaombea KURA WAGOMBEA wa CCM wa nafasi za URAIS, UBUNGE na UDIWANI.

WANANCHI wa JIMBO la Musoma Vijijini WAMEAHIDI kupiga kura, bila kukosa, tarehe 28.10.2020 na kupata USHINDI MKUBWA MNO kwa CHAMA cha MAPINDUZI (CCM).

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

## JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI – ILANI MPYA YA UCHAGUZI YA CCM (2020-2025) KUANZA KUTEKELEZWA TAREHE 1 NOVEMBA 2020

Posted on September 19, 2020



*Prof MUHONGO akiwa na BODABODA wa Kijiji cha Kataryo*

WANANCHI wa Kata ya TEGERUKA WAMEAMUA kujenga SEKONDARI ya PILI ili kutatua tatizo la mwendo mrefu wanaotembea WANAFUNZI wa SEKONDARI wa Kata hiyo.

KATA hiyo yenye VIJIJI 3 (Kataryo, Mayani & Tegeruka) vilivyo mbali mbali ina SEKONDARI moja. WANAFUNZI kutoka Vijiji vya Kataryo na Mayani wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 15 kwenda masomoni TEGERUKA SEKONDARI.

Tarehe 1.11.2020, WANANCHI wanaanza ujenzi wa SEKONDARI ya PILI ya Kata yao itakayojengwa eneo lililo katikati ya Vijiji vya Kataryo na Mayani. WAGOMBEA UBUNGE (Prof S Muhongo) na UDIWANI (Askofu Modekaye Mashauri) WAMEKUBALI KUSHIRIKIANA na WANANCHI hao kujenga Sekondari hiyo.

WANANCHI wa Kata ya Kataryo WAMEFURAHI na KUSHUKURU sana SERIKALI yao baada ya kuambiwa kwamba MRADI wa BOMBA la MAJI kutoka Ziwa Victoria (Mugango) kwenda Kiabakari na Butiama litakuwa na MATOLEO ya MAJI ndani ya VIJIJI vyote VITATU vya Kata hiyo. MRADI huo utagharimu TSH BILIONI 70.5 ambazo ZIMEISHATOLEWA na Serikali ya SAUDI ARABIA, BADEA na SERIKALI yetu. Utekelezaji wake unaanza hivi karibuni.

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI – USAMBAZAJI WA MABANGO, VIPEPERUSHI & VITABU VYA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA ILANI ILIYOPITA

Posted on September 11, 2020



*Usambazaji wa MABANGO & VIPEPERUSHI vya CCM ndani ya Vijiji vyote 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini.*

(1) MABANGO 4,000 (elfu nne) ya MGOMBEA URAIS wa CCM, Mhe Rais Dkt John Joseph Pombe MAGUFULI yanasambazwa ndani ya Vijiji vyote 68.

(2) VIPEPERUSHI 5,000 (elfu tano) vyenye Muhtasari wa MIRADI itakayotekelezwa (2020-2025), vinasambazwa. MIRADI hii inatokana na ILANI mpya ya UCHAGUZI ya CCM ya 2020-2025.

(3) VIPEPERUSHI 5,000 (elfu tano) vya Muhtasari wa WASIFU wa MGOMBE UBUNGE, Prof Sospeter Mwijarubi MUHONGO, vinasambazwa.

(4) VITABU 10,000 (Volume I & II) vyenye TAARIFA za Utekelezaji wa ILANI ya UCHAGUZI ya CCM ya 2015-2020, usambazaji wake utafikia tamati tarehe 1.10.2020

(5) VIPEPERUSHI 4,200 (elfu nne mia mbili) vya kuvaa shingoni vya WAGOMBEA UDIWANI 21 (@200) wa CCM vinaanza kusambazwa kesho (9.9.2020). Mgombea Ubunge, Prof Muhongo amewatengenezea vipeperushi hivyo.

(6) BENDERA za CCM 500 (400 kutoka Chamani Dodoma & 100 za Mgombea Ubunge) zinagawiwa.

**UZINDUZI WA KAMPENI ZA CCM ZA WILAYA YA CCM YA MUSOMA VIJIJINI**

**Mahali:**
Bwai Kwitururu, Kata ya Kiriba

Sospeter Muhongo
Jimbo la Musoma Vijijini

# PROF MUHONGO ARUDISHA FOMU ZA MAOMBI YA KUGOMBEA NAFASI YA UBUNGE WA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on July 18, 2020



*Ijumaa, 17.7.2020, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Peter Francis Mashenji ALIPOKEA FOMU za Prof Sospeter Muhongo za kuomba kugombea nafasi ya UBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini.*

Prof Muhongo alisindikizwa na WASAIDIZI wake 5 {4 wanaotembelea Wanavijiji kila siku wakitumia PIKIPIKI na Dreva 1}. Wasaidizi wengine 3 wako masomoni ambao ni: Webmaster (1) na Wasoma taarifa kwenye On-line Radio (2).



# PROF MUHONGO ACHUKUA FOMU YA KUWANIA UTEUZI WA CCM KWA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on [July 16, 2020]



*Jumatano, tarehe 15.7.2020, Ndugu Peter Francis Mashenji, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Musoma Vijijini ALIMKABIDHI Prof Sospeter Muhongo FOMU YA CCM YA UCHAGUZI.*



*Prof Muhongo akiwa na WASAIDIZI wake 4 (ametekeleza nao Ilani ya CCM ya 2015-2020, kwa muda wa miaka 5), baada ya kuchukua FOMU YA UCHAGUZI (15.7.2020).*

# MENGINEYO

## (30 Juni 2021 – 1 Julai 2020)

# WASAIDIZI 6 WA MBUNGE WA JIMBO WANUNULIWA PIKIPIKI MPYA 6

Posted on March 4, 2021




*Tukio la ununuaji na upokeaji wa PIKIPIKI MPYA 6 za Wasaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini.*

Jumatano, tarehe 3 Machi 2021, MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo AMEWANUNULIA WASAIDIZI wake PIKIPIKI MPYA 6 na kuwazawadia PIKIPIKI za ZAMANI walizokuwa wanazitumia.

JIMBO la Musoma Vijijini lina KATA 21 zenye VIJIJI 68 na VITONGOJI 374.

WASAIDIZI wa MBUNGE wamegawiwa maeneo yao ya kazi na KILA JUMAMOSI Ripoti za kazi zao za wiki lazima Mbunge huyo apewe.

Kwa hiyo, WANAVIJIJI wanafuatwa huko huko VIJIJINI mwao na hawana sababu ya KUFUNGA SAFARI kwenda kumtafuta Mbunge, badala yake wao (wanavijiji) ndio wanatembelewa kwenye makazi

yao au sehemu zao za kazi za kiuchumi na kwenye miradi ya maendeleo.

Mbunge huyo ametoa VITENDEA KAZI vifuatavyo:

*Pikipiki tokea Mwaka 2015
*Mafuta ya Pikipiki kila wiki
*Smartphone & Bando
*Laptop
*GPS

Vilevile, Wasaidizi wa Mbunge huyo wanapewa BONUS ya kila mwisho wa Mwaka.

**KARIBUNI TUJENGE MUSOMA VIJIJINI**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SHEREHE ZA EID AL FITR NA MIRADI YA MAENDELEO YA MUSOMA VIJIJINI

Posted on May 16, 2021



*EID AL FITR mwaka huu ya Musoma Vijijini iliyofanyika kwenye MISIKITI 3 ya VIJIJI vya Bukima, Kiriba na Kakisheri/Kigera.*

EID AL FITR ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini husherehekewa KILA MWAKA kwa MISIKITI 3 kuandaa sikukuu hiyo. Jumla ya Misikiti Jimboni mwetu ni 37.

Kwa MWAKA HUU (2021) mzunguko wa MISIKITI 3 wa kila Mwaka umetua kwenye MISIKITI ya VIJIJI vya:
*Bukima
*Kiriba
*Kakisheri/Kigera

MADHEHEBU YA KIKRISTO nayo husherehekea KRISMASI na PASAKA kwa mtindo huu huu wa mzunguko ndani ya VIJIJI 68 vya JIMBO la Musoma Vijijini.

UTARATIBU huu wa kuwaweka WANANCHI pamoja wakati wa SHEREHE za KIDINI na wakati wa KAZI za kujiletea MAENDELEO yao ni sehemu ya MPANGOKAZI wa MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo.

**MASHINDANO YA KUHIFADHI QURAAN**

*WAISLAMU wa Jimbo la Musoma Vijijini wameamua kutayarisha MASHINDANO hayo kwa kushirikiana na Mbunge wao wa Jimbo. Tarehe itapangwa.

SHEREHE za KIDINI, mbali ya kufanyika kwa TAFRIJA za pamoja, hutumika KUKUMBUSHANA UTEKELEZAJI ya MIRADI ya MAENDELEO ya KATA iliyoandaa SHEREHE kwa Mwaka huo.

**(1)EID AL FITR KWENYE MSIKITI WA KIJIJI CHA BUKIMA**

WANANCHI wamekumbushwa na kuhimizwa kukamilisha MIRADI ifuatayo:

(a) Wodi ya Mama&Mtoto ya Zahanati ya Bukima

(b) Ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa kwenye Shule zote za Msingi na Sekondari yao.

(c) Kasi iongezwe kwenye ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Butata

**(2) EID AL FITR KWENYE MSIKITI WA KIJIJI CHA KIRIBA**

WANANCHI wamekumbushwa na kuhimizwa kukamilisha MIRADI ifuatayo:

(a)Ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa na Ofisi za Walimu wa S/M Kiriba B. Shule hii inahama kutoka kwenye eneo la pamoja na S/M Kiriba A

(b)Kasi ya ukamilishaji wa Maabara, Vyumba vipya vya Madarasa na Jengo la Utawala la Kiriba Sekondari iongezeke.

(c) Kitongoji cha Kubuingi cha Kijiji cha Kiriba kianze ujenzi wa SHULE SHIKIZI. Watoto wao wanatembea umbali mrefu kwenda masomoni kwenye S/M Kiriba A&B

**(3) EID AL FITR KWENYE MSIKITI WA VIJIJI VYA KAKISHERI NA KIGERA**

*Vijiji 2 hivi vinatumia Msikiti mmoja ambao unaendelea kujengwa kwa msaada mkubwa wa MAMA DIBOGO wa Musoma Mjini.

*Ujenzi wa Jengo la Madrasa utaanza hivi karibuni.

WANANCHI wamekumbushwa na kuhimizwa kukamilisha MIRADI ifuatayo:

(a) Kuongeza kasi ya ujenzi na ukamilishaji wa SEKONDARI MPYA, ya kisasa, (imefunguliwa mwaka huu – Kigera Secondary School) inayojengwa na Vijiji hivi viwili.

(b) Kasi iongezwe kwenye ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kakisheri

**MIRADI INAYOFADHILIWA NA SERIKALI**

Mbali ya kutoa mkono wa EID AL FITR, Mbunge wa Jimbo hilo ameongea na WANANCHI na kuwaelezea MIRADI mbalimbali (k.m. elimu, afya, maji, umeme, barabara za TARURA & TANROADS) itakayotekelezwa na SERIKALI kwa kutumia BAJETI ya Mwaka wa Fedha ujao, Mwaka 2021/2022.

Vilevile, MBUNGE huyo amesikiliza kero za Wananchi na kuzitatua.

**SHEREHE NA MAENDELEO MUSOMA VIJIJINI**

**TUENDELEE KUSHIRIKIANA NA SERIKALI YETU KUCHANGIA MAENDELEO YETU – TUTAFANIKIWA!**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## HITIMISHO

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 unaenda vizuri Jimboni mwetu, na mafanikio yake yanaonekana na kuthaminiwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Wanavijiji wanashirikiana na Serikali yao ya ngazi mbalimbali kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji ya jamii zao.

Taarifa hii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo letu ni ya mwaka mmoja wa fedha, yaani kuanzia tarehe 1 Julai 2020 hadi 30 Juni 2021. Uongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali yake ulibadilika ndani ya kipindi hiki. Nafasi ya Hayati Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli ilichukuliwa kuanzia tarehe 19.3.2021 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ndani ya kipindi hiki (1 Julai 2020-30 Juni 2021) imeibuliwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025), ambamo ndimo tulitoa vipaumbele vyetu vitano vya maendeleo.

Miradi yetu ya maendeleo ni endelevu, kwani inaibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano ambavyo ni endelevu, na nyenzo kuu za utekelezaji wake ambazo nazo zinaendelea kuhitajika kwa ustawi wa jamii yetu.

Vipaumbele vyetu ni: (i) elimu, (ii) afya, (iii) kilimo, uvuvi na ufugaji, (iv) tabianchi na mazingira, na (v) michezo na utamaduni. Nyezo kuu zinazohitajika kwenye utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vyetu ni maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, raslimali watu na taasisi za fedha na uchumi.

Ahadi za Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali yake zilizotolewa kwa wananchi wa Musoma Vijijini, chini ya uongozi wa Hayati Dkt John Joseph Pombe Magufuli, na baadae Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, zinaendelea kutekelezwa ikiwemo ahadi ya ujenzi wa barabara la Musoma-Makojo-Busekera (km 92) kwa kiwango cha lami.

Ahadi za Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, zimetekelezwa na kuvuka malengo yaliyowekwa kwa mwaka huu mmoja (1 Julai 2020-30 Juni 2021). Michango ya Mbunge huyu ni mingi na mikubwa kama inavyoainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, anaendelea kushirikiana kwa ukaribu sana na wananchi, viongozi wa Chama (CCM) na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye utekelezaji wenye mafanikio makubwa wa Ilani ya Uchaguzi (2020-2025) Jimboni mwetu.

Vilevile, Mbunge huyu anaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Chama chetu (CCM) kwa ngazi zote, yaani, kwenye Matawi, Kata, Wilaya (Musoma Vijijini), Mkoa (Mara) na Taifa (Tanzania).

## SHUKRANI

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini na viongozi wao wa ngazi za Vitongoji (374), Vijiji (68) na Kata (21), na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, wanatoa shukrani nyingi za dhati kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt John Joseph Pombe Magufuli kwa uwezeshaji na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2020 hadi mauti ilipompata tarehe 17.3.2021.

Baada ya kifo cha Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan alijaza nafasi ya U-Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti CCM Taifa. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 19.3.2021 hadi 30.6.2021, kiongozi mkuu kabisa wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM alikuwa Mhe Dkt Rais Samia Suluhu Hassan - Jimbo la Musoma Vijijini linamshukuru sana Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Mhe Dkt Philip Isdor Mpango kwa uwezeshaji na uongozi mzuri kwenye miradi ya maendeleo ya Jimboni mwetu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Serikali ya Mapinduzi, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Philipo Mangula, na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Mhe Dkt Bashiru Ally nao wanapewa shukrani nyingi za dhati kwa usimamizi wao mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu (CCM) kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja (1 Julai 2020-30 Juni 2021).

Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, na viongozi wengine wote wa ngazi mbalimbali za Serikali yetu wanapewa shukrani nyingi za uwezeshaji na ushirikiano wao kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja (1 Julai 2020 – 30 Julai 2021), utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Jimboni mwetu) ya Ilani ya

Uchaguzi ya CCM ulisimamiwa vizuri ki-Serikali na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhe Adam Malima, na Mkuu wa Wilaya yetu (Musoma) Mhe Dkt Vicent Naano Anney. Tunawashukuru wao na wafanyakazi wengine wote.

Shukrani nyingi pia zinatolewa kwa viongozi mbalimbali wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kuanzia ngazi za Tawi, Kata, Wilaya hadi Mkoa (Mara). Baadhi yao ni Mlezi wa Mkoa ki-Chama, Ndugu Kheri James, M-NEC Mkoa, Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Mkoa, Ndugu Samwel Kiboye, Katibu wa Mkoa, Ndugu Shaibu Ngatiche. Wengine ni Mweyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Nyabukika Bwire Nyabukika na Katibu wa Chama Wilaya, Ndugu Peter Francis Mashenji.

Waheshimiwa Madiwani wote 28 wa kuchagulia na wa Viti Maalumu, na wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) wanapewa shukrani za dhati kwa utimizaji wa wajibu wao kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu (CCM) ndani ya mwaka huu mmoja.

Shukrani nyingi inapewa RUWASA kwa kufufua miradi iliyokwama kwa miaka kadhaa, na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya usambazaji wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria na uchimbaji wa visima virefu vya maji vijijini mwetu.

TARURA na TANROADS wanaendelea kuboresha barabara zetu ambazo zinapitika kwa urahisi kwa majira yote ya mwaka.

Vyanzo vya fedha na vifaa vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini mwetu iliyobuniwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya mwaka huu mmoja wa fedha (1 Julai 2020 - 30 Juni 2021) ni vingi vikiwemo: Serikali Kuu na miradi yake kama vile EQUIP, EP4R, Wadau wa Maendeleo (PCI Tanzania na BMZ Germany), Benki za NBC, NMB na CRDB.

Mbunge wa Jimbo ametoa michango mingi na mikubwa kuchangia utekelezaji wa miradi inayoelezwa ndani ya kitabu hiki. Wanavijiji

wamechangia nguvukazi na fedha taslimu. Baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini wametoa michango yao na majina yao yametajwa ndani ya kitabu hiki. Michango kutoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ya Jimboni mwetu imeainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo anapenda kuwashukuru watu mbalimbali wenye fani mbalimbali anaofanya nao kazi za Jimbo la Musoma Vijijini. Orodha ni ndefu na kwa uwakilishi anawashukuru wawakilishi wao ambao ni Mtendaji Mkuu (Webmaster) wa Tovuti ya Jimbo letu (www.musomavijijini.or.tz), Dkt Isack Kambira.

Wengine wanaopewa shukrani ni Waandishi wa Habari wakiwakilishwa na Ndugu Sadick Hunga, John Makali na Shomari Binda. Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wanapewa shukrani nyingi kwa kazi zao nzuri - hao ni Vaileth Peter, Fedson Masawa, Verediana Mgoma na Hamisa Gamba.

Shukrani za kipekee na za muhimu sana zinapewa WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao kwa utashi wao wenyewe wameamua kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025. Miradi ya maendeleo inayotekelezwa vijijini mwao inabuniwa, inachangiwa (nguvukazi na fedha taslimu), inatekelezwa na inatunzwa na wao wenyewe.

Vilevile, wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanashirikiana vizuri sana na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa makubwa ya ukuaji, uimarikaji wa uchumi, na ustawi wa Jimbo lao la Musoma Vijijini.

Kitabu hiki kimetayarishwa na:
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini

**Prof. Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo**
Officier, Ordre des Palmes académiques
FGSAf, FAAS, MASSAf, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE, FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol

**Homepage/Tovuti:**
www.musomavijijini.or.tz

**Telephone/Simu:**
+255 754 400 800

**Date/Tarehe:**
30 Juni 2021